# KUINGILIANA NA KUJALIZANA KATIKA FUMO LIYONGO, KIFO KISIMANI NA MSTAHIKI MEYA

**DANIEL KIOKO NGUNZI**

**Tasnifu hii Imewasilishwa Katika Shule ya Mafuzu ili Kutosheleza Baadhi ya Mahitaji ya Shahada ya Uzamili Katika Kiswahili, Chuo Kikuu cha Egerton.**

**CHUO KIKUU CHA EGERTON**

**NOVEMBA, 2019**

## UNGAMO NA IDHINI

**Ungamo**

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijatolewa kutahiniwa kwa mahitaji ya shahada yoyote katika chuo chochote kile.

**Sahihi …………………………** **Tarehe ………………………**

**Daniel Kioko Ngunzi**

**ASM12/3764/14**

**Idhini**

Tasnifu hii imewasilishwa kwa idhini yetu kama wasimamizi na washauri walioteuliwa rasmi na Chuo Kikuu cha Egerton.

**Sahihi …………………….** **Tarehe …………………………..**

**Dkt. Mayaka Gwachi,**

**Idara ya Lugha, Fasihi na Isimu-jamii,**

**Chuo Kikuu cha Laikipia.**

**Sahihi………………………** **Tarehe………………………………**

**Dkt. Abdulraim Hussein Taib Ali,**

**Idara ya Fasihi, Lugha na Isimu,**

**Chuo Kikuu cha Egerton.**

**HAKILINZI**

**©2019, Ngunzi Kioko**

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kupiga chapa, kutafsiri au kuitoa tasnifu hii kwa njia yoyote ile bila idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu cha Egerton.

## TABARUKU

Tasnifu hii ninaitabarukia mke wangu mpendwa Ruth Kasyoka. Amejitolea mhanga kuhakikisha kuwa nimekamilisha elimu yangu pamoja na binti zangu Blessing Museo Tiana Mutanu na wazazi wangu: Bw. Ngunzi, Bi. Florence Mutio na Bi Annah Mutua. Wamenivumilia kwa muda ambao sikuweza kushirikiana nao kwa mambo mengi waliponihitaji. Waliniwezesha kutambua umuhimu wa masomo katika maisha yangu.

## SHUKRANI

Safari ndefu huanza kwa hatua moja. Siwezi kujigamba na kudai kuwa ni bidii zangu pekee ambazo zimeniwezesha kufanikiwa. Nitakuwa ninakosea nisipowatambua walionisaidia kufanikisha kazi hii kwa kunipa moyo, kunielekeza na hata kunisaidia nilipowahitaji. Inabidi kuwatambua walionisaidia nilipojikwaa na kunipa ushauri.
Kwanza kabisa ninamshukuru Mola kwa kunipa afya njema na nguvu za kukamilisha kozi hii. Umbali huu ninasema kuwa Yeye ni Ebeneza. Nashukuru chuo Kikuu cha Egerton kwa kunipa nafasi ya kujiendeleza kimasomo. Shukrani za dhati ni kwa wasimamizi wangu, Dkt. Mayaka Gwachi na Dkt. Abdurahim Hussein Taib Ali. Wamekuwa zaidi ya walimu nilipowashirikisha ili kufanikisha kazi hii. Sitasahau ushauri wao maishani. Rabuka awabariki zaidi.

Wahadhiri katika idara ya Fasihi, Lugha na Isimu katika chuo Kikuu cha Egerton wanastahili shukrani zangu za dhati. Michango yao wa kimaarifa yamenisaidia pakubwa sana katika maisha yangu ya  kimasomo. Ni mengi ambayo wamenijuza katika vikao mbalimbali vilivyo rasmi na visivyokuwa rasmi. Wahadhiri hawa ni: Dkt. Bartoo, Dkt. Kweya, Dkt. Walunywa, Dkt. Gacheiya, Dkt. Khaemba, Dkt. Mayaka na Dkt. Taib.

Sitasahau wanafunzi wenzangu tuliokuwa nao chuoni. Walinitia moyo na kushauriana nao katika kuboresha kazi hii. Miongoni mwao ni Nancy Kones, Ben Imire na Shem Nyakundi, Judy Kawira na Janice Mwikali. Asanteni kwa kunifaa katika mijadala na kunishauri. Mungu awabariki pia.

Mwisho, namshukru kwa mke wangu Bi. Ruth Kasyoka. Amekuwa rafiki wa karibu wa kunishauri na kunipa ari nilipovunjika moyo. Amenifaa kifedha kufanikisha kuyakidhi mahitaji yangu. Asante sana mke wangu na Mungu akubariki pia. Ninawashukuru wazazi wangu Bw. Ngunzi na Bi. Florence Mutio Nguzi, na Bi. Annah Mutua kwa unipa ushauri na motisha ya kuendelea na masomo. Ninawashukuru ndugu zangu Bon, Joseph, Peter na Dadangu Joyce. Hakika sikuweza kutaja kila mmoja aliyenifaa kwa njia moja au nyingine. Kwenu nyote nasema asante sana.

## IKISIRI

Utafiti huu umechunguza hali ya kuingiliana na kujalizana kwa kuathiriana, kuiga na kurudufiana ili kujalizana katika kufasili fasihi. Mwingiliano huu umejikita katika vipengee vitatu vya mwingilianomatini ambavyo ni uigaji, urudufiano na uathiriano kama vipengee vya mwingiliano matini. Tungo ambazo zimeteuliwa ni *Fumo Liyongo*(1950), *Kifo Kisimani*(2001) na *Mstahiki Meya*(2009). Mwingilianomatini huu ulilenga uigaji, urudufiano na uathiriano kama vipengele vya mwingilianomatini. Madhumuni ya utafiti huu ni kubainisha jinsi vipengele vya mwingilianomatini vinachangia katika kuendeleza, kufasiri na kukuza kazi za fasihi. Maswali yaliyoongoza utafiti huu ni: Je, kuna uathiriano katika *Fumo Liyongo*, *Kifo Kisimani* na *Mstahiki Meya*? Urudufiano unajitokezaje katika vipengele vya uhusika, msuko na maudhui? Mwandishi alitumia uigaji vipi kuendeleza fasihi ya Kiswahili? Utafiti uliongozwa na nadharia ya mwingilianomatini. Utafiti huu ulikuwa ni wa kiuthamano. Ulihusu kusoma tungo hizo kwa kina na kuzichambua kwa misingi ya nadharia ya mwingilianomatini. Vipengee vitatu vya mwingilianomatini vilitumika kutathmini kazi teule . Mbinu ya ufasiri na uchanganuzi wa yaliyomo ilitumiwa. Mtafiti alichambua uathiriano, urudufu na uigaji katika kiwango cha msuko, uhusika na maudhui. Kutokana na utafiti huu, imebainika wazi kuwa utendi wa *Fumo Liyongo*, tamthilia ya *Kifo Kisimani* na *Mstahiki Meya* zinaingiliana katika vipengele vya msuko, uhusika na maudhui. Mwingilianomatini huu unadhihirika wazi kama vile umejadiliwa kwa misingi ya nadharia ya mwingilianomatini. Mfumo wa mwingilianomatini huu unajengeka kutoka kiwango kimoja hadi kiwango kingine. Hali hii ya ujengano inazua wazi kuwa kazi za kifasihi hutokea kama mwangwi wa kazi za awali ambazo huweka msingi wa kazi hizo kwa njia mwafaka. Mtafiti aligundua kwamba, kazi hizi zimejengana. Ilhali kila kazi ina nafasi yake mahususi katika jamii, zinakubaliana kuendeleza maudhui mwafaka katika jamii inayokua na kuendelea kiuchumi na kisiasa. Inakisiwa kuwa wasomi wa kazi hizi watafaidika kwa masuala ya urudufiano, uigaji na uathiriano kama inavyojitokeza katika tungo hizi. Waandishi watapata mwanga wa jinsi wanavyoweza kujenga kazi zao kwa misingi ya kazi ambazo zimetungwa awali ili kufanikisha kazi zao zaidi. Hatimaye, mapendekezo kuwa kuna haja ya mwanda wa mwingilianomatini kuchunguza katika sehemu zingine za fasihi andishi na simulizi.

## ABSTRACT

This research focuses on establishing the interrelationship of texts in Kiswahili literature which touches on allusion, pastiche and parody in interpretation of Kiswahili literature. The selected texts which facilitated this study are *Fumo Liyongo*(1950), *Kifo Kisimani*(2001) and *Mstahiki Meya*(2009). The objective of this reseach was to demonstrate pastiche, parody and allusion in characterization, plot and thematic structure. The study also aimed at examining the impact pastiche, parody and allusion has on interpretation of literature works. as well as guiding on the new information which can be extracted from these texts when analysed on the basis of the selected parts of intertextuality. The study was guided by the following research questions: How is allusion in the selected texts portrayed? How are pastiche and parody illustrated at the level of characterization, thematic structure and plot in the selected texts? How does pastiche, parody and allusion hhelp in extracting new information when these texts are analysed according to intertextuality theory?. the research was interpretative in nature. it entailed carefully studying the selected texts and analysing them against the selected theory. the findings of the study indicate that pastiche, parody and allusion are clearly illustrated in the three above-mentioned texts in the characterization, plot, and thematically. With regard to theselected texts there is close inter-relationships between literature works which aims at complementing and enhancing previous works. It has given a basis on the use of the selected theory to guide interpretation and creation of more thrilling and up to date literature works but being guided on already existing texts. The research has illustrated a clear path towards achieving a democratic society in Africa from the lessons drawn from the selected texts. The selected theory has guided the study to achieve the set objectives. Recommendations have also been made concerning other areas related to intertextuality which need to be researched on. This is because intertextuality is a wide scope which can be used to interprete different literature texts at different levels to make it more explicit.

## YALIYOMO


**UNGAMO NA IDHINI** ..... i

**HAKILINZI** ..... iii

**TABARUKU** ..... iv

**SHUKRANI** ..... v

**IKISIRI** ..... vi

**ABSTRACT** ..... vii

**YALIYOMO** ..... viii

**SURA YA KWANZA** ..... 1

**UTANGULIZI** ..... 1

1.1 Usuli wa Mada ..... 1

1.2 Suala la Utafiti ..... 3

1.3 Madhumuni ya Utafiti ..... 3

1.4 Maswali ya Utafiti ..... 3

1.5 Umuhimu wa Utafiti ..... 3

1.6 Upeo na Mipaka ..... 4

1.7 Matatizo Yaliyojiri Katika Utafiti ..... 4

**SURA YA PILI** ..... 6

**MAPITIO YA MAANDISHI NA MISINGI YA NADHARIA** ..... 6

2.1 Utangulizi ..... 6

2.2 Tasnifu Zinazohusiana na Tungo Teule za Utafiti Huu ..... 6

2.3 Mapitio kuhusu Tendi ..... 11

2.4 Yaliyotafitiwa kuhusu Tamthilia Teule ..... 14

2.5 Misingi ya Nadharia ..... 15

**SURA YA TATU** ..... 18

**MBINU ZA UTAFITI** ..... 18

3.1 Utangulizi ..... 18

3.2 Muundo wa Utafiti ..... 18

3.3 Mahali pa Utafiti ..... 18

3.4 Walengwa ..... 18

3.5 Sampuli ..... 19

3.6 Ukusanyaji wa Deta ..... 19

3.7 Uchanganuzi na uwasilishaji wa data ..... 20

**SURA YA NNE** ..... 21

**UCHANGANUZI NA UFASIRI WA DETA.......................................................................21**
4.1 Utangulizi ....................................................................................................21
4.2 Uathiriano katika kiwango cha Msuko, Urudufiano katika Wahusika na Uhusika .......21
4.2.1 Msuko wa Utendi wa Fumo Liyongo ....................................................................21
4.2.3 Msuko wa Kifo Kisimani ..........................................................................23
4.2.3 Msuko katika Mstahiki Meya .....................................................................27
4.2.4 Uathiriano katika Kiwango cha Msuko ..........................................................30
4.2.5.1 Uthiriano katika Kiwango cha Uhusika.......................................................32
4.2.5.2 Wasifu wa Wahusika ..................................................................................51
4.2.5.3 Ulinganishaji wa Wahusika kwa kurejelea Idadi ...............................................53
4.3 Mwingiliano wa Kimaudhui.........................................................................53
4.3.1 Mwingiliano wa Kimaudhui kwa kurejelea Dhamira............................................54
4.3.2 Mwingiliano wa Kimaudhui kwa kurejelea Ujumbe.............................................56
4.3.2.1 Ufisadi ....................................................................................................56
4.3.2 .2 Unafiki ...................................................................................................59
4.3.2.3 Dini ........................................................................................................62
4.3.2.4 Ukosefu wa Uwajibikaji ..............................................................................64
4.3.2.5 Ubinafsi ..................................................................................................68
4.4. Namna Uathiriano, Uigaji na Urudufiano Unavyoelekeza Ufasiri wa Kazi za Fasihi..73
4.4.2.1 Ujinasibishaji wa Masuala Ibuka.................................................................73
4.4.3 Usisitizo ....................................................................................................75
**SURA YA TANO ..........................................................................................79**
**MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ...................................................79**
5.1 Utangulizi ....................................................................................................79
5.2 Muhtasari....................................................................................................79
5.3 Hitimisho....................................................................................................80
5.3.1 Mafaniko ya Utafiti .......................................................................................81
5.3.2 Utathmini wa Utendakazi wa Fasihi ...............................................................81
5.3.3 Jinsi Utendi wa Fumo Liyongo unavyotathminiwa na Tamthilia ya Kifo Kisimani. .81
5.3.4 Kuelekea Ustawi wa Kidemokrasia Katika Jamii ya Kiafrika; Mafunzo kutoka Utendi wa Fumo Liyongo, Kifo Kisimani(2001)na Mstahiki Meya (2009)....................................82
5.3.6 Mapendekezo ..............................................................................................85
**MAREJELEO ..............................................................................................86**
**KIAMBATISHO:...........................................................................................91**

# SURA YA KWANZA
# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa Mada

Fasihi katika Afrika Mashariki imekuwa ikiendelezwa kiutunzi na waandishi mbalimbali wakirejelea misingi tofauti. Baada ya utunzi, kuna kiwango cha uhakiki, uchambuzi na ufasiri ili kuweza kuelewa dhamira aliyokusudia mtunzi kwa wasomaji ya kazi yake. Uchambuzi wa kazi za fasihi ni jambo ambalo halifanyiki ovyo, bali ni mchakato unaongozwa na vigezo na vipengele mbalimbali.

Vipengele vya uchambuzi wa kazi ya fasihi ili kuelewa ujumbe na dhamira ya mwandishi ni kama vile; maana, uwakati, mwingiliano matini, upokezi, unusura, ukanda, fani, motifu, utamaduni na kufasiri kazi ya fasihi. Hata hivyo, baadhi ya vipengele hivi ni pana sana hivi kwamba haviwezi kuangaliwa kwa ujumla na maudhui. Kila mojawapo ya vipengele hivi huwa na umuhimu wake katika kuchambua. Mojawapo ya kipengele kama hicho ni kipengele cha mwingilianomatini.

Mwingilianomatini kama anavyosema Kristeva (1986) ni kipengele cha fasihi ambapo kazi au matini ya kifasihi inaonyesha kutegemeana, kuingiliana na kuathiriana kwa kazi fasihi zilizokuwepo awali na zile zilizopo sasa. Kristeva alisema kuwa, katika fasihi hakuna matini yoyote inayoweza kuangaliwa ikiwa pekee yake na kwa kujitegemea; anasisitiza kuwa lazima kutakuwa na matini nyingine inayohusiana na hiyo inayoangaliwa.Uchambuzi wa mwingilianomatini hauwezi kuchunguzwa kwa ujumla wake bali huweza kuchunguzwa kwa mujibu wa awamu za mwingilianomatini. awamu hizi hutegemea sana mtunzi au mwandishi na aina za mwingilianomatini ambazo huchaguliwa au kuteuliwa na msomaji au mhakiki. Kuna awamu tatu za mwingilianomatini; awamu ya ulazimu, kimaksudi na kibahati nasibu.

Kwa kurejelea awamu ya ulazimu, mwingilianomatini unaweza ukajitokeza kama njia isiyoepukika kupitisha mawazo fulani kwa ukamilifu. Hali hii ya mwingilianomatini humpa mwandishi nafasi ya kujenga kazi yake kwa misingi ya kazi ya awali. Kazi hii ya baadaye huweza kupata ufasili mwema iwapo msomaji ana ufahamu wa matini ya awali. Awamu hii inapisha uhuru wa mwandishi kutaja kazi ya mwandishi mtangulizi ambaye analenga kutumia matini yake kama msingi wa ufasili wake. Basi mwandishi wa baadaye anaweza akamtaja mwandishi wa awali au akatumia mandhari au msuko unaodokezea kwamba kazi yake imeathiriwa naye awali. Matini hii huundwa kama njia ya kuendeleza matini ya awali. Kazi ya baadaye huwa ni kama ukamilisho wa kazi ya mwanzo.

Mwingilianomatini pia hujikita katika umaksudi. Katika awamu hii, mwandishi anaamua kuunda matini ambayo ameiegemeza katika kazi ya mwandishi wa awali. Mfasili wa kazi ya baadaye si lazima awe na ufahamu wa kazi tangulizi ili kupata maana kamili ya matini ya baadaye. Awamu ya mwingilianomatini wa kibahati hutokea kwa baadhi ya watunzi wa matini za kifasihi. Aidha, matini hizi hutokea kuchukua muundo na mtindo sawa ijapokuwa hakuna uhusiano wa moja kwa moja. Aidha, waandishi wa matini hizi huweza kuathiriwa na hali sawa za kimazingira ambazo huwaelekeza kuwa ni  kazi zinazojengana.

Kuna aina za mwingilianomatini ambazo msomaji au mhakiki yeyote yule anaweza kuegemeza uelewa wa kazi ya fasihi husika. Undumakuwili ni aina ya mwingiliano matini inayojitokeza katika kufasili matini za waandishi tofauti. Mwandishi anaweza akawa na dhamira na malengo sawa na mwandishi wa matini nyingine. Maswala yanayozungumziwa ni yale yale ya awali.

Mwingilianomatini huweza kujitokeza kupitia urejelezi wa kazi zingine. Matini huweza kurejeleana ili kukamilishana kimawazo. Hali hii ya matini kuingiliana hujitokeza katika muundo. Kwa mfano, S.A Mohammed katika riwaya ya *Nyuso za mwanamke* anarejelea riwaya yake ya awali ya *Utengano*. Kazi hizi zinafanana kimaudhui na kimuundo. Ni kana kwamba S.A Mohammed anatumia *Nyuso za Mwanamke* kukamilisha wazo la riwaya ya *Utengano*; wazo ambalo ni ukombozi wa mwanamke kutokana na dhuluma na ukusanyaji katika jamii.

Unukuzi ni hali ya mwingilianomatini ambapo mwandishi wa matini ya baadaye anamnukuu mwandishi wa matini ya awali. Katika hiyo hali ya kunukuu anaweza kutaja mawazo hayo ni ya nani. Kwa mfano, Timothy Arege katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* amenukuu riwaya ya S. A. Mohammed ya *Utengano.* Mhusika Meya katika *Mstahiki Meya* anamwambia mhusika daktari Siki aionee nyumba yake paa. Haya ni maneno aliyotumia S. A. Mohammed katika *Utengano*, mhusika wa riwaya hii. Bw. Maksuudi anapotumia maneno hayo hayo kwa mkewe Bi. Tamima.

Kazi nyingi za fasihi huangaliwa kwa aina hizo za mwingiliano matini zilizoelezwa. Wanafasihi wanapoelezea dhana ya mwingilianomatini, huegemea aina ya unukuzi na urejelezi. Haijatokea kwamba kuna njia nyingine za kimwingiliano matini zinazoweza kutumiwa kama jicho la tatu kuhakiki kazi ya fasihi. Hili linadhibitishwa na kauli ya Kristeva mwaka gani  kuwa mwingiliano matini sio urejelezi wa kazi fulani katika kazi nyingine tu, bali pia ni ule uingiliano wa mtindo ya kiuashiriaji. Anaeleza kuwa dhana ya mwingiliano matini kama jumla ya maarifa na mbinu zinazoifanya matini kuwa na maana, ambapo maana ya matini huangaliwa kama inayoitegema matini nyingine. Kwake Kristeva, matini yoyote ile

huchukua au hufaidi kutokana na matini nyingine. Ni kwa msingi huu ndio utafiti huu ulinuia kuonyesha kuwa mbali na urejelezi, unukuzi na undumakuwili, kuna mikabala mingine ya mwingiliano matini ambayo inaweza kutumiwa kuchambua kazi ya fasihi ili kuelewa maana ya kazi husika.

## 1.2 Suala la Utafiti

Kazi za fasihi hujitegemea na vilevile hutegemeana kwa sababu ya kuathiriana aidha kiulazimu, kimakusudi au kibahati nasibu kwa mujibu wa Porter (1986). Hata hivyo athari hizi kiuchambuzi, huegemea urejelezi na unukuzi wa moja kwa moja. Utafiti huu ulichunguza ujalizano katika kazi za teule za fasihi *Utendi wa Fumo Liyongo* (1950), *Kifo Kisimani* (2001) na *Mstahiki Meya* (2009) hasa kwa kuzingatia urudufiano, uigaji na uathiriano kama mikabala tofauti ya kuchambua kazi za fasihi.

## 1.3 Madhumuni ya Utafiti

Utafiti huu unalenga kubainisha hali ya mwingiliano uliopo kati ya kazi ya *Mstahiki Meya*, *Kifo Kisimani* na *Fumo Liyongo*. Utafiti huu uliongozwa na madhumuni mahususi yafuatayo:

i. Kubainisha uathiriano uliopo katika msuko na uhusika wa *Utendi waFumo Liyongo*, *Kifo Kisimani* na *Mstahiki Meya*.
ii. Kuchanganua urudufiano na uigaji katika maudhui *Utendi wa Fumo Liyongo*, *Kifo Kisimani* na *Mstahiki Meya*..
iii. Kutathmini namna uigaji, urudufiano na uathiriano unaelekeza ufasiri na utunzi wa kazi za fasihi.

## 1.4 Maswali ya Utafiti

i. Je, kuna uathiriano gani katika msuko na uhusika katika kazi ya *Utendi wa Fumo Liyongo, Kifo Kisimani* na *Mstahiki Meya*?
ii. Urudufiano na uigaji unajitokezaje katika maudhui ya kazi ya *Utendi wa Fumo Liyongo, Kifo Kisimani* na *Mstahiki Meya*?
iii. Uigaji, urudufiano na uathiriano unatumikaje kuelekeza ufasiri na utunzi wa kazi za fasihi?

## 1.5 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu ni muhimu kwa sababu ulidhihirisha kuwa kazi za *Utendi wa Fumo Liyongo* (1950), *Kifo Kisimani* (2001) na *Mstahiki Meya* (2009) zinaingiliana kimatini. Utafiti huu ni muhimu pia kwani utaweza kubainisha uathiriano, uigaji na urudufiano gani

katika uhusika katika *Utendi wa Fumo Liyongo* (1950), na *Kifo Kisimani* (2001) na *Mstahiki Meya* (Arege; 2009). Inaonekana kuwa *Utendi wa Fumo Liyongo* (1999) ndio mkongwe zaidi hasa tukizingatia kwamba historia ya fasihi. Historia inadai kwamba ushairi ambao ni utanzu wa fasihi simulizi ndio mkongwe zaidi ukilinganisha na fasihi andishi ambayo ndiyo inajumuisha kazi za tamthilia ambazo mtafiti aliteua: *Kifo Kisimani* (2001) na *Mstahiki Meya* (2009).

Ni utafiti ambao uliweka kwa uwazi jinsi uthiriano, uigaji na urudufiano huu unajitokeza katika msuko katika kazi teule za fasihi hasa kwa kuzingatia vipengele vya uhusika maudhui na mtiririko wa vitushi. Kazi hii imetoa mchango katika jamii ya kiusomi kwa kubainisha: jinsi waandishi huiga kazi zilizochapishwa ili kuendelea kujenga kazi zao za fasihi; vilevile kuendeleza maudhui yanayohitaji kusisitizwa katika jamii na katika vipindi mbalimbali vya kihistoria. Utafiti umedhihirisha masuala mapya yaliyoibuka katika tungo hizi iwapo zilitazamwa kwa mwelekeo wa kimwingiliano matini.

**1.6 Upeo na Mipaka**

Upeo wa kazi hii ulikuwa ni *Utendi wa Fumo Liyongo* (1950) na tamthilia: *Kifo Kisimani* (2001) na *Mstahiki Meya (*2009). Matini za tungo hizi ndizo zilizotumiwa kama data. Mipaka ya kazi hii niilikuwa ni vipengee vitatu:uhusika, msuko na maudhui. Katika uhusika, wahusika nguli pamoja na wahusika wajenzi waliangaziwa. Msuko ambao unahusu mtindo wa uwasilishaji wa kazi hizi uliangaziwa kwa kupambanua upekee na urudufiano katika uwasilishaji wa matini hizi zilizo tofauti. Maudhui ambayo ni kipengee muhimu cha kuendeleza dhamira ya mtunzi wa matini yoyote ile pia yalitathminiwa kwa kuegemea kigezo cha uathiriano katika nadharia ya mwingilianomatini. Aidha, mtafiti alihitimisha utafiti wake kwa kudhihirisha namna uigaji, urudufiano na uathiriano ulivyoelekeza ufasiri wa kazi za fasihi.

**1.7 Matatizo Yaliyojiri Katika Utafiti**

Utafiti huu ulifanikiwa licha ya kuwepo na matatizo kadha wa kadha. Mtafiti alikumbana na tatizo la kusaka maana halisi ya baadhi ya maneno katika *Utendi wa Fumo Liyongo* kwa kuwa baadhi ya maneno na vifungu vilikuwa vimeandikwa katika lahaja ya Kipate.

## 1.7 Maelezo ya Istilahi

**Kipengele-** pia huitwa kipengee. Kumaanisha mkabala wa wazo au jambo. Kwa muktadha huu inatumika kumaanisha mawazo maalum yanayoangaziwa katika utafiti.

**Matini-** ni kazi zilizoandikwa kuwasilisha jambo fulani. Kwa muktadha wa kazi hii inarejelea kazi za fasihi teule.

**Mwingiliano-** ni hali ya kazi moja kuathiriana au kuhusiana. Kwa muktatdha huu wa uingiliaono matini inarejelea hali ya kazi teule kuwa na uathiriano au uhusiano.

**Utendi-** ni ushairi mrefu zaidi uanaoelezea mambo ya kina kuhusu shujaa fulani. Kwa muktadha wa kazi hii, utendi ni mojawapo ya kazi teule ambayo itahakikiwa.

**Uathiriano-** ni hali ya kazi moja kuhusuka katika uandishi na uchambuzi wa kazi nyingine.

**Uigaji-** ni hali ya sura ya kazi fulani kupatikana katika uwasilishaji wa kazi nyingine ya fasihi.

**Urudufiano-** ni ule urudiaji wa masuala fulani katika kazi ya fasihi na waandishi tofauti lakini wenye asili tofauti.

**Utendi-** ni ushairi mrefu zaidi uanaoelezea mambo ya kina kuhusu shujaa fulani. Kwa muktadha wa kazi hii, utendi ni mojawapo ya kazi teule ambayo itahakikiwa.

# SURA YA PILI
# MAPITIO YA MAANDISHI NA MISINGI YA NADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Sura hii ilishughulikia mapitio ya maandishi. Sura hii ina sehemu tatu ambazo kwanza, ni kazi za kitaaluma ambazo ziliandikwa na watafiti kuhusu mada zinazohusiana na kazi ya mtafiti. pili, iliangazia yaliyoandikwa kuhusu tendi kwa vile mojawapo ya tungo teule ni utendi. tatu, mtafiti aliangazia yaliyotafitiwa kuhusu tamthilia teule zilikazotumiwa na mtafiti kufanikisha kazi hii.

## 2.2 Tasnifu Zinazohusiana na Tungo Teule za Utafiti Huu

Utafiti wa Kang'e (2011) anaelezea kuwa tamthilia ya Kiswahili ni mojawapo ya tanzu za fasihi andishi ya Kiswahili. Tanzu nyingine za fasihi hii ni pamoja na riwaya, ushairi hadithi fupi na novela. Kwa mujibu wa utafiti wake, utanzu wa tamthilia ya Kiswahili umedhihirisha, kwa njia moja au nyingine, uhusiano wa kimatini. Wahakiki wamechunguza nyanja kadhaa za utanzu wa tamthilia kama vile: utunzi wa tamthilia, mwathiriano, usemezano, maendeleo ya maudhui, wahusika na mtindo. Utafiti wake ulilenga kuchunguza na kuchanganua mwingilianomatini katika tamthilia ya Kiswahili. Viwango na aina za mwingilianomatini zilichunguzwa na kubainishwa. Alitumia mbinu ya kiuthamano kwenye utafiti na kuongozwa na nadharia ya mwingilianomatini iliyoasisiwa na Kristeva (1966). Utafiti wake ulifanyiwa maktabani na kuhusisha tamthilia mbili za Kiswahili: *Mashetani* na *Kijiba cha Moyo zimeandikwa na nani na mwaka gani.*

Suala la mwingilianomatini katika tendi limeangaziwa na mtafiti Macha (2013). Makala haya yana lengo la kuchunguza kama tendi za Kiswahili huwa na mwingilianomatini na kubainisha vipengele vilivyoingiliana katika utanzu huu na dhima zake. Anadai kuwa, waandishi wa tendi mbalimbali za Kiswahili, wamekuwa wakitumia mtindo wa kuchanganya vipengele mbalimbali vya kisanaa katika kazi moja. Mtindo huu unatazamwa na makala haya kuwa ni mwingilianomatini katika tendi za Kiswahili. Mathalani, mwandishi anayeandika au simulia tendi za Kiswahili, hujikuta akichanganya matini za nyimbo, semi, hadithi ndani ya hadithi, maigizo, matumizi ya ishara, ngoma na kadhalika. Kuchanganya huko kwa vipengele tofauti katika kazi moja ni kitu ambacho kimezoeleka sana miongoni mwa wanafasihi. Kipengele hiki kimeandikiwa ili kuweka bayana kuwa katika tendi kunaweza kuwa na sifa mbalimbali za tanzu nyingine na kuziorodhesha ili zijulikane wazi. Hivyo makala yake yana lengo la kuthibitisha uwepo wa mwingiliano huo. Muwala wa vipengele na namna vinavyosaidiana kuleta muamano wa mawazo katika riwaya pia ni kazi ambayo

imechangiza sana katika utafiti huu. Kavoi (1996) ametumia nadharia ya umuundo na nadharia ya uhakiki-mtindo. Umuundo ni nadharia yenye mtazamo wa kuzingatia jinsi vipengele mbalimbali vinaletwa pamoja kuunda kitu kizima kilichokamilika. Kazi ya Kavoi ilimpa mtafiti changamoto ya kuchukua mkondo wa tamthilia kwa vile amejikita katika mkondo wa Riwaya. Ilimsaidia mtafiti kuelewa muamano wa mawazo katika tamthilia jambo ambalo limempa mtafiti msingi bora wa ufasili wa maudhui.

Maana ya fani, utunzi wa tamthilia na drama kwa jumla ni mojawapo ya tafiti ambazo zimejenga kazi hii. Mtafiti ameeleza umbuji wa wahusika, nafasi ya/ na majukumu waliyopewa na mtunzi. Ijapokuwa Musyoka (1999) amejishughulisha na kazi ya uhakiki, ni dhahiri kuwa hajahakiki kazi ya Mberia (2001), Arege (2009) na Utendi wa Fumo Liyongo (1950). Hivyo basi ni dhahiri kuwa kuna pengo la kiusomi kuhusu uhakiki wa kazi hizi kwa nadharia ya mwingilianomatini.

Kazi hii iliangazia mtindo kwa kuwa inahusu vipengele vya uhusika na msuko. Ili kupata msingi bora wa kuhakiki kazi hii mtafiti amepitia tasnifu ya Mwanzi(1995) ambaye alitalii mtindo kwa haja ya kutambua namna mwandishi anavyoteua na kutumia maneno kwa njia ya kipekee kuwasilisha mawazo, kuchora mandhari, hisia na vile anadokeza maana. Katika kazi yake, ijapokuwa ametafiti kuhusu fasihi lakini hajatafiti kuhusumwingiliano matini.

Kwa mujibu wa Kazungu (1982) kuna uchunguzi wa ukiushi na uchimuzi katika vitabu vitatu; *Asali Chungu* riwaya ya S.A Mohammed, *Swifa ya Nguvu Mali* na *Utemi* wa Hassan Bin Ismael na *Wakati Ukuta* tamthilia ya Ebrahim Hussein. Ni dhahiri kuwa anatafiti kuhusu tamthilia lakini anaegemea upande tofauti na kazi hii.

Vile vile Mumia (2000) anajitosa pia katika suala la uhakiki wa vitabu anatathmini vile mtindo umetumiwa kuimarisha muamano. Anatumia nadharia ya uhakiki-maana elimu mtindo na kuacha pengo la kiusomi kuhusu mwingiliano matini. Aidha, anampa mtafiti msingi bora wa kuelewa namna ya kuhakiki kazi ambazo ameteua kwa ajili ya utafiti huu.

Mojawapo ya kazi za kimtindo ni kazi ya uhakiki wa mtindo wa riwaya za John Habwe na Wanyama (2013) aliangazia mtindo katika riwaya za John Hamu Habwe. Alibainisha na kueleza aina za mbinu za lugha alizotumia mwandishi katika riwaya zake. Anaelezea utendakazi wa kila mbinu katika kufanikisha uwasilishaji wa ujumbe. Utafiti huu unahusiana na utafiti wa kazi hii kwa vile unahusu uhakiki na hasa uhakiki wa mbinu za kimuundo. Kazi hii ni tofauti na ya mtafiti kwa kuwa kiwango cha alichohakiki hasa kwa kuwa uhakiki huu unahusu mwingiliano matini, jambo ambalo hakuliangazia. Kazi hii ilimpa

mtafiti mwanga wa jinsi ya kuendeleza uhakiki huu kwa njia bora. Suala hili linatofautiana na uhakiki wa utafiti huu ijapokuwa ni katika kazi za fasihi andishi.

Utafiti upo unaoangazia usawiri wa wahusika watoto katika tamthilia zilizopendekezwa katika shule ya upili. Vilevile, anachunguza mtazamo wa wahusika watu wazima kuhusu watoto katika tamthilia husika hizo.Anahakiki tamthilia lakini anatumia nadharia tofauti na kazi hii. Ni utafiti wake Mutua (2013) katika kazi yake ya fani na fasihi zinazoibua fantasia za watoto.

Mtafiti akiangazia upande wa tamthilia ambapo ndipo kazi hii imejikita, ni dhahiri kuwa kunao wengine ambao tayari wamejikita katika ulingo wa tamthilia. Mojawapo wa kazi hii ni Ayodi; (2011) ambaye ameangazia suala la uhakiki wa tamthilia. Anajadili matumizi ya jazanda katika tamthilia teule ambazo ni tamthilia ya *Amezidi* ya Mohammed, (1985) *Mashetani* ya Hussein, (1971) *Usaliti Mjini* ya Imbuga, (1994) na *Mkaguzi Mkuu wa Serikal*i ya Golgol, (1979). Vilevile, hakugusia suala la mwingilianomatini katika kazi za fasihina hivyo basi kuna mwanya ambao unahitaji kutafitiwa hasa kuhusu suala la uingiliano matini katika fasihi ya Kiswahili. Utafiti wake ulijikita sana katika tamthilia ya Kiswahili ila haujaegemea upande huu wa mwingilianomatini.

Nduti(2000) ameangazia mwingilianomatini katika filamu za drama teule nchini Kenya. Katika kazi yake alichagua filamu tatu ambazo ni *Zeinabu Rudi Nyumbani* (2008) na *Billy Mbilikimo*, *Chaising Moses* (2009) na *Alexander Konstantaras na The village Cassanova* (2010) na Simon Nduti. Utafiti wake unaangazia kuhakiki vipengele vya mwingilianomatini katika hali za jamii na tamaduni mbalimbali ambazo zimejitokeza katika kazi hiyo. M'erimba anataja kuwa, filamu hizi huenda zikawa si kazi tofauti lakini ni kazi ambazo zimeundwa kwa kurekebisha kazi ambazo tayari zimekuwepo katika jamii. Kwa kutaja hivyo, ni dhahiri kuwa kazi hii inafanana na kazi hii ila zinatofautiana kwa kuwa yeye anangazia uingiliano matini katika filamu ilhali kazi hii inahusu uingiliano matini katika tamthilia teule.

Naye Bakari(2011) ameshughulikia swala la nadharia kama mkakati wa kufahamu riwaya za *Babu Alipofufuka*, *Bin-Adamu* na mkusanyiko wa hadithi fupi *Sadiki Ukipenda*. Nadharia iliyotumiwa katika utafiti huu ni ile ya usemezano. Hii ni kwa sababu lengo lake ni kuchanganua jinsi usemezano unavyoweza kujaliza mapengo yanayojitokeza katika za *Babu Alipofufuka*, *Bin-Adamu* na *Sadiki Ukipenda*. Utafiti wake umejaribu kujaliza mapengo yanayoleta matatizo ya ufahamu na usadikifu kazi alizoteua za kihalisiajabu. Katika kazi yake matukio yanasawiriwa kiajabu ajabu, ni ya kuogofya, kutisha na hayaeleweki kwa urahisi. Kwa kutumia nadharia ya usemezano, amerahisisha uelewa na usadikifu wa

vipengele hivi. Kazi hii inafanana na kazi hii kwa kuwa lengo lake ni sawa na la mtafiti kwa la kujaliza pengo kwa uelewa na usadikifu wa kazi teule. Aidha, kazi hii ni tofauti na hii kwa kuwa kazi zake ni tofauti na hizi na vile vile amejikita katika kiwango cha usemezano.

Katika suala la mwingilianomatini, Peter (2015) ameangazia Uingiliano kama kipngele katika kazi za wanafunzi. Aliangazia mwingilianomatini unajitokeza katika kiwango kipi miongoni mwa wanafunzi katika eneo la Tharaka Nithi. Alielezea kuwa mwingilianomatini uangazia uhusiano uliopo katika kazi tofauti ambazo mtu amekumbana nazo awali. Katika kazi yake anaangazia jinsi kazi hizi zinavyojitokeza katika kazi za wanafunzi hawa jinsi wanavyoziandika. Kazi hii ya Atieno kwa kiwango fulani inafanana na kazi hii kwa kuwa inaangazia uhusiano ulipo na kazi ambazo zimeandikwa awali mingoni mwa wanafunzi wa Tharaka-Nithi ila kuna nafasi ya kiusomi ambayo imeachwa ambayo mtafiti alidhamiria kuiziba. Aidha, kazi hii ni tofauti na kazi ambayo imeangaziwa ndio maana inabidi kuangazia kazi ya uingiliano matini katika kazi ambazo mtafiti ameteua. Aidha, kazi hii inamsaidia kuelewa zaidi kazi ambayo aliitafitia.

Mwingilianomatini katika novela za kazi teule za fasihi ambapo mtafiti ameteua kazi za Euphrase Kezilahabi *Nagona* na *Ziraili na Zirani* ya Wiliiam Mkufya katika *Swahili Forum* iliyowasilishwa na Deigner (2005). Katika kazi yake ameangazia uingiliano matini katika kazi ambazo mtafiti amezitaja hapo juu. Deigner amejikita katika kiwango cha ploti katika utafiti wake. Aliongozwa na nadharia ya mwingilianomatini. Mhimili ambao umetawala kazi yake ni kwamba katika kazi za fasihi hakuna kazi ambayo imejitenga. Anaangazia kwamba kila matini inajikita katika uakisi wa matini nyingine tofauti. Kazi hii imempa mtafiti uwazi wa kuchambua matini za kifasihi.

Kazi ya Deigner(2005) kwa kiwango kikubwa inafanana na kazi hii ila zinatofautiana kwa kiwango fulani. Kazi hii inafanana kwa kuwa kazi yake inahusu mwingilianomatini katika kazi za fasihi ambazo ni za Kiswahili. Aidha, inafanana na kazi hii kwa kuwa utafiti wake vile vile unaangazia uingiliano matini katika kiwango cha ploti. Hali hii imechangia pakubwa katika kazi hii kwa kuwa imempa mtafiti kuelewa mwafaka namna ya kuchanganua mwingilianomatini katika kiwango cha ploti. Aidha, kazi hii ni tofauti kwa kuwa inahusu mwngilianomatini katika kiwango cha uhusika na vile vile kiwango cha ploti. Kazi hii ni tofauti na kazi ya Deigner kwa kuwa amejikita katika upande wa novela ilhali kazi ya mtafiti ilijikita katika kiwango cha tamthilia.

Tamthilia zilizoandikwa nchini Kenya kati ya mwaka 1956 hadi 1982 ni utafiti wa Mugambi(1982). Anaelezea kuhusu maendeleo ya tamthilia kulingana na maudhui yanayojitokeza. Kwake, wanatamthilia wa kwanza nchini Kenya wanaendeleza mitazamo ya

kikoloni katika utunzi wao. Kizazi cha pili ni cha waandishi ambao wamekengeuka kutokana na jamii zao kama vile Ngugi wa Thiong'o na Said. Utafiti wake ulitusaidia kuelewa tamthilia za kikenya na watunzi wa kikenya ambao huenda waliwaathiri au waliathirika na waandishi tunaowachunguza na wale ambao Mugambi (1982) aliwatafiti.

Huku akielezea historia ya tamthilia nchini Tanzania, Mlama (1993) anasema tamthilia ilitungwa kwa minajili ya kikoloni kuwasisimua wahudumu wa serikali na kumsimanga mwafrika kwani ilimsawiri mwafrika kama kiumbe duni. Baada ya uhuru, futuhi zilitungwa za kuwakashifu waafrika walioiga mienendo ya wazungu bila kufikiria. Baadaye kidogo, watunzi wa tamthilia walianza kuambatanisha tamthilia na hali ya kiuchumi ya kijamii. Mawazo yake yalitufaa sana katika kuchunguza ikiwa tamthilia ya Kiswahili inakashifu wale watu wanaofuata mienendo ya wazungu kikasuku kupitia sauti mbalimbali za kijamii au la.

Makala kuhusu kazi za Kezilahabi mtafiti anahakiki motifu za dunia kama mahali pabaya na maisha kutokuwa na maana. Anachunguza namna kazi za Kezilahabi zinadhihirisha kuwa dunia ni mbayana inapaswa kutazamwa kama mahali pabaya pa kuishi. Kazi hii ya Wamitila (2003) kwa kiwango fulani inaoana na kazi ya mtafiti kwa kuwa anajikita katika kipegele cha fani ila ni tofauti na kazi ya mtafiti inayohusu kipengee cha mwingiliano matini.

Kunayo tasnifu nyingine inayoshughulikia mwingiliano wa fani na maudhui katika diwani za *michezo wa karata* (1997) na *Bara Jingine* (2001). Mtafiti aliongozwa na nadharia ya sosholojia na ameonyesha umuhimu wa vipengele vya kifani pamoja na athari za kimazingira katika kujenga fahiwa kazi za kifasihi. Mambo mawili makuu yanajitokeza katika utafiti wake. Kwanza, kazi zote zinafuata mkondo wa mashairi huru ya sitiari za michoro kwa kuonyesha kuwa kinachoonekana katika mchoro hakiwezi kutenganishwa na yale yanayoelezwa kupitia maneno ya mtunzi. Kazi ya Nzuki (2003) inaegemea upande wa wa uingiliano. Aidha hakuegemea upande wa mwingilianomatini katika kazi ambazo mtafiti ameziteua. Mtafiti amesaidika na utafiti huu kwa kuwa amepata ufahamu wa jinsi nadharia husika inavyotumika katika uchambuzi wa kazi za fasihi.

Katika tasnifu mtafiti Njoroge (1997) anahakiki riwaya mbili za waandishi wawili, Euphrase Kezilahabi, *Rosa Mistika* (1971) na Said A. Mohamed, *Tata za Asumini* (1990). Nadharia ambayo imemwongoza ni ya Mwingiliano matini. Aidha ametalii vipengele anuwai katika mwanda wa kimwingiliano matini kama vile ploti, wahusika, mandhari na maudhui. Isitoshe, anonyesha namna riwaya za namna riwaya hizi zunavyohitilafiana kwa kiasi tu katika kipengele cha ploti na wahusika. Hata hivyo Njoroge hakushughulikia vipengele vyote

katika mwanda wa wa kimwingiliano matini. Kwa ufupi, kazi ya Njoroge inatoa mwanga mkubwa katika kuzielezea kazi hizi. Mtafiti ametumia kazi hii kama msingi wa kumwezesha kuhakiki vipengele anuwai vya kifani katika tamthilia za *Kifo Kisimani, Mstahiki Meya* na Utendi wa *Fumo Liyongo*. Vipengele vya mwingilianomatini ambavyo amevishughulikia katika utafiti huu ni uhusika na maudhui katika kazi teule.

Katika tasnifu nyingine, mtafiti anahakiki riwaya mbili za Kezilahabi; *Nangona* na *Mzingile.* Anazilinganishana kuzitofautisha na kazi zake za kinathari za awali *Rosa Mistika* (1971) na *Kichwa Maji* (1974) na *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975). Hali kadhalika anchunguza maendeleo ya kazi zake hasa kwa upande wa maudhui na baadhi ya vipengele vya fani kama jazanda na sitiari. Anadhihirisha jinsi ambavyo matini za kifasihi simulizi na fasihi andishi kwa kuzingatia visasili katika riwaya za *Pedro Paramo* na *Babu alipofufuka*. Kwa ufupi kazi ya Ochoki (2005) inatoa mchango mkubwa kuzielezea kazi hizi vyema ingawa ina udhaifu wa kutodhihirisha kama kuna mwingiliano matini kati ya *Nangon*a na *Mzingile* zikilinganishwa na *Pedro Paramo*. Anaonyesha wazi kuwa *Nagona* na *Mzingile* ni riwaya moja.

Tamthilia kumi na nne za Kiswahili zinahakikiwa ambapo mtafiti anachukulia tamthilia iliyoandikwa kama kazi nyingine yoyote ya kifasihi iliyokamilika na kuihukumu kwa misingi ya kifasihi. Alionyesha maudhui muhimu yanayoshughulikiwa na waandishi wa tamthilia za Kiswahili na kuonyesha jinsi tamthilia za Kiswahili zilivyo na ukwasi mkubwa wa kimtindo. Kazi hii imemfaa mtafiti kwa kutolea mwanga zaidi kuhusu tamthilia mbali mbali za Kiswahili na kuzielewa kwa undani. Aidha, imemsaidia mtafiti kwani inaelezea historia fupi ya uandishi na uhakiki wa tamthilia. Hata hivyo, kazi hii ni tofauti na ya mtafiti kwani ilizingatia nadharia ya mwingilianomatini ili kuweza kuchumguza vipengele anuwai katika mwanda wa kimwingiliano.

### 2.3 Mapitio kuhusu Tendi

Tenzi za Kiswahili zimepata mjadala mkubwa hasa katika vipengele anuai ambavyo kwa hakika ndivyo vinazibainisha tenzi za Kiswahili na hata kuzitofautisha na tenzi nyingine zisizo za Kiswahili. Miongoni mwa mambo ambayo yamepata mjadala ni upatikanaji wa historia katika tenzi za Kiswahili. Mjadala huu umekitwa katika maswali mbalimbali kama vile, tenzi za Kiswahili zinahusu nini? Kuna uwezekano wa kupata historia katika tenzi za Kiswahili? Historia zinazopatikana katika tenzi za Kiswahili zina ukweli na uhalisia wowote? Historia katika tenzi za Kiswahili inatokana na ngano au visasili? Ukweli huo ni wa kisanaa au kijamii? Na ni kwa namna gani watunzi wa tenzi wanapata historia za Waswahili.

Utafiti wa Faki (2015) umechunguza sifa za kifani za Utendi au Utenzi wa Kiswahili. Utafiti huu ulichunguza vipengele vya fani kama vile; muundo, mtindo, wahusika, mandhari na matumizi ya lugha katika Utendi wa Kiswahili. Mfano, Fumo Liyongo, ili kuona ni jinsi gani sifa za kifani zinavyojidhihirisha katika tenzi za Kiswahili. Aidha, utafiti huu umetofautiana na utafiti wa sasa kwa kuwa utafiti wa sasa unahusu vipengele vya mwingiliano matini jambo ambalo halijaangaziwa na mtafiti wa awali. Aidha, umemsaidia mtafiti wa baadaye kuelewa mtindo uliotumika kwa kuwa ni mojawapo ya kipengee kinachotafitiwa lakini kwa kulinganisha na kazi ya tamthilia.

Kwa mujibu wa mtafiti ambaye anachunguza dhana ya tenzi imetazamwa kwa mitazamo tofauti ambayo wakati mwingine hutofautiana. Ufasili wa tenzi umekuwa ukielezwa kwa kuangalia sifa. Katika makala haya, istilahi itakayotumika ni tenzi ambayo itakuwa na maana sawa na tendi hivyo istilahi zote zinatumika sawa. Wataalamu mbalimbali wamejaribu kufasili dhana ya tenzi / tendi kama ifuatavyo.

Mecha(2013) anaeleza kuwa utenzi umetokana na kitenzi tenda ambacho kinamaanisha kufanya tendo. Anabainisha kuwa utenzi huwa na mistari minne yenye silabi nane kwa kila kipande, mistari huwa na muungano wa matukio, unaweza kuhusu falsafa au masuala ya kidini, unaweza kutoa simulio la kweli au la kubuni na huwa na utangulizi, kiini na hitimisho. Mtaalamu huyu anaelezakuwa kuna ugumu katika kutafuta kisawe mwafaka cha utenzi katika lugha mbalimbali.

Uchunguzi wa Wamitila (2003) ulijadili utendi kama shairi refu la kisimulizi linalozungumzia kwa mapana na mtindo wa hali ya juu matendo ya mashujaa au shujaa mmoja. Anasema kuwa utendi huwa na sifa nyingi na huleta pamoja hadithi ya shujaa, magari, visasili, historia, pamoja na ndoto za taifa fulani. Fasili hii inatupa utata inapoeleza utendi kama shairi refu la kisimulizi. Utata unajitokeza katika kupima urefu wa ushairi ulio katika masimulizi. Tutatumia kipimo gani kupima urefu huo? Na mpaka wa ushairi mrefu na mfupi unaanzia wapi na kuishia wapi. Fasili hiyo inahitaji maelezo zaidi ya kipimo kipi kinafaa kutumika.

Ushairi wa matendo kwa mujibu wa Mulokozi (1999) ni utungo mrefu wenye kusimulia matukio ya kishujaa yenye uzito wa kijamii au kitaifa. Matukio hayo yanaweza kuwa ya kihistoria na visakale. Ufafanuzi huu wa Mulokozi umepiga hatua mbelekwa kueleza utendi kama ushairi wa matendo. Utendi hufungamana na matendo wakati wa utendaji wake. Matendo hayo huathirika utendi unapokuwa katika maandishi.

Kutokana na fasili za wataalamu hawa tunaweza kusema kuwa utendi ni ushairi unaosimulia tukio fulani kwa matendo. Usimuliaji wa tukio huambatana na matendo

ambayo hufanywa na msimuliaji. Utendi unaweza kuhusu tukio lolote la kijamii ambalo laweza kuwa la kishujaa au lisiwe la kishujaa. Makala haya yalikusudia kufafanua taswira ya kifo cha shujaa katika utendi kwa kurejelea kifo cha shujaa Liyongo kama alivyoelezwa katika kitabu cha *Tenzi Tatu za Kale* kilichohaririwa na Mulokozi mwaka (1999) na shujaa Imanuel (Yesu Kristo) kama anavyoelezwa katika *Biblia takatifu*.

Kabla ya kujikita katika ufafanuzi huo ni muhimu kufahamu dhana ya kifo, taswira, shujaa na utendi. Kwa kuanza na dhana ya utendi, Mulokozi (1999) anaeleza kuwa, utendi ni hadithi ya kishairi kuhusu mashujaa wa kihistoria na wa kubuni, wa jamii au taifa. Anaendelea kueleza kuwa baadhi ya tendi zina sifa za kiriwaya, ila tu badala ya kuwa katika umbo la nathari zina umbo la kishairi.

Vile vile Mulokozi (1999) anarekebisha kidogo fasili yake na kueleza kuwa utendi ni utungo mrefu wa kishairi wenye kusimulia hadithi ya ushujaa na mashujaa. Ukizichunguza fasili hizi utagundua kuwa tendi zina sifa ya kishairi, zinatokana na masimulizi (zilizo nyingi), zinahusu mashujaa ambao wanaweza kuwa wa kihistoria au wa kubuni. Pamoja na sifa hizo tendi pia huhusu masuala mengine ya kijamii kama vile kutoa mawaidha kwa jamii, hivyo si lazima utendi umhusu shujaa peke yake.

Dhana ya kifo inaweza kufasiliwa kuwa ni kitendo cha kutolewa uhai au kupatwa na mauti. Wamitila (2003) amefafanua dhana ya taswira kuwa hutumiwa kuelezea neno, kirai au maelezo ambayo yanaunda picha fulani katika akili ya msomaji. Anaendelea kueleza kuwa, taswira zinaweza kuwa za kimaelezo (yaani maelezo fulani yaliunda picha) au za ki-ishara (zinazounda picha ambayo inaashiria jambo fulani au imeficha ujumbe mwingine). Kwa mujibu wa Wamitila (2003) neno shujaa, hutumika kuelezea mhusika mkuu katika kazi ya kifasihi ambaye anaweza kuwa wa kike au wa kiume. Kimsingi neno hili haliashirii wema tu.

Mulokozi (1996) kwa upande mwingine ameeleza kuwa, mashujaa wa utendi wa Kiswahili ni wa aina tatu (3) ambazo ni mashujaa wa kijadi wa Kiafrika, kwa mfano Fumo Liyongo katika *Utendi wa Fumo Liyongo* Mohamed Kijumwa (1913) na Abushiri bin Salim katika *Utendi wa Vita vya Wadachi Kutamalaki Mrima* Hemed Abdallah K. (1895), mashujaa wa kidini, hasa mtume Muhamadi na masahaba wake (k.m. *utendi wa Ras 'lghuli*) na mashujaa wa kubuni kwa mfano Tajiri katika *Utendi wa Masahibu*.Mulokozi anaendelea kueleza kuwa, kati ya aina hizo tatu za mashujaa, riwaya ya Kiswahili imetumia mbili tu. Wahusika wa kijadi wa Kiafrika na wahusika wa kubuni. Wahusika wa kidini hawajatumiwa kikamilifu Kutokana na ufafanuzi huu ni dhahiri kuwa, mashujaa wa kidini bado hawajaelezwa ipasavyo na ndio sababu makala haya yalijikita katika kuelezea angalau

kwa sehemu kuhusu shujaa Emanuel katika *Biblia* akihusishwa na shujaa wa kihistoria na wa kijadi Fumo Liyongo katika *Utendi wa Fumo Liyongo.*

**2.4 Yaliyotafitiwa kuhusu Tamthilia Teule**

Utafiti wa Endovu (2017) ulifanywa ambao ulishughulikia suala la upole kama linavyodhihirishwa katika tamathali za usemi na ukuzaji wa maudhui katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*. Ametumia mtazamo wa Nadharia ya Brown na Levinson (1987) hasa kipengele cha mikakati ya upole. Data ya utafiti huu ilitokana na uchambuzi wa matamshi ya wahusika katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*. Lengo la mtafiti ni kubainisha iwapo tamathali za usemi hudhihirisha upole katika mazungumzo ya wahusikakinyume na ilivyo katika utafiti huu mwingine. Matokeo yake yanadhihirisha kuwa, tamathali za usemi katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* zimedhihirisha upole kutokana na namna wahusika wanavyoingiliana.

Lengo lake la pili ililikuwa ni kubainisha iwapo upole hudhihirika katika ukuzaji wa maudhui katika tamthilia ya *Mstahiki Meya.* Ijapokuwa mtafiti ameangazia upole katika ukuzaji wa maudhui, hajatathmini uathiriano, uigaji au urudufiano kama inavyotarajiwa kuangaziwa katika kazi hii. Aidha, kazi hii imechangia pakubwa katika kuelewa maudhui jambo ambalo litampa mtafiti uwezo wa kutathmini ujalizano katika kazi za fasihi teule.

Utafiti wake ulidhamiria pia kuchunguza iwapo miktadha mbalimbali ya mazungumzo huchangia kudhihirisha upole. Matokeo yanaonyesha kuwa, matumizi ya mikakati ya upole hudhihirika kupitia miktadha mbalimbali ya mawasiliano.Kwa jumla, utafiti huu umedhihirisha kuwa, upole una nafasi kubwa katika kuimarisha kazi ya tamthilia. Kwa hivyo, ndiposa mawasiliano yakamilike ni lazima viwango na matumizi ya mikakati ya upole ya wahusika yazingatiwe. Kazi yake haijalenga uathiriano, uigaji au urudufiano unaojitokeza katika tamthilia ya Mstaiki Meya jambo ambalo limeshughulikiwa katika kazi hii ya baadaye. Kazi hii imempa mtafiti msingi bora wa kuhakiki vipengele vya mwingiliano matini katika *Mstahiki Meya* kama mojawapo ya tamthilia teule kwa kuyaweka wazi masuala makuu yanoayojitokeza.

Utafiti mwingine ulilenga kuchunguza na kuchanganua mwingilianomatini kati ya tamthilia za *Mstahiki Meya* (2009) na *Mkaguzi Mkuu wa serikali* (1979). Katika kuhakiki hayo, ametumia nadharia ya Mwingilianomatini. Ameongozwa na malengo matatu ya utafiti kuchunguza jinsi tamthilia zinavyoingiliana kifani na kimaudhui vilevile kuchunguza iwapo nadharia ya Mwingilianomatini inafaa katika uhakiki wa tamthilia ya Kiswahili. Kutokana na utafiti huu, imebainika wazi kwamba Tamthilia ya *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* na *Mstahiki Meya* zinaingiliana katika vipengele vya msuko, usawiri wa wahusika, mandhari na maudhui.

Hatimaye, tulitoa mapendekezo kwa watakaofanya tafiti za baadaye kuhusiana na swala la kuingiliana kwa matini. Pendekezo hili lilimpa mtafiti changamoto la kuzama zaidi ili kuangazia mwingilianomatini katika kiwango cha kazi za fasihi tofauti bila kujikita kwa tamthilia tu. Mtafiti alipashwa mbinu mwafaka za kutathimini mwingilianomatini katika kazi za fasihi.

Mgawanyo wa wahusika katika kazi yoyote ya fasihi hujumuisha wahusika wakuu na wahusika wajenzi. Wahusika wakuu katika Tamthilia ya *Mstahiki Meya* ni Meya, Diwani I na II, Diwani III na Daktari Siki. Hii ni kazi yake Kamau (2015) ambaye ametafiti kuhusu mojawapo ya tamthilia teule za kazi hii. Alijikita katika mgawanyo wa wahusika jambo ambalo limewacha pengo la kiusomi kuhusu uathiriano. Hivyo basi kazi hii inatarijiwa kuziba pengo hilo. Hata hivyo, ni kazi ambayo imemwezesha mtafiti kuelewa zaidi tamthilia ya Mstahiki Meya hasa kuhusu kipengee cha uhusika.

Utafiti wa Massoud (2013) unahusu maudhui na fani katika tamthilia za kiswahili ambao umetumia mifano ya tamthilia ya *Mashetani* na *Kivuli Kinaishi*. Utafiti huu ni utafiti linganishi ambao ulilengakuchunguza mtindo wa kimaudhui na kifani katika tamthilia ya *Mashetani* na *Kivuli Kinaishi* ili kuona ni jinsi gani msanii anaweza kutofautiana ama kufanana na msanii mwingine katika uteuzi na utumizi wa vipengele vya kimtindo. Kwa vile utafiti wa wa Massoud ni linganishi, hali hii ya ulinganishi inaifanya kuwa sawa na utafiti huu ijapokuwa unalenga kazi tofauti. Aidha, unamfaa mtafiti kwa kumpa maarifa kuhusu ulinganishaji wa matini hali ambayo imwezesha kuafikia malengo yake.

Mtafiti Kipyegon (2013) amechunguza taswira chanya ambazo mwandishi anaangazia kumhusu mwanamke katika *Natala* na *Kifo Kisimani*. Pia, anachunguza changamoto zinazokabili mwanamke katika harakati zake za kujikomboa. Anaangazia nafasi na utambulisho wa mwanamke kama unavyodhihirika katika *Natala (*1997*)*. Anaangazia nafasi dhalilishi na dunishi. Kazi ya Kipyegon inaguzia tamthilia ya Kifo Kisimani ambayo ni mojawapo ya kazi teule katika utafiti huu. Mtafiti mtangulizi amwangazia mtafiti wa baadaye maudhui ya nafasi ya mwanamke katika tamthilia hii. Amempa mtafiti pengo la kiusomi ambalo analiziba kupitia utafiti huu. Aidha, amempa mtafiti ufahamu bora zaidi wa maudhui katika kazi hii.

## 2.5 Misingi ya Nadharia

Nadharia ya mwingilianomatini ni dhana inayohusishwa na mnadharia wa kifaransa Julia K.(1986) ambaye aliizua kutokana na nadharia ya usemezano ya Mikhail B. (1990),

wafuasi wa nadharia hii ya mwingilianomatini wanaoshikilia kuwa kazi za kifasihi kuingiliana na kuhusiana katika kile kinachoweza kuitwa "mwanda wa kimwingilianomatini. Makala haya yaliongozwa na mwega wa kinadharia wa mwingilianomatini. Ili hadhira ya fasihi ielewe, kazi yoyote ya fasihi lazima ihusishe vipengele vingine nje ya muktadha wa usomaji au usimulizi ule Mshengyezi (2003). Dhana ya kuingiza vipengele hivi ndiyo huitwa mwingilianomatini.

Wataalamu wanaounga mkono mawazo ya nadharia hii wanamtaja mwasisi wa nadharia hii kuwa ni Mikhail M. Bakhtin ambaye alikuwa mwanaisimu na mhakiki wa kazi za fasihi aliyeishi kati ya mwaka 1895-1975 Njogu na Wafula, (2007). Njogu na Wafula (2007) walizidi kusema kuwa Bakhtin aliamini kwamba kazi ya fasihi ina sauti mbalimbali zinazoingiliana na kupiga mwangwi katika kazi nyingine zilizotangulia, zilizopo au zitakazokuja baadaye. Ufafanuzi huo pia uliwahi kutolewa na Wamitila (2006) aliposema kuwa Bakhtin anaamini kuwa utanzu wa riwaya una uwezo wa kuingiza vipengele vya tanzu nyingine lakini ukabakia na sifa zake kama utanzu.

Hali hiyo ndiyo pia hujitokeza katika tendi mbalimbali za Kiswahili ambazo zina mwingiliano na vipengele vingi sana katika kazi moja. Kwa ufafanuzi wa Wamitila, utanzu wa fasihi kuwa na vipengele vingine ndani yake hakuondoi hadhi ya utanzu huo. Kwa ujumla, tunaposema kuingiliana kwa matini katika kazi za fasihi tunamaanisha kazi moja ya kifasihi kuwa na sifa za tanzu nyingine ndani yake.

### 2.5.1 Mihimili ya uingiliano matini

ii) Hali ya kazi za fasihi kurudufiwa/yaani unduma kuwili. Mfungamano wa maneno kujitokeza katika matini mbili katika usemi au mbinu za uandishi kama vile uradidi, mkazo au msuko katika matini mbili au zaidi. Mhimili huu utatumiwa katika kudondoa uingiliano matini katika msuko na mbinu za uandishi kama zinavyojitekeza.

ii) Ujinaishaji na urejeleo. Hii ni kama inavyojitokeza katika marejeleo.

iii) Hali ya ulinganishaji. Hali hii kuzuka kutokana na hali ya mtu kuingiliana na kazi fulani ya kifasihi. Mwandishi anaweza kutumia kazi iliyoandikwa kuleta dhana fulani katika kazi yake kwa njia inayoeleweka. Kama inavyojitokeza katika vitabu ambavyo vinakisiwa kulingana. Mhimili huu utatumiwa katika kubainisha ulinganisho uliopo katika kazi teule za fasihi ambazo zimetafitiwa.

iv) Mwandamo wa ushirikishi / Uathiriano. Ni hali ya kazi za fasihi kuathiriana. Mhimili huu utatumiwa kuonyesha jinsi kazi teule jinsi zimeathiriana katika utunzi.

v) Hali ya kazi za fasihi kuakisi kazi zingine. Hali hii hujitokeza pale ambapo kazi fulani ya fasihi inaakisi kazi nyingine. Mhimili huu utatumiwa kudhihirisha jinsi kazi moja inaakisiwa katika kazi nyingine.

vi) Uwekaji sambamba wa kazi za fasihi (*Juxtapositio*n). Ni usambamba unaojitokeza katika kazi za fasihi. Mhimili huu utatumiwa pamoja na mhimili wa ulinganishaji kudhihirisha kuwa kazi za fasihi si kazi tofauti bali ni sambamba.

Kwa mujibu wa Porter (1986), mwingilianomatini una vipengee vifuatavyo:

i. Uathiriano
ii. Urudufiano
iii. Uigaji
iv. Utafsiri
v. Wizi wa kitaaluma
vi. Unukuzi
vii. Utohozi

Mtafiti aliongozwa na vipengee vya kwanza vitatu.

# SURA YA TATU
# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Katika sura hii mtafiti ameonyesha kwa kirefu mbinu ya utafiti zilizotumiwa kukusanya na kuchanganua data. Utafiti huu ulitumia utaratibu wa maktabani ambapo tamthilia mbili na utendi wa Kiswahili ulisomwa. Miles na Huberman kama walivyotajwa na Kibaara (2012) wanasema kuwa katika uchunguzi wa kithamano deta inayokusanywa haiandikwi kihisabati. Hii inamaanisha kuwa hakuna hisabati lakini maelezo huzingatiwa kuliko nambari. Ili kuafikia haya mahali pa utafiti, kundi tafitiwa, sampuli, uteuzi wa sampuli na vifaa vya kukusanya data zilishughulikiwa katika sehemu hii.

## 3.2 Muundo wa Utafiti

Utafiti huu ulikuwa wa uchanganuzi wa yaliyomo. Utafiti wa kithamano unahusu mbinu, mipango na vifaa ambavyo haviwezi kutoa data yenye kutumia takwimu. Data ya kithamano hupatikana kwa umbo la maneno na mazungumzo, katika utafiti data ilikusanywa kutoka kwa matini teule. Mbinu iliyotumika kukusanya data ni ya uchanganuzi wa tungo teule. Hii ni kulingana na maelezo yanayoshikamana kimuwala namfumo wa kithamano., kutokana na hali za matini mbalimbali kuingiliana kwa kujitokeza katika kazi hizi tofauti za kifasihi. Mtafiti alisoma kazi teule na kuonyesha jinsi matini hizi zilivyoingiliana katika uwasilishaji. Uchanganuzi huu ulihusu maelezo ya kina jinsi kazi mbalimbali zinavyoakisiwa katika kazi za waandishi wengine.

## 3.3 Mahali pa Utafiti

Utafiti huu ulishughulikia uchanganuzi wa mwingilianomatini katika tungo teule za fasihi ambazo ni za *Utendi wa Fumo Liyongo*, *Kifo Kisimani* na *Mstahiki Meya*. Tungo hizi zitapatikana katika maktaba kwa hivyo utafiti utafanyika maktabani. Mahali hapa paliteuliwa kwa kuwa vitabu vilipatikana maktabani na kwa hivyo data iliyotarajiwa kukusanywa ilipatikana huko. Mathalani, ili kutimiza malengo ya utafiti huu, mtafiti alitembelea maktaba. Mtafiti alisoma matini za mwingilianomatini na tasnifu zilizoandikwa kuhusiana na mada hii ya utafiti. Mtafiti pia alisoma tungo ambazo aliziteua kimaksudi na kuzichanganua kwa kuongozwa na nadharia ya mwingiliano matini.

## 3.4 Walengwa

Katika utafiti, kundi tafitiwa kwa hakika halimaanishi tu watu, mbali linaweza kurejelea matini, taasisi ama kitu chochote kinachochunguzwa (Daecon na wenzake 1999:

41). Kundi tafitiwa la utafiti huu lilikuwa ni matini za *Utendi wa Fumo Liyongo*, *Kifo Kisimani* na *Mstahiki Meya*.

### 3.5 Sampuli

Sampuli katika utafiti huu ilitokana na kundi tafitiwa kama ambavyo limetajwa hapo juu lilitokana na matini katika tungo za *Utendi wa Fumo Liyongo*, *Kifo Kisimani* na *Mstahiki Meya*. Sampuli hii ni tungo ambazo zinaadhihirisha hali ya ujalizano ambao mtafiti alikusudia kubainisha kwa uwazi kwa kufanya utafiti. Katika tungo hizi mtafiti alilenga kipengee cha uhusika na maudhui katika utafiti huu ambapo aliangazia mwingilianomatini katika nafasi zao, sifa na umuhimu wao.

Katika utafiti huu, sampuli ilitumika kimakusudi. Uteuzi huu ulitumika kwa sababu mtafiti alihitaji ya matini maalum zilizoafiki malengo ya utafiti wenyewe. Ni kutokana na hali hii ya kusoma makala na tungo za fasihi ambapo mtafiti alikutana na tungo hizi.  Hali ya ujalizano ilichunguzwa kwa msingi ya mwingilianomatini kwani ilisaidia kuleta uelewekaji.

### 3.6 Ukusanyaji wa Deta

**Hatua ya Kwanza**

Kwa kizingatia vipengele vya vitatu vya mwingilianomatini: uigaji, uathiriano na urudufiano data  iliainishwa kwa kutumia mbinu ya mara tokezi.

**Hatua ya Pili**

Kutoa muhtasari wa vipengele vya mwingilianomatini na vilivyotumika katika kazi teule. Lengo lilikuwa nikutambua vipengele vipi vya mwingilianomatini vilivyotumika zaidi katika kiwango cha uhusika na msuko huku mtafitiakiongozwa na mhimili wa uathiriano wa hali ya kazi za fasihi kuakisi kazi zingine za fasihi.

**Hatua ya Tatu**

Kuchanganua vipengele vya uhusika. Katika kiwango hiki mtafiti aliongozwa na mhimili wa nadharia ya mwingilianomatini wa hali ya ulinganishaji na pia mhimili wa uathiriano.

**Hatua ya Nne**

Kutathmini vipengele vya urudufiano katika kiwango cha msuko katika kazi teule za fasihi.

**Hatua ya tano**

Data iliyokusanywa ilinakiliwa, ikatathminiwa na kuwekwa kikategoria na kutumiwa kama ushahidi wa kujaribia na kujibu maswali ya utafiti.. Katika kuchanganua data, hali ya mwingilianomatini katika tungo teule za fasihi ilibainishwa kwa misingi ya uchanganuzi matini.

**3.7 Uchanganuzi na uwasilishaji wa data.**

Mbinu ya uchanganuzi wa yaliyomo ilitumiwa kukusanya data kwa kufuata utaratibu ufuatao:

Mtafiti alisoma kwa makini kazi tatu alizochagua na kuainisha vipengele vya mwingilianomatini. Mbinu ya usambao wa maratokezi ilitumika kutafuta vipengele vya msuko na uhusika.

Mtafiti alianza kwa kuorodhesha hali ya msuko wa tungo zote tatu. Baadaye alichunguza uathiriano na uigaji ulipo kama vipengele muhimu vya mwingilianomatini. Aliongozwa na vigezo viwili ambavyo ni:

i. Vitushi
ii. Umantiki

Katika uhusika na wahusika, mtafiti aliongozwa na vigezo vifuatavyo:

i. Majina ya wahusika katika tungo zilizo teuliwa
ii. Wasifu wa wahusika katika matini za fasihi zilizotuliwa.
iii. Migogoro anaopambana nayo kila mhusika
iv. Mazingira ya wahusika wanaoathiriana katika kazi za kifasihi zilizoteuliwa.
v. Dhima ya wahusika katika matini za kifasihi.
vi. Idadi ya uhusika katika tungo zilizoteuliwa.

Maudhui yalichunguzwa kwa kuzingatia vigezo vitatu kwa mujibu wa Wamitila(2008). Vigezo hivyo ni:

i. Dhamira
ii. Ujumbe
iii. Mtazamo na msimamo

Kwa kuwa utafiti ulihusisha mbinu ya uchanganuzi wa yaliyomo, takwimu elezi zilitumiwa. Hatua hii ilimwelekeza mtafiti kutambua ufasili mpya wa tungo hizi zilipofasiliwa kwa vigezo na mihimili ya mwingilianomatini. Mbinu ya kimaelezo ilitumiwa kueleza namna vipengele vya uhusika na msuko na maudhui kwa takwimu elezi.

# SURA YA NNE
# UCHANGANUZI NA UFASIRI WA DETA

## 4.1 Utangulizi

Utafiti huu ulichunguza mwingiliano na ujalizano uliopo katika kazi teule za fasihi. Utafiti ulidhamiria kuangazia ujalizano na mwingiliano uliopo katika viwango vya msuko, wahusika, uhusika na maudhui. Aidha, mtafiti aliongozwa na nadharia ya mwingilianomatini ili kuyaweka masuala aliyokusudia wazi. Hivyo basi, mtafiti alionyesha jinsi mwingiliano matini unavyoelekeza ufasiri wa kazi ya fasihi.

Katika sura hii, mtafiti ameonyesha jinsi msuko wa matini tatu teule ambazo ni utendi wa *Fumo Liyongo*, *Kifo Kisimani* na *Mstahiki Meya*. Uathiriano uliopo katika msuko umebainishwa. Mtafiti aliangazia suala la urudufiano uliopo katika wahusika na uhusika. Mwandishi ameangazia namna uathiriano, uigaji na urudufiano unavyoelekeza ufasiri wa kazi za fasihi. Katika kila kiwango, mifano mahususi imedondolewa kutokana navitabu teule ili kuthibitisha yanayozungumziwa. Uchanganuzi na ufasiri wa deta uliongozwa na nadharia ya mwingilianomatini ikijikita katika vipengee vitatu vya mwingilianomatini ambavyo ni uathiriano, uigaji na urudufiano.

## 4.2 Uathiriano katika kiwango cha Msuko, Urudufiano katika Wahusika na Uhusika

Katika kiwango hiki, mtafiti aliangazia uathiriano katika kiwango cha msuko na urudufiano uliopo katika kiwango cha wahusika na uhusika. Hali hii iliongozwa na mawazo ya wataalamu mbalimbali kuhusu uhusika na msuko. Msuko ulimpa msomi wa kazi hii nafasi ya kuelewa kazi teule za kifasihi zinahusu nini hasa. Aidha, mtafiti anapiga hatua zaidi kujadili hali ya uathiriano uliopo katika kiwango hiki cha msuko. Wahusika na uhusika wao nao walitathminiwa ili kubainisha kwamba kazi teule za kifasihi zinaathiriana.

### 4.2.1 Msuko wa Utendi wa Fumo Liyongo

Kwa mujibu wa TUKI (2011) Msuko ni dhana ya kimtindo ambayo huelezea namna mwandishi anavyofuma mawazo yake ili kupata umantiki katika kuwasilisha mawazo yake. Aidha, Senkoro (2011) anaelezea kwamba wahusika ni watu au viumbe waliokusudiwa wawakilishe dhana, mawazo au tabia za watu katika kazi za fasihi. Hiki ni kipengele muhimu cha kuzingatia katika ulinganishaji wa kazi za fasihi.

Kisa cha Liyongo kinahusu mgogoro kati ya Fumo Liyongo na kaka yake, mfalme wa Pate, ambaye katika utendi huu hatajwi jina bali katika mapokezi mengine anaitwa Daudi Mringwari. Hadithi inaanza Liyongo akiwa ni kijana amekwisha baleghe, mwenye kusifiwa

nchini kote kwa nguvu na ushujaa wake. Anaishi nyumbani kwake Ungwana wa Mashaha ambalo ni eneo la Shaka, jimbo la Ozi.

Mjumbe wa Wagalla unafika Pate kumtembelea Sultan Daudi. Sultan huyo anamsifia Liyongo kwa Wagalla, lakini wao hawaamini maneno yake. Anaamua kumpelekea Liyongo barua ya kumwita aje Pate ili Wagalla wamwone. Liyongo, anapopata barua hiyo anafunga mizigo yake na kuanza safari ya kwenda Pate. Ni mwendo wa siku nne, lakini Liyongo anatumia siku mbili tu. Anapokaribia mji wa Pate anapuliza panda yake,inapasuka. Mji wote unasikia na kujua kuwa Liyongo ameingia. Anapuliza panda ya tatu na kuingia mjini hadi barazani kwa Sultan. Watu wanakusanyika kumwona. Anatua mzigo wake na kutoa vitu vya kutosha kujaza nyumba nzima.

Wagalla wanakiri kuwa kweli Liyongo ni mtu mwenye nguvu. Wanamwomba Sultan awaruhusu wapate mbegu yake. Sultan anakubali, Liyongo anaozwa mke wa Kigalla ambaye anamzalia mtoto wa kiume. Anamlea vizuri mtoto huyo hadi anakuwa kijana mzuri mwenye nguvu. Sifa za Liyongo zinavyozidi kuenea ndivyo fitina za Sultan zinavyozidi. Mfalme anahofu kuwa Liyongo atamnyan’anya ufalme.

Mwisho Liyongo anagundua kuwa mfalme anataka kumua; anaondoka Pate na kwenda kuishi nyikani miongoni mwa Wasanye na Wadahalo wamwue Liyongo huko mwituni. Anaahidi kuwatuma Wadahalo wanaofanya urafiki na Liyongo, halafu wanashauri wawe wakila pamoja kikowa. Chakula wanachokula ni makoma, ambayo wanapeana zamu za kuyaangua kutoka mtini. Zamu ya Liyongo inapofika, wanatarajia kwamba atapanda juu ya mkoma kuangua makoma, na wao watapata nafasi ya kumuua kwa mishale yao akiwa kule juu ya mti. Kwa bahati Liyongo anagundua hila yao na kuamua kuangua makoma kwa mishale yake kutoka chini. Hivyo hawafanikiwi kumuua.

Wasanye na Wadahalo wanakwenda mjini na kumweleza Sultan kuwa kuua Liyongo haikuwezekana. Sultan anmwambia warudi porini wamweleze Liyongo kuwa mjini hakuna hatari tena, halafu waende naye mjini. Wanarudi na kumweleza hivyo. Liyongo anamwamini na kurudi nao mjini Pate. Baada ya siku chache Sultan anaitisha ngoma, akiwemo Liyongo. Wakati wa ngoma hiyo askari wanamzunguka Liyongo na kumshika. Anatiwa gerezani na kuamuliwa auawe. Siku ya kuuawa inapokaribia, Liyongo anaambiwa afanye ombi lake la mwisho. Anaomba apigiwe ngoma ya mwao na gungu. Wakati ngoma inaandaliwa anampelekea mama yake ujumbe wa kishairi kupitia kwa kijakazi Saada ambaye humletea chakula kila siku kwamba siku hiyo ampikie mkate wa wishwa na kati yake atie tupa ya kukatia vyuma. Mama yake anafanya hivyo. Askari wanamyang’anya Saada mikate mizuri na kuacha ule wa wishwa anampelekea Liyongo. Ngoma yake inapoanza kupigwa, Liyongo

anatoa ile tupa na kukata minyororo iliyofungiwa, kisha anavunja lango la jela na kutoroka na kurejea nyikani.

Wakati jaribio hilo liliposhindwa, Sultan anamshawishi mwanawe Liyongo aende kwa baba yake na amwulize ni kitu gani kiwezacho kumuua. Anamwahidi kumpa uwaziri na kumwoza binti yake iwapo atafanikiwa. Mwanawe anafululiza hadi Shaka kwa baba yake na kumwuliza swali hilo. Liyongo anatambua kuwa kijana huyo alikuwa ametumwa na adui yake lakini bado anakubali kumwambia siri yake kuwa kimuuacho ni sindano ya shaba ikimchoma katika kitovu chake. Kijana anarudi kwa sultani na kumweleza alivyoambiwa. Sultan anafurahi, anampa zawadi nyingi, halafu anampa sindano ya shaba na kumwambia arudi tena kwa baba yake akamuue.

Kijana anarudi kwa Liyongo anasubiri hadi baba yake anapolala usingizi, halafu anamchoma sindano ya shaba kitovuni. Liyongo anatoka usingizini kwa ghadhabu, anachukua upinde wake na kwenda kisimani, anapiga goti na kutia mshale katika upinde huku kauelekeza mjini na kukata roho. Watu wanapomwona wanadhani yu hai, hivyo kwa siku tatu wanaogopa kwenda kisimani kuteka maji. Mwisho wanamtuma mama yake aende akabembeleze aondoke pale ili wateke maji. Mama yake anakwenda hapo kisimani kila siku kumbembeleza kwa mashairi bila mafanikio. Mwishoni maiti ya Liyongo inaoza na kuanguka. Na ndipo wanapobaini kuwa yu marehemu.

Mfalme anapopata habari ya kifo chake anafurahi sana. Anamwita mtoto wa Liyongo na kumweleza habari ya kifo cha baba yake. Yule kijana badala ya kulia anacheka. Mfalme anakasirika na kumyang’anya nguo na vitu vyote alivyompa, kisha anamfukuza mjini, anakimbilia porini kwa Wagalla na kufia huko.

### 4.2.3 Msuko wa Kifo Kisimani

Mchezo unaelezea kuhusu utawala wa Mtemi Bokono. Mchezo unaanza asubuhi ambapo viti vimepangwa tayari kwa mkutano wa Mtemi Bokono. Mwelusi ambaye ni kijana anaingia uwanjani na kutoweka baada ya muda. Anamkuta Mama Kaloo akiwa anafagia na kupanga viti tayari kwa mkutano. Mwelusi ana mawazo ambayo yanadhihirika kupitia uzungumzi nafsia wake. Hafurahishwi na jinsi Mtemi Bokono anavyowanyanyasa Wanabutangi.

Kaloo anafikiria kuwa Mwelusi ni mmoja wa watu ambao wameanza kuhudhuria mkutano wa Mtemi Bokono. Kinyume na hayo, Mwelusi anamkejeli Mtemi Bokono kwa ubinafsi wake. Batu anaingia na kuanza kuzunguka uwanja. Batu ndiye mshauri mkuu wa mtemi Bokono. Baada ya muda agundua kuwa watu wamekataa kuhudhuria mkutano wa Mtemi

Bokono. Bokono anapofika anakuta uwanjani hakuna watu. Kaloo, Gege ambaye ni nduguye Mwelusi anaingia uwanjani. Gege anaunga mkono ungozi wa Mtemi Bokono jambo ambalo linamuudhi nduguye Mwelusi. Walioko uwanjani wanaanza kusifu Mtemi punde tu anapoingia. Wanamsifu kuwa ataongoza Butangi miaka mia moja.

Hali ya watu kutoudhuria mkutano linamuudhi Mtemi Bokono sana jambo ambalo linamsukuma kumshinikiza mshauri wake mkuu ambaye anaitwa Batu kufanya uchunguzi halafu ampelekee jibu. Ukweli ni kwamba, watu wamechoka na uongozi mbaya wa mtemi baada ya kuzinduliwa na Mwelusi.

Butangi ina majengo ya utawala. Katika majengo haya ndipo anapoishi Mtemi Bokono. Mwandishi anatupatia picha ya Mtemi Bokono ambaye hafurahishwi na hali ilivyo baada ya watu kutohudhuria mkutano. Bokono anasimama huku akiangalia vitu vilivyo ukutani na mara kwa mara anagusa hiki na kile. Mkewe anayeitwa Nyalwe amekaa kitini raha mustarehe, akijipepea. Wana mfanyikazi anayeitwa Mgezi. Mgezi anakuja hadi alipo Nyalwe na kumuambia kuwa chakula kiko tayari.

Wanaketi mkekani ili wale. Wanapokaa ili wale Bokono hali chakula ana wasiwasi sana. Nyalwe anapomuuliza ni kwa nini hali anamjibu kwa kejeli na kumuuliza juu ya vyeo vyake; mke, mwandani na msiri wake. Nyalwe alitaka kujua kinachokuwa kikimsumbua mumewe kiasi kwamba hataki kula.

Nyalwe anamueleza mumewe kuhusu ndoto ambayo mumewe alikuwa ameiota usiku. Alikuwa anaota akiwa anafukiwa kaburini akiwa angali hai. Nyalwe anapoeleza mumewe kuhusu ndoto yake, Mtemi Bokono anakubali kuwa ana hofu ya kunyang'anywa utawala. Nyalwe anamuomba abadilishe mienendo yake na anamuonya dhidi ya vibaraka wake wanaomdanganya kuwa anapendwa na Wanabutangi.

Bokono anakataa kuwa anadanganywa na kusema kuwa ni kweli anapendwa na Wanabutangi. Anamkasirikia mkewe na kumuona kuwa ni kama anaungana na mahasidi wake kumwangamiza kisiasa. Anakanusha madai kwamba Batu anampotosha kiushauri na kuendelea kumwamini. Mkewe anamwacha na kujipa shughuli na mambo mengine. Mara anasikia Bokono anapiga duru kuwa ameumwa na bafe. Anaashiria ukutani kuwa hapo ndipo Bafe alipo. Ukweli ni kwamba hakuna Bafe na hivyo anaashiria kuwa amechanganyikiwa. Ni hofu tu, hakuna bafe yeyote humo ndani.

Baada ya utulivu wa Bokono, mara mgeni anaingia. Alikuwa ni mama Agoro ambaye alikuwa amekasirishwa na wazo la uwanja wa watoto wa kuchezea kunyakuliwa. Uwanja huo ulikuwa umenyakuliwa kwa matumizi ya kibinafsi. Aidha, jambo hilo halimfuraishi Mama Agoro na hivyo anakubali kutumwa na wengine ili kuuliza vile hali ilivyo.

Mandhari yanabadilika kutoka kwa makao makuu ya utawala wa Butangi na kuwa ni katika Gereza. Yule kijana anayeitwa Mwelusi alikuwa tayari amekamatwa na kutiwa gerezani. Amekamatwa kwa madai kwamba yeye ndiye amechochea watu wasihudhurie mkutano wa Mtemi Bokono. Ametiwa gerezani ambapo analindwa na Askari I, Askari II na Askari III. Kabla hajapelekwa gerezani ametiwa ndani na makachero. Makachero hawa ndio wanaanza kumdhulumu mhusika huyu.

Makachero hawa wanaitwa Mweke na Talui. Mweke na Talui wanaanza kumdhulumu. Wanaanza kwa kumuita mtukufu mtemi na anaponyamaza wanazidi kumchapa na kumsukuma hapa na pale. Mwelusi analalamika kuwa taya zake zinawaka moto kwani waliodai wamekuja kuzungumza naye wanafanya hivyo kwa mateke na makofi. Wanamhoji Mwelusi na kumuuliza kama yeye ni Mwelusi wa Biuki na kama anatoka kijiji cha Bunyanya na ukoo wa Langine. Anapojibu wanamsifu na wanazidi kumchapa.

Makachero wanamuuliza kama yeye ndiye kiongozi wa kundi la Kabakaba. Mwelusi anakiri kuwa yeye hajui kundi la aina hiyo. Mwelusi anapokataa wanazidi kumchapa. Batu anaingia na kuwakataza kumchapa. Anaomba nafasi ili azungumze naye. Kwa upole anamshawishi Mwelusi akiri kuwa ndiye kiongozi wa Wanamapinduzi na aombe msamaha kwa Mtemi Bokono.

Mwelusi anapolia juu ya maumivu Batu anamwambia kuwa atapewa dawa nzuri akitoka gerezani. Batu anamwacha Mwelusi peke yake kwani anadai kuwa akili ya binadamu hufanya kazi vizuri akiwa peke yake. Anaporudi anapata kuwa Mwelusi bado hajaamua. Anataka akiri kwamba anatumiwa na majirani ili kuchafua Butangi. Mwelusi anapokataa kukiri basi naye Batu anakasirika na kudai kwamba amepotoshwa. Anatoa agizo kwa Askari waendelee kumdhulumu na kuondoka. Mwelusi anaendelea kufungiwa gerezani.

Wafungwa gerezani hawapewi chakula bali wanategemea chakula wancholetewa na watu wao. Kwa mfano, Mwelusi analetewa chakula na dadake anayeitwa Andua. Jambo la kushangaza ni kwamba, hata baada ya kuletewa chakula kutoka nyumbani, Askari wanaolinda gereza wanakula chakula chenyewe na labda kumpa mfungwa makombo. Ili kufanikiwa katika mbinu zao, wanamkataza jamaa ya mfungwa kumuona mfungwa. Askari I na Askari II wanaanza kula chakula cha mfungwa licha ya kukatazwa na Askari I. Katika hali ya kukataza kula chakula cha mfungwa hali ya mtafaruku inazuka kati yao. Askari I anawarejelea kuwa ni walafi. Baada ya kutulia Askari III alinza kuelezea jinsi walivyomnyanyasa mfungwa mmoja. Ana wasiwasi kuwa ikiwa utawala wa Mtemi huenda ukafika mwisho.

Mwandishi anaendeleza matukio katika kiambo cha Tanya ambaye ni mamake Mwelusi. Tanya ameketi akidondoa nafaka. Gege ambaye ni nduguye Mwelusi amekaa karibu na uzio akiukaguakagua. Punde anauachilia na kuanza kujishughulisha na utengenezaji wa ala ya muziki. Mamake anamuuliza kwa nini hajaenda kumtazama nduguye, Mwelusi kule gerezani. Gege anamwambia mama yake asimzomee. Anaendelea kutengeneza ala na kusema kuwa wasichana watamtambua. Katika kumbukumbu zake Mwelusi anarejea na kumuuliza hali ya uwanja wa ngoma. Wazungumza kuhusu hali ya Butangi. Gege anamshurutisha nduguye kwa kujali jamii kila mara na kusahau maisha yake mwenyewe. Mwelusi anamuomba aionee huruma Butangi na awe mzalendo.

Gege anapoendelea na mawazo yake, Andua anarejea nyumbani kutoka kisimani. Anarejea upande mmoja wa uso wake ukiwa na jeraha. Anamwambia mama yake kuwa hakupigana mbali amechapwa na Askari. Askari wamemchapa wakimzuia kutega maji katika kisima cha Mkomani kwa kudai kuwa hawaruhusiwi. Wakati huo naye Azena anawatembelea na kumtuliza Tanya kuhusu maumivu aliyonayo kwa sababu ya bintiye na mwanawe ambaye yuko gerezani. Tanya anamwelezea kuwa hata chakula hakimfikii. Anamuomba asife moyo na aendelee kumpelekea chakula.

Baada ya Tanya kuhimizwa na Azena asife moyo, anaamua kumpelekea Andua chakula gerezani mwenyewe. Tanya alitaka pia kuonana naye. Wakati huu amempelekea chakula. Atega pia naye analeta chakula. Katika chakula alichokuwa nacho Atega kulikuwepo pia na mkate wa wishwa na tembo. Askari wanamkataza Tanya kumwona mwanawe na kuelezea kuwa watampa chakula wenyewe licha ya kushawishiwa na Askari I. Askari wanakula chakula na kumpa Askari I ampe mfungwa mkate wa wishwa.

Askari I anakataa kushiriki katika ulevi. Anatoa hadithi kuhusu yaliyompata Makea. Askari II na III wanapolewa, kumbe naye Mwelusi anaendelea kukeketa minyororo iliyokuwa imemfunga kwani Atega alikuwa ameweka tupa ndani ya ule mkate wa wishwa. Ghafla umati wa watu unakuja kumtoa Mwelusi kwa kuwa Askari walikuwa wamelewa chakari.

Baadaye, habari zinamfikia Mtemi Bokono kuwa Mwelusi ametoroka Gerezani. Hali hii inasababisha mkutano kati ya Bokono na vibaraka wake. Lengo la mkutano huu ni kupata suluhu la Mwelusi na uchochezi wake. Kabla hawajapata habari ya kutoroka kwa Mwelusi, walikuwa wanatoa maoni kuwa auliwe. Aidha, Kame alipinga wazo hilo.

Mshauri mkuu wa Mtemi, Batu, anatumia makachero; Mweke na Talui kumshawishi Gege. Anamwambia amlete Gege pale na kumshawishi Gege kuwa wakimsaidia

kumwondoa Mwelusi basi watampa bintiye Mtemi anayeitwa Alida kuwa mkewe. Anahaidiwa mali nyingi pia.

Baada ya Gege kushawishiwa na kushawishika, anamwendea mamake ambaye yuko nyumbani na kumwuliza aliko Mwelusi. Batu naye anamwuliza Tanya akubali kumshawishi mwanawe ili akubali kuacha uchochezi. Azena naye anaingia huku akitembea kwa shida. Anasema kuwa tatizo lake ni kuwa walivamiwa na majirani zao. Ukweli ni kwamba si majirani waliowavamia bali ni wahuni waliokuwa wamelipwa na utawala wa Mtemi Bokono. Mwelusi na Atega wanajaribu kuingia nyumbani lakini wanatoroka baada ya kuelekezwa na Azena kuwa Batu yuko hapo.

Mwelusi walipotoroka walielekea kisima cha Mkomani ambapo wanaenda kukanusha madai kuwa maji ya kisima hicho hayaruhusiwi kuchotwa na umma. Ni asubuhi, Zigu amesimama huku macho akiwa na kisu mkononi tayari kumkabili yeyeote atakye kiuka kanuni. Andua anapoenda kuteka maji, zigu anamkataza. Baadaye Atega na Mwelusi wanamwambia kuwa wako tayari kuvunja kanuni lakini Zigu hamtambui Mwelusi. Zigu yuko tayari kutetea kanuni za kisima naye Mwelusi, Atega na Andua wako tayari kudai haki ya Wanabutangi ya kuteka maji. Gege naye anakuja na kumwambia Mwelusi kuwa alitaka kumwona. Anamdaganya waende chemba. Walipoenda chemba, Gege alimkabili nduguye kwa kumchoma kisu tumboni hali ambayo ilisababisha kifo chake.

Kutamatisha tamthilia hii, mwandishi anatuelekeza katika ukumbi wa utawala wa Butangi. Kiti cha mtemi kiko mahali pake lakini hakina mtu. Batu pia yuko ukumbini. Nyalwe anaingia kwa wasiwasi na kumwonya mumewe kuwa kuna umati unaokuja. Mtemi Bokono anapuuza. Ghafla wanaingia watu ambao wamechoshwa na udhalimu wa Mtemi Bokono. Wako tayari kumwua lakini Atega anawaonya wasimwage damu. Wote wanafungwa kwa kamba na kupelekwa kizuizini. Wanamwacha mkewe Bokono kwa madai kuwa hakuhusika katika uovu wa mumuwe. Wanabutangi wanapata ukombozi wao kwa kuhitimisha uongozi wa kidhalimu wa Bokono.

### 4.2.3 Msuko katika Mstahiki Meya

Tamthilia hii inaelezea kuhusu utawala wa Mstahiki Meya ambaye ni kiongozi anayesimamia Baraza la mji wa Cheneo. Wamechaguliwa na umma ambao ni watu wa eneo la Cheneo. Wanacheneo wana matumaini nao kuwa watawaboreshea hali ya maisha. Aidha, Mstahiki Meya, Diwani I na Diwani II wanasahau majukumu yao kama viongozi na kuungana na Bili ambaye anawashauri vibaya. Wanatumia nafasi zao kujinufaisha wenyewe.

Ni dhahiri kuwa Mstahiki Meya hajali maslahi ya Wanacheneo waliomchagua ambao wanaishi katika hali mbaya ya maisha. Aliposhika usukani alianza kuendeleza ufisadi kama njia ya kujilimbikizia mali akiwa na rafikiye Bili. Ananyakua viwanja vya umma na kumgawia rafikiye Bili. Wanauza vipande hivyo ili kuishi maisha ya kifahari kama vile kumpeleka mkewe ng'ambo akajifungulie huko. Wanamfanyia hila mwanakandarasi wa Baraza ili watumie nafasi hiyo kupora mali yauma pia. Bili anamshauri kulishtaki Baraza ili alipwe fidia kisha amgawie kiasi fulani cha pesa atakazolipwa kama fidia. Bili anamshauri Meya wauze fimbo ya umeya ili wapate pesa za kujilipa marupurupu.

Diwani III ni tofauti na Diwani I na Diwani II. Diwani III ni tofauti nao kwani anajali maslahi ya Wanacheneo. Madiwani wa Baraza la mji wa cheneo wanaunga mkono mkono sheria zinazowakandamiza Wanacheneo. Sheria hizo ni kama kutotozwa kodi kwa madiwani ilhali wafanyikazi wengine kama mama muuza ndizi wanatozwa kodi. Zaidi ya hayo, wanakubaliana kujiongezea mshahara zaidi. Mwanya mwingine wanaotumia kujinufaisha ni kupitia kuunga mkono kamati za madiwani ambazo hazina manufaa kwa Mwanacheneo wa kawaida.

Ubadhirifu unaendelezwa na viongozi ambao wanatumia pesa za umma vibaya pasipo kujali. Kwa mfano, Meya atengewa pesa za kujinafasi ambazo anajumuisha Bili katika kujinafasi. Bili na familia yake wanaungana na familia ya Meya katika hoteli ya Kajifahari. Anawapangia karamu kubwa Mameya ambao wanatarajiwa kuzuru eneo lake. Anawatafutia vyakula vya bei ghali pamoja na kuagiza mvinyo kutoka Ufaransa. Ubadhirifu zaidi unajitokeza wakati Meya anamuita mhubiri aje kuiombea Baraza. Anamlipa shilingi laki moja kila mwezi na kugharamia petroli ya kumleta barazani na kumrudisha nyumbani. Anawalipa madiwani ovataimu pia. Bili naye analipwa kwa huduma ambazo anatoa kwa Baraza ilhali nafasi yake haijatambulika kikatiba. Istoshe, anatoa ushauri mbaya unaompotosha Meya. Ubadhirifu huu ukiendelea, wanacheneo wanakosa chakula na huduma za kimsingi kama vile elimu na matibabu.

Ubadhirifu wa Meya umesababisha nakisi katika baraza la cheneo. Baraza lina nakisi ya shilingi milioni mia moja na ishirini. Haliwezi kulipa mishahara ya wafanyikazi. Hali hii inasababisha baraza kutegemea mikopo kutoka nchi za ulaya. Mikopo yenyewe inapopatikana inatumika vibaya na hivyo kuzidisha nakisi.

Wanacheneo wamekosa huduma za kimsingi kama vile elimu. Meya mwenyewe anakiri kwamba elimu ya Wanacheneo ni ya kiwango duni kabisa. Hali hii inasababisha kuwapeleka wanawe ng'ambo wakasomee huko. Sekta ya afya imeathiriwa pia. Hakuna

dawa hospitalini na wauguzi na madaktari hawalipwi pia. Mstahiki Meya anampeleka mkewe ng’ambo kujifungulia huko. Meya anawadaganya Waridi na Siki kuwa dawa ziko njiani.

Hali hii ngumu ya maisha inasababisha migomo ya wafanyakazi. Wafanyakazi wa baraza wanagoma kudai nyongeza ya mishahara. Wanapogoma na kuandamana, wanafurushwa na Askari ambao wamelipwa na Meya. Istoshe, Meya anatisha kuwafuta wafanyakazi ambao wamegoma huku akidai kwamba kuna wengi ambao wamesoma na hata kazi ya utopasi hawana.

Mwandishi anaelezea mbinu zilizotumika na Mstahiki Meya kujidumisha mamlakani. Mstahiki Meya anatumia vitisho, polisi, ubaguzi, vishawishi na propaganda. Meya anambagua Diwani III kwa kuwa ni mwadilifu na anatetea maslahi ya wafanyakazi. Diwani III hafurahishwi na jinsi wafanyakazi wanafyodhalilishwa na viongozi. Meya amemtenga kiasi kwamba anafanya mikutano mingine bila kumjumuisha. Anadaganya kuwa dawa ziko njiani ilhali hakuna dawa ambazo zimeagizwa. Anawahonga Askari ili wamtii kwa kila jambo na hasa kuwatawanya wale wanaogoma. Anatumia vitisho kwa waliogoma kuwa atawaachisha kazi halafu kuajiri waliohitimu chuoni na hawana kazi. Alitumia idhaa kwa kuamrisha idhaa ya taifa kucheza nyimbo za uzalendo kabla na baada ya vipindi maarufu. Anatumia mbinu hii kama njia ya kuwapumbapaza wanyonge Cheneo.

Utawala wa Mstahiki Meya unawatelekeza wanyonge. Wanawalipa wanyonge mshahara duni ambao hauwezi kuyakidhi mahitaji yao ya kimsingi kama vile chakula na mavazi. Mwandishi anaeleza kuwa Wanacheneo wanakula Makombo na mizizi na hata matunda mwitu. Mwanawe Dadavuo Kaole alimpa mwanawe maharage yalolala kwa kuwa hakuwa na chakula kingine cha kumpa. Zaidi ya hayo, hakuweza kukitokosa chakula hicho kwa kuwa hakuwa na mafuta taa na bei ya makaa pia ilikuwa juu.

Dadavuo Kaole anakuwa mgonjwa na hivyo kupelekwa zahanatini. Anapopelekwa zahanatini inadhihirika kuwa hakuna dawa na hivyo kupewa huduma ya kwanza tu. Ni dhahiri kuwa wengine wanajifia huko kwa kukosa matibabu kama anavyoeleza mhusika Waridi. Watoto wa maskini wanatembea kwa miguu kwenda shuleni. Wafikapo shuleni wanafukuzwa kwa kukosa karo. Watoto wa madiwani wanapelekwa shuleni kwa magari yenye *air conditioner* ambayo ni ya serikali. Wafanyikazi wanaishi katika mabanda. Madiwani wanaishi kwa makasri yaliyorembeshwa. Wanacheneo wanaendelea kuangamia lakini jambo hili halimtishi Meya. Anapoambiwa kuwa kuna mtoto amekufa anasema kuwa ni mmoja tu.

Hali ya maisha ya wafanyakazi yaendelea kuwa mbaya zaidi. Mstahiki Meya hataki kuwapatia nyongeza ya mishahara. Baraza lina pesa za kuwapa madiwani lakini halina pesa

za kuwapa wanyonge.  Hali hii ya ukatili inawasukuma Diwani III  na Daktari Siki kwenda kwa Mstahiki Meya kuzungumza naye kuhusu hali mbaya ya wanacheneo. Aidha, Mstahiki Meya anawapuuza na kumsikiliza Bili ambaye anampotosha. Wafanyakazi wamechoka na wameamua kutorudi kazini. Usafiri nao pia umetatizwa kwa kuwa wafanyakazi wa bohari za mafuta nao pia wamegoma. Wanaosafisha mji pia nao wamegoma hali ambayo imesababisha mji kuwa mchafu zaidi na pia kuwa na harufu mbaya.

Hali inakuwa si nzuri jambo ambalo linawasukuma wawakilishi wa wafanyakazi kwenda kudai haki yao kwa Mstahiki Meya. Wawakilishi hawa ni Tatu, Medi na Beka. Meya kwa kupotoshwa na ushauri mbaya wa Bili, Diwani I na Diwani II anawapuuza. Hali ya mtafaruku inakumba Cheneo na kusababisha Makao makuu kutaka kujua kinachoendelea. Bili anapotambua kuwa hali si nzuri anaamua kuzima simu naye Mhazili wa Meya anagoma. Hali hii inaibua hisia kali Cheneo na hivyo makao makuu yanawatuma Askari kumkamata Mstahiki Meya. Uongozi mbaya na dhalimu wa Mstahiki Meya Sosi unakomeshwa hivyo.

### 4.2.4 Uathiriano katika Kiwango cha Msuko

Uathiriano katika msuko uliangaziwa kwa msingi wa vitushi na umantiki ambavyo ndivyo hufumwa kuunda matini za fasihi. Mtafiti alizingatia na kurejelea vitushi kwa lengo la kupata umantiki katika kazi zilizoteuliwa za kifasisihi. Jedwali lifuatalo linaangazia hali ya uathiriano uliopo katika kiwango cha msuko kwa kuangazia vitushi. Jedwali lifuatalo linatoa mkondo wa vitushi unaotawala kazi zote tatu za kifasihi:

| **Kazi zilizoteuliwa za kifasihi/Vitushi** | **Sihiri** | **Kuwepo kwa kiongozi dhalimu** | **Uwogawa kupote za uongo** | **Njama ya kumwua anaye -jali maslahi ya** | **Usaliti wa mtu wa karibu** | **Maangamizo** | **Ukombozi katika jamii** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Fumo Liyongo | Ndio | Ndio | Ndio | Ndio | Ndio | Ndio | La |
| Kifo kisimani | La | Ndio | Ndio | Ndio | Ndio | Ndio | Ndio |
| Mstahiki Meya | La | Ndio | Ndio | La | Ndio | La | Ndio |

*Jedwali 1: Mtiririko wa ploti katika tungo teule za kifasihi*

Jedwali 1 linaashiria jinsi kazi zilizoteuliwa jinsi ziliathiriana kimsuko. Tukio la kwanza katika kazi hii ni hali ya kuwepo kwa mhusika aliye na nguvu za kiajabu. Hali hii inajenga tukio la kwanza katika utungo wa Fumo Liyongo. Kama vile inavyodhihirika katika jedwali, tungo za tamthilia zilizoteuliwa zinaanzia katika tukio la pili ambalo ni hali ya

kuwepo na udhalimu kwa viongozi walio mamlakani. Hali hii inaleta uhalisia na kuondoa udhahania uliopo katika kazi ya awali ili kuafikia lengo la mwandishi la kuikosoa jamii ya kisasa. Katika kitushi cha tatu, hali ya woga wa watawala dhidi ya kupoteza nafasi zao za uongozi inajengwa. Kitushi hiki kinatawala tungo zote tatu kuashiria kiini cha mgogoro unaozuka katika kazi hizi. Ili kutatua tatizo hili, njama ya mauaji inapangwa ili kumwondoa mhusika anayekisiwa kuwa tisho kwa kiongozi anayetawala. Kitushi hiki kinatokea katika tungo mbili za kwanza ilhali katika tamthilia ya baadaye ambayo ni Mstahiki Meya inajiepusha na hatua hii kuashiria jinsi jamii inavyoendelea kukomaa kisiasa.

Wazo la usaliti linajenga tukio linalofuata kuashiria kuwa, jamii bado inaendelea kuthamini usaliti ili kuendeleza maovu katika jamii. Hali hii inatokea katika tungo zote tatu kuashiria kuwa ni uovu unaoendelezwa na jamii kutoka jadi. Usaliti unatumika kukuza mgogoro katika kilele. Baadaye, maangamizo yanatokea ili kuondoa tishio kwa viongozi walio mamlakani. Kazi ya baadaye inahepa mkondo huu wa kikatili jambo ambalo linaashiria kuwa jamii inaendelea kupiga hatua kidemokrasia. Mwishowe, ukombozi unapatikana baada ya juhudi za wanajamii kudai haki yao. Hali hii inapatikana katika kazi mbili za baadaye. Utungo wa kwanza unaashiria tofauti kwani kiongozi dhalimu bado anaendelea kutawala na hakuna hatua yoyote inayochukuliwa na jamii. Bila shaka, kwa kuangazia mtiririko wa vitushi, ni dhahiri kwamba tungo hizi tatu zinajalizana katika kuafikia lengo la mwandishi katika jamii. Ni wazi kuwa utungo wa *Kifo Kisimani* unajengwa na *Utendi wa Fumo Liyongo* nao unajenga kazi ya baadaye ambayo ni *Mstahiki Meya*.

Kwa kurejelea umantiki, ni dhahiri kwamba kazi ya *Kifo Kisimani* na *Mstahiki Meya* zimeathiriana katika kiwango cha msuko. Kama vile imejitokeza katika kazi ya iliyotangulia ya Fumo Liyongo, utendi unaanzia kwa kumchora mhusika aliye na nguvu za ajabu. Mhusika huyu anayeitwa Fumo Liyongo ndiye anayezua hali ya uwoga moyoni mwa mfalme Daudi Mringwari. Uwoga wa mfalme huyu ndio uaozua wivu dhidi ya Fumo Liyongo. Hali hii ya uoga inadhihirika miongoni mwa viongozi ambao mwandishi amewatumia kama viongozi katika kazi ya *Kifo Kisimani* ambaye ni Mtemi Bokono na Meya Sosi katika *Mstahiki Meya*.

Inabainika wazi kuwa, viongozi walio mamlakani ambao ni dhalimu hutumia nguvu walizo nazo ili kuwazima viongozi ambao ni tishio kwao hasa wanaoweka wazi mtendo yao ya kidhalimu. Aidha, baada ya kuwepo na viongozi dhalimu, kunao wale ambao wako tayari kupinga uongozi mbaya na kusimama na wale ambao wanadhalilishwa. Katika *Fumo Liyongo,* kijakazi Sada ndiye anayeenda kumwambia mamake Fumo jinsi anavyostahili kufanya kumnasua Fumo kutoka jela. Aidha, katika *Kifo Kisimani* na *Mstahiki Meya*,

mwandishi anachukua mkondo huo huo ili kuwachora wahusika ambao wako tayari kuelekeza hatua za ukombozi.

Katika misuko ya kazi zote tatu, mtindo sawa umetumiwa kukabiliana na wale ambao wanapinga uongozi wa walio mamlakani. Wanaopinga uongozi mbaya wanapangiwa njama ya kuondolewa ulimwenguni kama ilivyo katika *Fumo Liyongo* na *Kifo Kisimani.* Katika *Mstahiki Meya*, kwa kuwa inaashira hatua ambayo jamii imepiga kidemokrasia, mauaji hayakutokea lakini anayepinga anatolewa vitisho vikali zaidi.

Kuna usawa wa mandhari ambao unadhihirika katika kazi za kifasihi zilizoteuliwa. Katika *Fumo Liyongo* na *Kifo Kisimani*, kifo cha mhusika anayeonekana kuwa tisho kwa kiongozi kinatokea katika kisima. Hali hii ya utaratibu ambao umetumiwa katika kufuma kazi hizi mbili unaashiria uathiriano katika kiwango cha msuko. Katika *Mstahiki Meya*, suala la kisima limetokea ambapo tunatajiwa kuwa wafanyikazi katika bohari la mafuta wamegoma ili kupinga uongozi mbaya. Kwa kuwa jamii ya kiafrika inaedelea kukomaa kidemokrasia, mauaji hayatokei humu kisimani ila wafanyikazi wanaandamana kudai haki zao. Mauaji yanayotokea katika kitabu hiki cha *Mstahiki Meya* yalitokea kwa sababu ya kutelekezwa kwa wanajamii na uongozi. Wanatelekezwa kwa kukosa huduma za kimsingi kama vile chakula na matibabu hospitalini.

#### 4.2.5.1 Uthiriano katika Kiwango cha Uhusika

Katika jamii kila mwandishi ana lengo la kupitisha ujumbe kupitia kwa mhusika. Kwa mujibu wa kazi hii mtafiti alijikita katika wahusika wa uhalisia kwa kuwa wahusika waliopo ni wa kiuhalisia. Katika wahusika na uhusika wao, mtafiti aliangazia tabia ambapo ni sifa za ndani na za nje. Mtafiti alijikita katika usawiri wa majina ambapo tunapata mbinu ya kimajazi ikitumika. Kwa kutumia vigezo vya tabia na uhalisia, mtafiti aliweza kuwalinganisha wahusika kama ilivyojadiliwa katika sehemu hii.

Wahusika wanapatikana katika muktadha maalumu kwa mujibu wa Wamitila (2008). Muktadha huu si tu wa kijiografia, kijamii, kitamaduni au kisiasa bali pia ni muktadha wa kiisimu au kilugha. Wamitila anaendelea kufafanua uchambuzi wa historia na maendeleo ya fasihi unadhihirishwa kuwa wahusika wa kifasihi hubadilika kadiri wakati unavyoendelea. Wahusika wanaopatikana katika kazi za kifasihi za miaka ya zamani wanaotofautiana kwa kiasi kikubwa na wahusika wanaopatikana katika kazi za kifasihi za miaka ya baadaye.

Wamitila anamtambua mhusika wa kimwingilianomatini kuwa ni mhusika anayeitwa hivyo kwa kuwa anahusiana na mhusika anayepatikana katika matini iliyotangulia. Uhusiano

huweza kutokea kwa njia tofauti, majina, wasifu, mgogoro anaopambana nao mhusika, mazingira yake na dhima katika kazi za kifasihi.

Vigezo vilivyotumiwa kuainisha wahusika na uhusika wao ni:

a) Tabia-Katika kiwango hiki, mtafiti aliangazia wasifu wa mhusika. Ameangazia sifa za ndani za wahusika huku akiwalinganisha na kuwalinganua.
b) Mgogoro anaopambana nao mhusika- mtafiti amewajadili wahusika kwa kuzingatia kigezo cha migogoro waliopambana nayo. Hali hii ilimwezesha kutambua iwapo kuna hali ya kuathiriana katika uteuzi wa uhusika.
c) Mazingira/mandhari- mandhari yanayomzunguka mhusika yametathminiwa ili kuafikia uamuzi wa iwapo kazi hizi zinaathiriana au la.
d) Majina- majina ya wahusika yalitiliwa maanani kutambua iwapo kuna athari inayoibuka.
e) Dhima- katika kuhakiki uhusika wa kazi teule za kifasihi, nafasi ya wahusika katika kujenga maudhui na kielezo chao katika jamii kilizingatiwa.
f) Idadi- idadi wanayotumia watunzi wa kazi za fasihi huweza kushabihiana wazo ambalo linazua hali ya uathiriano.

Katika harakati za kusoma kazi hizi teule, hali ya uhusika ulibainisha uathiriano kama ifuatavyo:

**Fumo Liyongo kuwa Mwelusi (*Kifo Kisimani*)**

Mwelusi amepewa sifa za Fumo Liyongo na hasa kwa kurejelea mhimili wa uingiliano matini wa kurudufiwa kwa kazi za fasihi. Mwelusi amekuwa shujaa ambaye amejitolea kupingana na utawala mbaya wa Mtemi Bokono. Anatekeleza jukumu lake kwa kuhamasisha watu wa eneo la Butangi kujikomboa kutokana na uovu wa Mtemi Bokono. Hali hii inazua uhasama dhidi yake na viongozi wanaomuunga mkono Mtemi Bokono. Baadaye, mhusika mmoja anayeitwa Batu ambaye ndiye mshauri mkuu wa Mtemi Bokono anatumika kumkamata Mwelusi na kufungiwa jela.

Kwa upande mwingine, hali hii ndiyo iliyomkumba mhusika Liyongo katika kazi ya *Utendi wa Fumo Liyongo*. Liyongo anaonekana kuwa tisho kwa nduguye Daudi Mringwari aliyekuwa mfalme wa kisiwa cha Pate. Liyongo anaishi nyumbani kwake Ungwana wa Mashaha. Ujumbe wa Wagalla unafika Pate kumtembelea Sultan Daudi. Sultan huyo anamsifia Liyongo kwa Wagalla lakini wao hawaamini maneno yake. Anaamua kumpelekea Liyongo barua ya kumwita aje pate ili Wagalla wamwone. Liyongo, anapopata barua hiyo

anaanza safari ya kwenda Pate. Safari ya kwenda Pate ni mwendo wa siku nne lakini Liyongo anachukua siku mbili tu. Anapokaribia mji wa Pate anapuliza panda yake. Watu wanakusanyika kumwona. Anatua mzigo wake na kutoa vitu vya kutosha kujaza nyumba nzima. Wagalla wanakiri kuwa Liyongo ni mtu mwenye nguvu nyingi. Hali hii inazua wivu kutoka kwa Sultan wa Pate.

Kama ilivyo kwa mhusika Mwelusi katika *Kifo Kisimani*, Fumo Liyongo anapangiwa njama ili kutiwa mbaroni. Nduguye Mringwari anatumia askari. Sultan anaitisha ngoma ya gungu na mwao na kuwaalika mashaha wote wa ngoma, akiwemo Liyongo. Wakati wa ngoma hiyo askari wanamzunguka Liyongo na kumshika. Anatiwa gererzani. Baada ya kutiwa gerezani, inaamuliwa auawe. Sultan anapanga namna ya kumwua ili kumwondoa katika jamii kwa kuwa alimwona kama tishio la uongozi wake. Alimwona kuwa angeweza kumnyang'anya uongozi wake.

Katika Tamthilia ya *Kifo Kisimani*, mhusika Mwelusi naye baada ya kukamatwa Batu anapendekeza Mwelusi auawe kwa kudai aiondokee jamii. Wazo ili linatokana na mshauri mkuu wa Mtemi Bokono lakini linapngwa na mshauri Kame kama ifuatavvyo:
Wahusika hawa wanaishia kutoroka gerezani. Hali ya mwingilianomatini kwa njia ya uathiriano inajitokeza pia. Liyongo anatoroka kwa gerezani kwa njia ya kiajabu kwani alitumia kipawa chake kwa shaha kujiopoa. Alimtuma kijakazi Sada aende akamwambie mama yake amtengenezee mkate wa wishwa na kutia ndani yake tupa. Tupa hii angeitumia kukereketa minyororo aliyofungwa kwayo ili aweze kutoroka gerezani. Kijakazi Sada alifikisha ujumbe huu kwa mamake Liyongo ambaye alitengeneza mkate wa wishwa na kutia tupa ndani yake. Liyongo alitumia tupa hii kuweza kutoroka gerezani baada ya kukereketa minyororo aliyokuwa amefungwa nayo. Aidha, waliokuwa karibu na Liyongo hawakuelewa ule ujumbe wakati alipomtuma kijakazi Sada.

105. Kamba 'Sada akutuma,
Enda amwambie mama,
Afanye mkate mwema,
Kati tupa aitiya

106. Sada akabalighisha,
Mamake yakamuwasha,
Akaufanya wa wishwa,
Mate kampikiya.

111. Hata usiku kufika,

Matezo wakayadika,
Kana ada wakaweka
Tasa, pembe, siwa piya.

Katika tamthilia ya *Kifo Kisimani*, Mwelusi alitumia mbinu sawa na ya Liyongo jambo ambalo linaonyesha mwingilianomatini kwa njia ya uathiriano. Mwelusi anaweza kutoroka gerezani kwa kutumia tupa ambayo aliitumia kukereketa mnyororo aliyokuwa amefungwa nayo. Swali ni, tupa iliweza kufika gerezani vipi? Katika upekuzi wa maandishi ya tamthilia hii mtafiti aligundua kuwa mamake Mwelusi ambaye ni Tanya ndiye aliyemtengenezea mkate wa wishwa na ndani yake katia tupa. Aidha, alitengeza mikate tofauti lakini mmoja katia wishwa ili aweze kuwakanganya walinda gereza ambao walikuwa na mazoea ya kula chakula cha mfungwa. Walikula chakula cha mfungwa. Alitia tupa kwa mkate wa wishwa kwa kuwa mkate wa wishwa haupendezi na kwa hivyo wangetumia mikate mingine lakini mkate wa wishwa wakampa mfungwa.

Baada ya Mwelusi kupata mkate wa wishwa alichukua tupa iliyokuwa ndani na kutumia kukeketa minyororo aliyokuwa amefungwa nayo. Usiku Askari walipokuwa wamelala Mwelusi alikeketa minyororo na alipomaliza nao umati mkubwa ukaja na kuvunja lile lango kubwa la gereza na hivyo kumtorosha Mwelusi. Hali hii inaingiliana na vile Liyongo alivyotoroka kutoka gerezani hali ambayo ni mwingilianomatini kwa njia ya uathiriano.

**Tanya**: Watu walifanya vizuri kukufungua minyororo na kukufungulia.

**Mwelusi**: Walinifungulia. Hawakunifungua minyororo. Walipokuja nilikuwa nimeikata tayari. Mambo yalikuwa yamepangwa vyema. Atega aliniletea tupa ikiwa katika mkate wa wishwa. Aliwaletea askari tembo. Walipokuwa wakinywa tembo, tupa ilikuwa inatafuna minyororo.

**Tanya**: (*Akimwangalia Atega*) Asante, mwanangu. Sikujua kikapu ulichowapatia askari kilikuwa kimebeba maarifa na usalama kwa mwanangu. (*Kwa Mwelusi*) Karibu nyumbani, mwanangu. **UK. 82(*Kifo Kisimani*)**

Ili kufanikisha mbinu zao za kutaka kuwaua wahusika hawa, hali ya uathiriano katika kazi hizi mbili tofauti inadhihirika jambo ambalo linaashiria uingiliano matini. Nikianza na

mhusika Liyongo, njama ilipangwa na Sultan Mringwari kwa kushirikiana na Wasanye na Wadahalo. Mfalme anawashawishi Wasanye na Wadahalo wamuue Liyongo akiwa mwituni. Anaahidi kuwapa reale mia iwapo watamletea kichwa chake. Wasanye na Wadahalo wanafanya urafiki na Liyongo, halafu wanashauri wawe wakila pamoja kikowa. Chakula wanachokula ni makoma, ambayo wanapeana zamu za kuyaangua kutoka mtini. Zamu ya Liyongo inapofika, wanatarajia kwamba atapanda juu ya mkoma kuangua makoma, na wao watapata nafasi ya kumuua kwa mishale yao akiwa kule juu ya mti. Kwa bahati Liyongoanagundua hila yao na kuamua kuangua makoma kwa mishale yake kutoka chini. Hivyo hawafanikiwi kumuua.

45. Mfalme changaliya,
Mwituni mekimbiliya,
Wasanye kawazengeya,
Na Wadahalo pamoya.

46. Mfalme kawambiya,
'Liyongo kunipatiya,
Kitwa mukinieteya,
T' awapa riale miya.'

Mwishowe waliposhindwa waliamua kutumia mbinu tofauti na iliyotumiwa hapo awali. Wanatumia aksari sawa na wanavyotumiwa askari kumkamata mwelusi ili wamuue. Wasanye na Wadahalo wanakwenda kumweleza Liyongo kuwa mjini hakuna hatari tena, halafu waje naye mjini. Liyongo anawaamini na kurudi nao mjini pate. Baada ya siku chache Sultan anaitisha ngoma ya gungu na mwao ili waweze kupata nafasi ya kumkamata. Anakamatwa na kutiwa gerezani sawa hali inayomkabili mhusika Mwelusi.

119. Sulutani kawaitiya,
Askari kumzengeya,
Mwane liyongo sikiya,
Ili kumwandaliya.

Kumtia gerezani hawakufaulu kumwua kwa vile alitoroka kama vile imetajwa. Mbinu waliyotumia ni kumsihi mwanawe Liyongo akubali kumwua kwa kumuuliza siri yake ili aweze kumwua. Mwanawe alimbembeleza na bila kujua ila ya mwanawe anamwambia siri ya nguvu zake kuwa anaweza kufa iwapo atadungwa kwa kitovu kwa sindano. Mwanawe Liyongo aliaidiwa kumwoa bintiye mfalme iwapo angefaulu kumwua babake. Hali hii ndiyo inayompa msukumo wa kutekeleza unyama huo.

120. Wakamuona ndiyani,

Wakampeka asikhini,

Hata kwenyi Sultwani,

‘ Mwanae Liyongo akaya.

127. ‘Au wewe wakiyuwa,

Nambiya sifanye tuwa,

Uwaziri utapowa,

T’ akuoza bintiya’

Mwanawe Liyongo anakubali kumwua babake. Alikuwa ameahidwa uwaziri na pia kumpa bintiye. Liyongo anakubali kumwambia mwanawe siri. Kijana anarudi kwa Sultan na kumweleza alvyoambiwa. Sultan anafurahi, anampa sindano ya shaba na kumwambia arudi tena kwa baba yake akamuue. Kijana anarudi kwa baba yake na ndipo Liyongo alipogundua kwamba kijana huyu alikuwa katumwa na adui yake.

Kijana anarudi kwa Liyongo, anasubiri hadi baba yake anapolala usingizini, halafu anamchoma sindano ya shaba kitovuni. Liyongo anatoka usingizini kwa ghadhabu, anachukua upinde wake na kwenda kisimani, anapiga goti na kutia mshale katika upinde huku kauelekeza mjini na siku tatu wanaogopa kwenda kisimani kuteka maji. Mwisho wanamtuma mama yake aende akambembeleze aondoke pale ili wateke maji. Mama yake anakwenda hapo kisimani kila siku kumbembeleza kwa mashairi bila mafanikio. Mwishoni maiti ya Liyongo inaoza na kuanguka na ndipo watu wanapobaini kuwa yu marehemu.

Mfalme anapopata habari ya kifo chake anafurahi sana. Anamwita mtoto wa Liyongo na kumweleza habari ya kifo cha baba yake. Yule kijana badala ya kulia anacheka. Mfalme anakasirika na kumnyang’anya nguo na vitu vyote alivyompa, kisha anamfukuza mjini, anakimbilia porini kwa Wagalla na kufia huko.

213. Mfalme kabaini
“Kabisa huna imani
Epuka mwangu matoni
Na nyumbani nitokeya.

214. Usikuje mui wangu
Wewe adui ya Mungu

Tena vua nguo zangu
Vaa yako mazoweya.

Hali hii inaashiria mwingilianomatini. Hasa kwa njia ya uathiriano. Kazi ya pili ambayo ni *Kifo Kisimani* imeathiriwa kiuhusika hasa ikirejelewa vile mambo yanayomkumba Liyongo ni sawa na yanayomkumba mhusika Mwelusi katika Tamthilia hii. Mwelusi anasalitiwa na nduguye Gege ambaye anajifanya kuwa ana ujumbe maalum kwake. Mwanzo anamuuliza mama yao Tanya aliko Mwelusi kwani ameamua kumuunga mkono katika harakati za kupambana na Mtemi Bokono. Mamake Mwelusi kwa kutojua njama ya mwanawe Gege kwa Mwelusi anamwelezea mahali Mwelusi aliko.

Gege:Usiendelee kunikasirikia, Mama! Msimamo wangu kumhusu Mwelusi umebadilika. Nimegundua kwamba nakosea kutosikizana naye. Kutoka leo shida zake zitakuwa shida zangu. Sasa hamu yangu kuu ni kumwona na kumuomba msamaha. Nilidhani ningemkuta hapa.

Tanya: Ulijua vipi alikuja nyumbani?

Gege: Nilimwambia. Nataka sana kumwona ili kumwomba msamaha na pia kumpa pole kwa mkasa uliomkumba. Uk. 97(*Kifo Kisimani*)

Uathiriano zaidi wa kazi hizi unadhihirika wakati Gege anapoitwa katika ikulu kwa Mtemi Bokono kuelezewa vile akikubali kumwua Mwelusi jinsi atakavyozawadiwa. Hali hii inalinganishwa na ile ya mwanawe Liyongo ambaye aliitwa katika ikulu ili kuzawadiwa kwa kumwua babake. Aidha, uathiriano huu unajitokeza zaidi pale Gege anaahidiwa kuozwa bintiye Mtemi Bokono anayeitwa Alida sawa na Mwanawe Fumo Liyongo ambaye aliaihidiwa zawadi kama hiyo tu ya kuozwa bintiye Mfalme Mringwari. Aidha, anaahidiwa zawadi zingine kama vile jiana la heshima ‘MKUKI WA ALMASI’. Zaidi aliahidiwa kupewa mali nyingi kama vile n’gombe na ardhi.

Batu: Kulingana na kazi ambayo ameifanyia Butangi,anastahilijina, ‘Mwamba wa Butangi’ au ‘Mkuki wa Almasi’

Bokono: ‘Mkuki wa Almasi’ . Ameitetea Butangi kwa silaha. Kitendo chake na ‘Mkuki wa Almasi’ ni mambo yanayooana vizuri. Mwiteni.Uk.99(*Kifo Kisimani*)

Katika hali inayowakumba wahusika hawa wawili katika kifo inaashiria uathiriano wa kazi hizi jambo ambalo ni mwingilianomatini. Kama vile Liyongo alipofia kisimani, kifo cha Mwelusi kinatokea kisimani vile vile. Mwelusi anadaganywa na kakake waende chemba kwa kuwa ana ujumbe muhimu alioachiwa na marehemu baba yao ambao ameambiwa na mama na kwa hivyo waende chemba ili amwambie. Mahali walipoenda chemba ilikuwa ni kisimani ambapo alitekeleza mauaji hayo kwa kumchoma kisu tumboni.

Gege: (*Kwa Zigu*) La Zigu! Kisu chako hakitapata kazi. Naomba fursa nizungumze na ndugu yangu. Anatilia maanani sana kusikiza. Nikizungumza naye kisu chako hakitakuwa na kazi. (Kwa Mwelusi) Tafadhali Mwelusi!Nina ujumbe muhimu kwako. Twende chemba.

Mwelusi: Kazi ya umma kwanza. Kisha mazungumzo baina ya ndugu. Uk.95( *Kifo Kisimani*)

Kama vile imejitokeza, mandhari ya Mwelusi katika *Kifo Kisimani* yanashabihiana na yale ya Fumo Liyongo katika utendi. Kuna mandhari ya gereza ambayo yanaashiria mahali ambapo wahusika hawa wanakuja kufungwa na wanaotawala. Baadaye, kunatokea mandhari ya kisimani ambapo wahusika hawa wanapatana na mauti. Kama vile imejadiliwa, hali za wahusika hawa kitabia pia zinafanana. Ni wahusika wanaodhihirika kuwa wenye nguvu fulani zinazomtisha kiongozi anayetawala. Aidha, nguvu zao zinatofautiana kwa kuwa, Mwelusi ana nguvu za kimawazo au kiakili tu ilhali Fumo Liyongo amesawiriwa kuwa na nguvu za kimwili na kiakili.

Migogoro ambayo wahusika Mwelusi na Fumo wanayopambana nayo vilevile inashabihiana. Kama vingozi wanakumbana na hali ya kuchukiwa na viongozi walio mamlakani kwa kuwa wanaonekana kama tishio kwao. Wanapitia hali ngumu ya maisha kwani wanalazimika kujificha ili wasijulikane walipo ili kuhepa mauti. Mwishowe inadhihirika kuwa wanakuja kupatana na mauti baada ya kusalitiwa na jamaa zao wa karibu. Tofauti ni kwamba, Fumo anasalitiwa na mwanawe ilihali Mwelusi anasalitiwa na kakake.

Kwa kuzingatia dhima za wahusika hawa, Mwelusi na Fumo wana nafasi sawa katika jamii. Wanatumika kama vielelezo vya wanajamii ambao hujitolea mhanga kupigania haki za wanajamii wenzao. Wanawahimiza watu katika jamii kuendelea kupigania haki za jamii kwani huenda juhudi zao zikafua dafu kama ilivyo katika *Kifo Kisimani*. Aidha, wanatumika kuwakashifu viongzi wanaoendeleza udhalimu katika jamii kwa kuwaangamiza watu wanaotofautiana nao kimawazo. Watunzi wa tungo hizi wamewatumia wahusika hawa kujenga maudhui ya ukoloni mamboleo, ufisadi, uongozi mbaya na ukatili.

**Mwanawe Liyongo kama Gege (*Kifo Kisimani*)**

Hali ya uathiriano katika kiwango cha uhusika inadhihirika katika wahusika ambao wametajwa hapo juu. Gege anatumiwa na Mtemi Bokono kumwondoa Mwelusi ambaye alikuwa tisho kwa uongozi wa Mtemi Bkono. Hali hii inawiana kwani mwanawe Liyongo anahaidiwa kumwowa bintiye mfalme na akakubali kama alivyofanya Gege. Kwa kuwa ana tama ya kupata mali na umaarufu, anakubali kauli hiyo.

> Batu: Kulingana na kazi ambayo ameifanyia Butangi, anastahili jina, 'Mwamba wa Butangi' au 'Mkuki wa Almasi'
>
> Bokono: 'Mkuki wa Almasi'. Ameitetea Butangi kwa silaha. Kitendochake na 'Mkuki wa Almasi' ni mambo yanayooana vizuri. Mwiteni. Uk.99 (*Kifo Kisimani*)

Wahusika hawa ni dhahiri kuwa sifa zao wanaonekana kuwa wenye sifa sawa na nafasi zao zinawiana katika kila kazi. Hali hii ianadhihirika kama ifuatavyo:

Wenye tamaa- Gege na mwanawe Fumo Liyongo wanadhihirisha tamaa yao kwa vile wanavyojitokeza kuwaua jamaa zao ili kujinufaisha. Mwanawe Liyongo anakubali wito wa Mfalme Mringwari kwa tamaa ya umaarufu wa kumwowa bintiye mfalme. Hali hii ya tamaa ya umaarufu inadhihirika Gege anaitikia wito wa mshauri wa Mtemi Bokono kukubali kumwua kakake ambaye alikuwa tisho kwa uongozi wa Mtemi Bokono.

Wenye kusalitiwa- Kutokana na hali yao ya tamaa. Usaliti wao vile vile unaathiriana jambo ambalo linazua mwingilianomatini. Mwanawe Liyongo anasalitiwa kwa kukatazwa kuoa bintiye Mringwari kama anavyoahidiwa. Hali hii ndiyo inayomkumba Gege katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*. Gege ambaye alikuwa ameahidiwa kumwowa Alida aliye bintiye Mtemi Bokono. Aidha, Bokono anakataa kumwoza bintiye na kukana kwa kusema kuwa hapakuwa na ahadi kama hiyo.

> Gege: (Ambaye anaendelea kusimama bado) Na..
>
> Batu: Na nini?
>
> Gege: Lile jambo jingine. (Bokono anamwangilia Batu kwa mshangao Batu kwa mshangao)
>
> Batu: Jambogani?
>
> Gege: Zawadi yangu kuu.

**Batu**: Gani?

**Gege**: Ndoa yangu na Alida?

Uk.98 (*Kifo Kisimani*)

120. Wakamuona ndiyani,

Wakampeka asikhini,

Hata kwenyi Sultwani,

Mwanae Liyongo akaya.

127. 'Au wewe wakiyuwa,
Nambiya sifanye tuwa,

Uwaziri utapowa,

T' akuoza bintiya'

(*Utenzi wa Fumo Liyongo*)

Hawana utu- Gege na mwanawe Liyongo wanadhihirisha kukosa utu kwa kutekeleza kitendo cha kinyama dhidi ya watu wa jamaa zao. Unyama wa mwanawe Liyongo uanajitokeza anapomwua babake kwa kumchoma sindano ya shaba. Uhasama wa wa Gege unajitokeza anapomwua kakake Gege pasipo kujali hisia za mamake na dadake Andua.
Ni wauwaji- uuaji wao unadhihirika wakati Gege anamwua kakaye naye mwanawe Liyomgo alitekeleza mauaji ya babake

Wenye majuto- Ni dhahiri kuwa Gege anajuta kwa kuwa mwishowe baada ya kutekeleza mauaji ya Mwelusi hakuzawadiwa ndoa kati yake na Alida. Jambo hili linamhuzunishha kiwango cha kulia machozi. Mwanawe Liyongo naye hakufanikiwa kumwoa Alida kama alivyokuwa ameahidiwa badala yake alifukuzwa mjini.

Wahusika hawa wanadhihirisha uathiriano uliopo baina ya kazi hizi mbili ambazo watunzi wake ni tofauti jambo ambalo linaashiria mwingilianomatini. Mtafiti akiangazia nafasi zao katika kazi hizi, bila shaka hali ya uathiriano linajitokeza. Nafasi zao katika kazi hizi zinadhihirisha hali ya urudufu, yaani kurudufiwa kwa kazi hizi hali ambayo inaangaziwa katika moja ya mihimili ambayo nimetaja hapo juu. Migogoro wanayopambana nayo Gege na Mwanawe Fumo Liyongo inashabihiana. Kwanza wanatatizika kupata umaarufu na mali. Katika hali hii, nafasi ya kuwasaliti jamaa zao inapotokea wanaishambikia ili kukidhi tamaa

zao kama vile imejitokeza katika nukuu zilizotolewa. Wote wanaafikia lengo la kuwaua majamaa zao ili waweze kutuzwa. Katika kupata tuzo inasadifu kuwa zawadi waliyotayarajia zaidi ni nafasi ya kumwoa bintiye kiongozi. Katika hatua hiyo, viongozi wanaghairi nia na kukataa kuwapa zawadi hiyo. Katika *Fumo Liyongo*, mfalme anaamua kuchukua zawadi alizokuwa amempa mwanawe Liyongo kwa kuwa alifurahia kifo cha babake. Gege naye anafukuzwa kutoka ikulu na makachero waliomhadaa kuwa angemwoa bintiye mfalme. Mwishowe watu katika jamii wanawashambulia wahusika hawa kwa kuwasaliti jamaa zao. Bila shaka migogoro wanayopambana nayo mwanawe Fumo na Gege inashabihiana hali ambayo inaashiria uathiriano katika tungo hizi.

Wahusika hawa wana nafasi sawa katika kazi teule za fasihi. Wanatumiwa kujennga maudhui ya usaliti, tama na mauti kama vile imedhihirika hapo juu katika nukuu zilizotolewa. Wanatumiwa kukashifu ukatili miongoni mwa wanajamii. Aidha, wanawajenga wahusika wakuu ambao ni Fumo katika Utendi wa *Fumo Liyongo* na Mwelusi katika *Kifo Kisimani*. Kwa kuangazia tabia zao, wahusika hawa ni kielelezo cha watu katika jamii wanaopinga maendeleo kwa sababu ya ubinafsi wao. Gege na Mwanawe Fumo wana ubinafsi kwa kuwa wanajijali wao wenyewe na hawajali wanajamii wenzao kama vile imedhihirika katika nukuu zilizotolewa.

**Mamake Liyongo kama Tanya (*Kifo Kisimani*) na kama Mamake Dadavuo Kaole (*Mstahiki Meya*)**

Mamake Liyongo katika utendi anarudufiwa katika *Kifo Kisimani* kama mhusika Tanya ambaye ndiye mamake Mwelusi. Vilevile, anajitokeza katika tamthilia ya Mstahiki Meya kama mhusika mama Dadavuo Kaole. Mamake Liyongo anapitia wakati mgumu kumwokoa mwanawe kutoka hali ngumu anayopitia. Ndiye aliyetengeneza mkate wa wishwa na ndani yake akatia tupa ili mwanawe aweze kujiopoa kutoka kwa hali mbaya anayokumbana nayo. Anahuzunika zaidi baada ya mwanawe Fumo kuuawa kando ya kisima.

184. Kuwa Liyongo mekwima  
Uko nde ya kisima  
Sasa watu wamekoma  
Mai hawapati ndiya

185. Hapana ayapatayo  
Mtu mai atekao  
Kula mtu uko kwao  
Hapana wa kutokeya (Utendi wa Fumo Liyongo)

Kwa upande mwingine mhusika Tanya katika *Kifo Kisimani* anapitia hali ile iliyopitiwa na mhusika mtangulizi mamake Fumo Liyongo. Mama huyu anakiri kuwa hali yake si nzuri anapozungumza na Batu ambaye ni mshauri mkuu wa Mtemi Bokono.

**Batu**: Tanya, humwelewi Batu vizuri.

**Tanya**: Bila shaka simwelewi vizuri. Njiwa atamwelewaje vizuri kozi! (*Anaacha kufanya kazi na kumwelekea Batu*). Njiwa na kozi ni ndege wenye maisha tofauti. Tungalikuwa sote njiwa, au sote kozi, ningalikuelewa vyema zaidi. Tungalikuwa na mienendo sawa na tabia zinazolingana, ningalikuelewa vizuri zaidi.

**Batu**: Tanya, usemayo si kweli. Umekosea kabisa. Mimi si kozi. Na wewe si njiwa.

**Tanya**: (*Kama kwamba hukuyasikia maneno ya Batu*) Vifaranga vyangu viko taabani! Kimoja hakipo tena. Kimenyakuliwa na kozi. Mheshimu kozi! Ujasiri mwingi! Maisha katika kilele cha mbambakofi. **Uk.76 (*Kifo Kisimani*)**

Anayerejelewa kama kifaranga aliyepotea ni Mwelusi mwanawe Tanya. Hali iliyomkumba mamake Liyongo ndiyo iliyomkumba Tanya jambo ambalo linaashiria mshabaha mkubwa katika kazi hizi.

Mshabaha zaidi unajitokeza katika Mstahiki Meya ambapo kuna mhusika mamake Dadavuo Kaole ambaye alikuwa anapitia hali mbaya kwa sababu ya mwanawe aliyekuwa ameugua kwa kula chakula kibaya kilichotoka kwa Meya. Zaidi ya hayo, mama huyu yuko taabani kwa kuwa anahofia maisha ya mwanawe yatafika kikomo hali iliyowaafiki wahusika watangulizi. Hii ni kwa sababu zahanatini hamna matibabu kwa ukosefu wa dawa. Hali hii inatokea kimakusudi kwa kuwa Meya amekataa kuleta dawa hospitalini na badala yake anaishi kuwadaganya kuwa dawa zimo njiani.

**Waridi**: (*Kwa ukali*) Mbona hivi? Subiri huko nje mpaka uitwe!

**Mama**: (*Kwa unyonge.*)Tafadhali mwanangu, nihurumie.(*Akiashiria mtoto.*)Ni hiki tu. Sina chengine. (*Anawatazama huku machozi yanamtoka.*) Niokolee mwanangu **uk.3 (*Mstahiki Meya*)**

Kama vile imejitokeza katika nukuu zilizotolewa, tabia za wahusika hawa ni sawa. Wanajali maslahi ya jamii zao ndio maana wanajitolea kuhangaikia hali za wana wao. Mamake Fumo anamjali mwanawe ndio maana anatengeneza mkate wa wishwa na ndani yake kutia tupa ili aweze kumnasua mwanawe kutoka jela. Aidha, hali ni hiyo hiyo kwa

mamake Mwelusi ambaye anatia bidii zaidi kumwokoa mwanawe kutoka jela. Tofauti hapa ni kwamba, licha ya kuwa anamshughulikia mwanawe kwa kumpikia na kumpelekea chakula gerezani, si yeye aliyetia tupa ndani bali ni Atega aliyekuwa rafiki wa kike wa Mwelusi. Migogoro wanayopambana nayo kina mama hawa ni sawa hali ambayo inaashiria mwingiliano matini katika kiwango cha uhusika. Wanapitia hali ngumu ya kuwaokoa wanao kutoka kwa mauti. Mamake Fumo anajitahidi kumwokoa lakini hakufaulu. Hali sawa ndiyo anayopitia Tanya ambaye ni mamake Mwelusi katika *Kifo Kisimani*. Anamficha Mwelusi asijulikane aliko lakini mwishowe anaishia kupatwa na Gege aliyetekeleza mauaji yake. Hali zao zinasadifu hali yake mamake Dadavuo Kaole katika *Mstahiki Meya* anayepambana kumwokoa mwanawe kutoka kwa mauti ila tunaachwa katika hali ya taharuki kwa kuwa hatujui kama mwishowe alipona. Aidha, kwa kuangalia mandhari ya wahusika hawa, kuna hali ya kushabihiana inayojitokeza kati ya *Utendi wa Fumo Liyongo* na *Kifo Kisimani*. Akina mama hawa wanapewa mandhari ya mashambani ilhali katika *Mstahiki Meya* mazingira yake hayabainiki waziwazi iwapo zahanati iko mjini au mashambani.

**Batu (*Kifo Kisimani*) kuwa Bili (*Mstahiki Meya*)**

Mhusika Batu ndiye mshauri mkuu wa Mtemi Bokono. Washauri wengine ni Kame na Zigu. Wahusika hawa wanarudufiwa kinafasi, sifa na matendo katika *Mstahiki Meya* na Bili ambaye anamshirikisha mhubiri. Aidha, anamshauri Mtemi vibaya kwa kuwa anaunga mkono uongozi wa kuwanyanyasa na kuwangamiza wengine. Anapanga njama ya watu wa Batuitui waashambulia kabila la akina Azena. Batu anatekeleza haya ili wanabutangi waendelee kuunga mkono utawala wa Bokono. Mkewe Bokono anaelewa fika kuwa mumewe anadaganywa na washauri wabaya wanaompotosha na kwa hivyo atakuja kuingia mashakani lakini Bokono hakubali.

> Bokono: (*Kwa sauti thabiti*) Napendwa sana na watu. Uongozi wangu ungelikuwa mbaya, watu hawangelikuwa wakinipongeza katika kila pembe ya Butangi.
>
> Nyalwe: Unadanganywa. Unadanganywa na wanafiki unaowaita washauri…
>
> uk.15-16(*Kifo Kisimani*)

Katika *Mstahiki Meya*, mhusika Bili anashabihiana na Batu. Bili ambaye ni mshauri wa Meya hajali maslahi ya wanacheneo bali anajali maslahi yake binafsi. Kama Batu, anaunga mkono uongozi mbaya wa Meya ili aendelee kupata mali ya umma kutoka kwa Meya kwa njia ya kifisadi. Aidha, ni kiongozi mnafiki kama mwenzake mtangulizi kwa kuwa baada ya mambo kuharibika anazima simu na kutoweka. Anamshauri Meya auze fimbo ya

umeya ili wajipatie marupurupu halafu wadanganye kuwa imepotea. Vilevile, ndiye anaunganisha Meya na mhubiri mnafiki ili amwombee. Bili anamshauri Meya amsimamishe mwanakandarasi kazi ili aweze kumleta mwanakandarasi mwingine licha ya kuwa muda wake haukuwa umeisha na vilevile ilikuwa kinyume na kanuni. Kama mwenzake mtangulizi, anampotosha Meya kwa kumpa ushauri unaopotosha.

**Meya**: Bili je? Si mfanyikazi wa Baraza la mji!
**Diwani II**: Anaweza kulipwa kwa huduma za ushauri kwa Baraza.**UK27 (Mstahiki Meya)**

Kwa kuzingatia kigezo cha tabia, inabainika wazi kuwa wahusika hawa wanajali maslahi yao wenyewe. Wanawashauri viongozi vibaya ili waweze kufanikisha ndoto zao za kuendelea kunufaika kutoka na uongozi. Aidha, wanamwambia kiongozi kuwa anaongoza vizuri ilhali wanajua kuwa anaongoza vibaya. Ni viongozi ambao hawajali maslahi ya wanajamii bali wanajijali wao wenyewe.

Migogoro wanayopambana nayo pia inashabihiana. Wanamsifu kiongozi aliye mamlakani huku wakishikilia imani kuwa jamii haitazinduka. Mwishowe wanajipata pabaya baada ya jamii hiyo kuzinduka na utawala kuporomoka. Wahusika hawa wanatumiwa na mwandishi kujenga maudhui ya ushauri mbaya katika jamii. Aidha wanawajenga wahusika wakuu katika tungo zote mbili ambao ni Meya Sosi na Mtemi Bokono.

**ASKARI I, II na III (*Kifo Kismani*) *kuwa* DIWANI I, II na III (*Mstahiki Meya*)**

Mbinu ya utatu imetumiwa na waandishi hawa kwa njia inayozua hali ya uathiriano. Ni wazi kuwa kazi hizi zimeathiriana kwa kiwango kikubwa kupitia wahusika hawa watatu ambao wametajwa hapo juu. Uathiriano huu umezuka kwa kuwafumanisha wahusika ambao wanachukua sifa sawa za kimtindo.

Katika tamthilia ya *Kifo Kisimani*, mwandishi ametumia wahusika hawa watatu ambao ni Askari I, II na III. Askari II na III wanaochukua sifa sawa zinazokinzana na sifa za mhusika wa tatu ambaye ni Askari I. Mhusika Askari III anadhihirisha hali ya uadilifu na utu uzima ambao haupatikani katika wahusika wenzake katika kundi hilo. Hali hiyo ndiyo inajitokeza katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*. Katika tamthilia hii, Diwani I na II wanachukua sifa na tabia za Akari II na III. Diwani III anachukua sifa zinazokinzana na zile za wenzake kama Askari I.

Kundi la kwanza la Askari II na III wanajali maslahi yao wenyewe ndio maana wanakataa kumpa Mwelusi chakula anapoletewa na majamaa zake. Wanaendelea kuunga

mkono uongozi mbaya wa Mtemi Bokono. Wanatekeleza vitendo vya kikatili dhidi ya watu wa Butangi kama vile wanavyosimulia kisa cha mwanabutangi waliyemwua baada ya kutalii sehemu zake za siri. Askari I naye anapinga uongozi mbaya wa Mtemi Bokono licha ya kuwa anafanya hilo kwa busara. Anapigania haki ya mfungwa ambaye ni Mwelusi apewe chakula chake. Mwishowe anaungana na wanamapinduzi wa Butangi kumtoa Mtemi Bokono mamlakani.

Askari III: Kiko wapi chakula chake?
Askari I: Mikononi mwako!
Askari III: Kilicho mikononi mwangu ni haki ya tumbo langu.
Askari I: Nini, bwana wewe? Mfungwa hajakula tangu aingizwe humu.
Askari III: Kwa hivyo?
Askari I: Kwa hivyo tumpatie chakula chake. Uk.37 (*Kifo Kisimani*)
Askari II: Nilikuwa katika kikosi kingine. Na tulikuwa na kazi tofauti na hii tunayoifanya sasa.
Askari I: Nakusikiza.
Askari II: Kazi tofauti tofauti. Kwa mfano, kuminya habari kutoka kwa watuhumiwa(kimya kifupi). Siku moja tulimkamata mtuhumiwa. Baada ya kumhoji alikataa katakata kukiri makosa.
Askari I: Makosa gani?
Askari II: Kutumiwa na majirani ili kuleta kimbuga katika Butangi.
Askari I: Mlifanya nini…
Askari II: Nilibadilika kuwa mkisi! Majani yaliyokuwailichukua gogo la mwangati. Punde karibu yalipata rangi mpya. UK.41 (*Kifo Kisimani*)

Katika Mstahiki Meya, hali ni hiyo hiyo ambayo inaashiria mwingilianomatini kwa mujibu wa wahusika hawa. Diwani I na II wanakubaliana katika kauli ya kuendela kuwanyanyasa wanajamii Cheneo. Wanaunga mkono uongozi mbaya wa Meya Sosi ili waendelee kunufaika. Wanadai nyongeza ya mishahara na marupurupu mengine ilhali wafanyakazi wengine huko Cheneo hawalipwi mishahara kwa wakati na wanapolipwa mishahara yenyewe ni duni na hulipwa nusu. Hawatozwi kodi ilhali wameidhinisha mama muuza ndizi kutozwa kodi. Wanakiri kwamba wamechaguliwa wajifae wenyewe hali ambayo inaashiria ubinafsi kama wenzao katika utungo wa *Kifo Kisimani*. Kinyume na tabia zao, ni Diwani III ambaye ana utu na anatumia nafasi yake kama diwani kumshauri meya ila hasikilizi ushauri wake. Anapinga wazo la nyongeza ya mishahara kwa madiwani lakini kauli yake inatupiliwa mbali.

**Meya**: Nashukuru ndugu zangu. Hapa nilipo sina hata soda. Kama lipo jambo ninaloweza kuwafanyia msisite kuniambia.

**Diwani I**: Labda marupurupu kidogo Mstahiki Meya.

**Diwani II**: *Overtime* labda. Uk.60(*Mstahiki Meya*)

Kwa kuangazia kigezo cha migogoro wanayopambana nayo, ni dhahiri kuwa Askari II na III pamoja na Diwani I na II wanajaribu wawezavyo kudumisha utawala ulio mamlakani lakini juhudi zao zinafeli na wanakosa kuafaulu. Mwishowe wanaathirika vibaya uongozi wa Meya unapoporomoka. Aidha, Askari I na Diwani III wanapambana na hali ya utawala mbaya wakiwa ndani ya utawala wenyewe na mwishowe juhudi zao zinafanikiwa na utawala mbaya unapoporomoka. Mandhari ya wahusika hawa ni tofauti kwa kuwa askari wanapatikana gerezani ilhali madiwani ni katika ofisi ya Meya Sosi. Kwa kurejelea tabia zao, ni dhahiri kuwa kundi hili la wahusika ni wenye ubinafsi wanaojali maslahi yao kama vile imejitokeza. Aidha, kuna mshabaha zaidi kwa kuangazia kigezo cha dhima yao katika tungo hizi. Wanatumiwa na mwandishi kuwajenga wahusika wakuu katika kila tungo. Waandishi wanawatumia kukashifu ubinafsi miongoni mwa watu katika jamii.

**Atega**: Baraza litaundwa upya. (Kwa Bokono, Batu, Mweke na Gege) Samahani! Nilisahau kuwapasha ujumbe. Zingu na Talui walituambia tuwasalimie.

**Batu**: Wako wapi?

**Kame**: Wanawasubiri.

**Bokono**: Wapi?

**Askari I**: Wapi? Gerezani bila shaka. Uk.105(*Kifo Kisimani*)

**Askari II**: (*Kwa udhabiti.)* Ndugu Meya, tumetumwa na makao makuu kuwachukua mwende kuelezea mbele hali hii ya mambo.

**Meya**: (*Anabadilika ghafla.*) Yote haya ametiwa chumvi na wanahabari. Si kweli wanavyodai. (Askari wanaanza kuwakaribia)

**Askari I**: Si neno. Utawaelezea hayo waliotuma huko mbele. Uk.79(*Mstahiki Meya*)

**Daudi Mringwari (*Fumo Liyongo*) kuwa Mtemi Bokono (*Kifo Kisimani*) na Mstahiki Meya Sosi (*Mstahiki Meya*)**

Katika Utendi wa *Fumo Liyongo*, mhusika Mfalme Daudi Mringwari anamjenga mhusika Mtemi Bokono katika *Kifo Kisimani*. Mtemi Bokono naye anasawiriwa katika

mhusika Meya Sosi katika *Mstahiki Meya*. Wahusika hawa wanadhihirisha hali ya uathiriano katika tabia, migogoro wanayopambana nayo, mandhari na dhima yao katika kazi za kifasihi zilizoteuliwa. Wahusika hawa wote ni viongozi katika kazi wanazotumika. Katika *Utendi wa Fumo Liyongo*, Daudi Mringwari ni kiongozi katika kisiwa cha Pate huko Mombasa. Katika *Kifo Kisimani*, Mtemi Bokono ni kiongozi katika eneo la Butangi naye Meya Sosi ndiye meya katika eneo la Cheneo kama inavyodhihirika katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*.

8. Walienda Wagala
   Kwa jumbe wa Pate dola
   Kwa kununua chakula
   Pamoya kumwangaliya

9. Wagala hao yuwani
   Ni wakuu wa mwituni
   Kabila ya sulutwani

10. Sulutwani Pate Bwana
    Papo naye kanena
    Wagala mumemuona
    Liyongo kiwatokeya? **(Utendi wa Fumo Liyongo)**

Zaidi ya wahusika hawa kuwa viongozi, majina yao ni ya kimajazi. Daudi ni jina ambalo linatoka katika Biblia kurejelea Myaudi mmoja aliyefanikiwa kuliua jitu la jamii ya Wafilisti lililoitwa Goliathi lililokuwa linawahangaisha wana wa Israeli. Daudi alifanikiwa kuliua kwa kutumia jiwe moja tu.

Jina Mtemi Bokono nalo ni la kimajazi. Mtemi inamaanisha mhusika aliyetwikwa jukumu la kuongoza watu katika jamii hasa katika jamii zilizotumia hali ya ujamaa kama njia ya kuongoza. Nalo jina Bokono ni jina linalotumika mitaani kumaanisha vitu ambavyo ni feki. Hali hii inadhihirika katika uongozi wa wa Mtemi Bokono ambapo tunagundua kwamba mhusika huyu ni kiongozi aliye feki kwa kuwa anaamini sifa za uongo kuwa anapendwa na Wanabutangi ilhali hapendwi. Aidha, inadhihirika kuwa Mtemi Bokono sawa na jina lake, ni kiongozi asiyeelewa wajibu wake kama kiongozi katika jamii.

**Nyalwe**: Unadanganywa. Unadaganywa na wanafiki unaowaita washauri waaminifu.
**Bokono**: (*Akimnyoshea kidole*) Usitukane macho na masikio yangu!
**Nyalwe**: Unadaganywa!

**Bokono**: (*Sauti kali)* Sidanganywi! **Uk. 15(*Kifo Kisimani*)**

Hali sawa inajitokeza katika Mstahiki Meya ambapo mhusika Meya Sosi amepewa jina la kimajazi. Sosi ni chakula katika jamii ambacho hupendwa sana na watoto. Sawa na jina lake, Meya Sosi anapenda kula sana. Anaandaliwa meza iliyo na vyakula vya aina mbalimbali ilhali bado analalamika kuwa, viyai alivyopewa ni vidogo. Sawa na jina lake, Meya Sosi anatumia nafasi yake kama meya kujinufaisha. Ananyakua ardhi ya umma, kujiwekea *entertainment vote* na kuagiza nyongeza ya mishahara kwa wandani wake ambao ni madiwani. Hali hii inaashiria kuwa jina lake kama mhusika ni la kimajazi. Kama inavyodhihirika katika kazi zote tatu, inadhihirika kwamba wahusika Daudi Mringwari, Mtemi Bokono na Meya Sosi wanapewa majina ya kimajazi ambayo yanajenga sifa na tabia zao zinazolingana kwa kiwango fulani hali ambayo inaashiria urudufiano.

**Meya**: (Akijisemea mwenyewe huku akila na kunywa.) Viyai vidogo…

**Dida**: Mwenye kuayaleta Mstahiki Meya anasema hali zimebadilika. Kuku wanataga madogo hivi. **Uk.8-9(*Mstahiki Meya*)**

Kwa kurejelea tabia zao, inadhihirika kuwa wahusika hawa wana sifa sawa kama viongozi walio dhalimu. Wahusika hawa wanakiuka haki za kibinadamu katika uongozi wao. Wana woga wa kupoteza uongozi wao kama viongozi katika maeneo wanayotawala. Hali hii inadhihirika wazi katika *Utendi wa Fumo Liyongo* ambapo Mfame Mringwari anapanga njama ya kumwangamiza Fumo kwa kuwa alimwona kama tishio kwa uongzi wake. Mwenzake Mtemi Bokono katika *Kifo Kisimani* naye anajengwa kwa sifa za Daudi Mringwari. Mtemi Bokono anawatumia washauri wake kupanga namna ya kumwangamiza Mwelusi aliyeonekana kuwa tishio kwake kwa kuwazindua Wanabutangi dhidi ya uongozi mbaya. Katika Mstahiki Meya, Meya Sosi anadhihirisha udhalimu kama kiongozi licha ya kuwa hakufikia hatua ya mauaji kama wenzake watangulizi. Anamtishia hasidi wake wa uongozi Siki dhidi ya kurudi kwake tena kwa madai ya kuukosoa uongozi wake. Aidha, wahusika wote ni fisadi kwa kuwa wanatumia mamlaka waliyonayo vibaya ili wajinufaishe.

19. Tumi kenda kwa haraka
    Kwa Liyongo akafika
    Kampa kaumunika
    Akasoma yote piya

20. Na liyongo akajibu
    Kwa hishima na adabu

Nitakuja kwa karibu
Nitwiiye Maulaya (*Utendi wa Fumo Liyongo*)

**Zigu**: (*Baada ya kimya kifupi*) Napendekeza mfungwa afe kutokana na ugonjwa wa moyo gerezani. Huenda watu watanung' unika hapa na pale. Kisha watanyamaza… (uk.61) ***Kifo Kisimani***

**Meya**: Hakikisha mtu huyo halikaribii lango kuu kuanzia sasa. Jengo langu alione paa. *Alright?*
**Gedi**: *yes sir.* Uk.15***(Mstahiki Meya)***

Migogoro wanayopambana nayo Mfalme Daudi, Mtemi Bokono na Meya Sosi ni sawa. Viongozi hawa wanahangaika kihisia dhidi ya kudumisha uongozi wao. Ili kufanikiwa katika wazo hili, wanapanga namna ya kupambana na mahasidi wao wa kisiasa. Mwishowe, wanafanikiwa kuwaondoa mahasidi hao hasa katika kazi za kwanza mbili tangulizi. Mtemi Bokono na Meya Sosi juhudi zao za kudumu mamlakani zinaondolewa na hivyo kupoteza nyadhifa zao. Aidha, katika Utendi wa Fumo Liyongo, hali yake inabadilka kwa kuwa msomi anaachwa katika hali ya taharuki kwa kuwa hatujui kilichomfanyikia mhusika huyo kama kisasi cha jamii kwa kumwua Fumo Liyongo.

Wahusika hawa wana mandhari sawa katika tungo wanazotumika hali ambayo inaashiria uigaji. Mazingira ya wahusika hawa ni katika makao ya utawala. Katika *Utendi wa Fumo Liyongo*, mandhari ya Daudi Mringwari ni katika makao ya utawala wa kiongozi wa pate. Ni katika makao haya anapomtumana mwanawe Fumo aje ili waweze kumshawishi atekeleze mauaji Fumo. Katika tamthilia ya *Kifo Kisimani*, mazingira ya Mtemi Bokoni ni katika ukumbi wa utawala. Ni katika mazingira haya ambapo Gege naye anashawishiwa kutekeleza mauaji ya Mwelusi. Katika tamthilia ya Mstahiki Meya, mandhari ya Meya Sosi hasa ni katika majengo ya ofisi ya utawala na pia utofauti unaingia kwa kuwa ana mandhari zaidi ambayo ni nyumbani kwake na pia katika sehemu za burudani kama vile hoteli ya Modern Resort. Kwa wahusika wote watatu, inadhihirika kuwa majengo ya utawala ni mazingira yao hali ambayo inaashiria ujalizano katika uhusika na wahusika

179. Kayuwa hana fahamu
Naye ulele kwa tani
Achamka hamuoni
Kiyana amekimbiya

180. Babake akishutuka
Chembe uta akashika
Kwa haraka akatoka
Nde mui kayendeya (*Utendi wa Fumo Liyongo*)

**Gege**: Kazi ya mikono yangu yenyewe! Nimeuchomoa mwiba tayari…

**Bokono**: Butangi inahitaji wazalendo wadhabiti kama wewe… uk.98(*Kifo Kisimani*)

Wahusika hawa wanatumiwa na mwandishi kama kielelezo cha viongozi dhalimu katika jamii. Wanawajenga wahusika wenzao katika tungo wanazotumika. Daaudi anamjenga mhusika Fumo katika *Utendi wa Fumo Liyongo*, Mtemi Bokono anamjenga mhusika Mwelusi katika *Kifo Kisimani* naye Meya Sosi anamjenga mhusika Siki katika utendi wa *Mstahiki Meya*. Hivyo basi, ni dhahiri kuwa kuna hali ya uathiriano wa kiuhusika kwa kurejelea tungo hizi tatu kama inavyodhihirika katika usawiri wa wahusika hawa katika sifa, migogoro wanyopambana nayo, tabia, majina na mandhari yao.

### 4.2.5.2 Wasifu wa Wahusika

Mwelusi katika *Kifo Kisimani* ana sifa sawa na Fumo Liyongo. Hali hiyo pia inadhihirika katika Mstahiki Meya kupitia mhusika Siki. Wahusika hawa ni wenye msimamo dhabiti. Wanakataa uongozi mbaya unaoendelezwa na viongozi walio mamlakani na kupigania haki za wanyonge. Fumo Liyongo anachukua nafasi yake kama malenga na kuwatumbuiza wenyeji wake wanaokuja kumwangalia gerezani. Aliipigania jamii yake dhidi ya maovu ndio maana wanamshabikia kwa uhodari wake. Aliwapigania wakati walipovamiwa na mahasidi wao. Aidha, Mwelusi katika Kifo Kisimani anapinga njama za kuwadhalilisha wana Butangi kupitia kwa uongozi mbaya wa Mtemi Bokono. Anaendelea na msimamo huo licha ya dhuluma anazopata kwa kufungiwa gerezani na hata kupigwa. Hali hiyo inadhihirika kwa mhusika Siki ambaye ni binamuye Meya Sosi lakini haungi mkono uongozi mbaya. Anamwambia Meya Sosi ukweli licha ya kuwa hataki kumsikiliza na baadaye anamwamrisha aione nyumba yake paa.

Ni dhahiri kuwa mhusika mwanawe Fumo Liyongo anatumika kama kielelezo cha watu wanaowasaliti jamaa zao katika jamii. Jambo hili ni kweli kwa kuwa alimwua babake Liyongo ili aweze kutekeleza matakwa ya Mfalme Mringwari.

Nafasi ya mwanawe Fumo Liyongo inarudufiwa katika kazi ya *Kifo Kisimani* ambapo mhusika Gege anachukua nafasi hiyo hiyo tu kwani naye anamsaliti kakake Mwelusi ambaye alimwua jambo ambalo linaashiria mwingilianomatini kwa njia ya undumakuwili.

Mwanawe Liyongo anatumika kama kielelezo cha jamaa wenye tamaa inayowaongoza kutekeleza unyama unaokiuka utu. Hali hii inarudufiwa katika *Kifo Kisimani* kupita mhusika Gege jambo ambalo linaashiria mwingilianomatini katika uhusika katika kiwango cha nafasi. Gege anadhihirisha kukosa hisia kwa nduguye Mwelusi na kutekeleza mauaji yake. Jambo hili linamuudhi mama yao zaidi na watu wa Butangi kwa jumla. Kwa mwanawe Liyongo kumwua babake hali hiyo ilizua huzuni nyingi kwa jamaa zake na hasa mamake Liyongo.

Kijakazi Sada katika Utendi wa *Fumo Liyongo* ana nafasi sawa na Andua katika Kifo Kisimani. Sada anatumika kama kielelezo cha wafanyakazi wanaojitahidi kuendeleza utu katika jamii kwa kumjali mfungwa na pia kuficha siri ya kuingizwa kwa tupa gerezani. Nafasi hii inachukuliwa na mhusika Andua ambaye alivumilia mateso kwa kupigwa na Askari kila anapomletea mfungwa chakula. Aidha, hali hii inaleta mshabaha mkubwa kinafasi za wahusika.

Mhusika Mfalme Mringwari anachukua nafasi sawa na mhusika Mtemi Bokono na Mhusika Mstahiki Meya. Ni vielelezo vya viongozi wabaya wanaochukua nafasi zao katika uongozi kuwanyanyasa watu wanaowaongoza. Mfalme Mringwari anapanga jinsi ya utekeleza mauaji ya Fumo Liyongo kwa kuwa alimwona kama tisho la uongozi wake. Vilevile Mtemi Nasaba Bora alichukua nafasi yake kutekeleza uovu wa kutekeleza mauaji ya Mwelusi kwa kuwa alimwona kama tisho. Mstahiki Meya anatekeleza maauji ya Wanacheneo kwa kutokuwa mwajibikaji katika kazi yake hasa kwa kuleta dawa za wagonjwa hospitalini.

Mwanawe Fumo Liyongo pia ana nafasi sawa na Gege. Wanachukua nafasi za kuwa vielelezo vya watu wanaowasaliti jamaa zao kwa sababu ya tamaa ya mali. Gege anachukua jukumu la kumwua kakake ili aweze kupata umaarufu na mali. Nafasi hii ni sawa na mhusika Mwanawe Fumo Liyongo anayemwua Babake ili aweze kuwa maarufu na huku akiwasaliti wanacheneo ili ajinufaishe kutokana na uongozi wa Mstahiki Meya. Anamshauri meya vibaya badala ya kumwambia ukweli wa jinsi mambo yalivyo.

Bili ana nafasi inayoshabihiana na nafasi ya Batu katika *Kifo Kisimani*. Mhusika Bili anachukua nafasi sawa na mwenzake mtangulizi kwa kuwa aliweza kumpa Mstahiki ushauri mbaya kama vile wanaotumia nafasi zao kuwapotosha wenzao katika kuwashauri. Vilevile ni wahusika wanaochukua nafasi zao kuwapotosha wengine ili wajinufaishe wao wenyewe.

Vilevile, wahusika hawa wanachukua nafasi za watu wanaowazunguka viongozi ili wajinufaishe wao wenyewe.

Mamake Fumo anachukua nafasi sawa na mhusika Tanya ambaye ni mamake Mwelusi. Mamake akina mama hawa wanajali maslahi ya wanao na ndio maana wanachukua jukumu la kuwanasua wanao kutoka gerezani. Ni wavumilivu kwani wanavumilia hali ngumu ambazo wanao wanazipitia. Aidha, mwandishi wa Mstahiki Meya ana mhusika Mama Dada Vuo Kaole ambaye anafanya kila awezalo ili kumnasua mwanawe kutoka kwa mauti. Aidha anavumilia hali ngumu ya maisha wanayopitia ya kukosa chakula na pia matibabu zahanatini.

#### 4.2.5.3 Ulinganishaji wa Wahusika kwa kurejelea Idadi

Kwa kurejelea idadi, kuna hali ya mwingiliano baina ya *Kifo Kisimani* na *MstahikiMeya*. Katika Kifo Kisimani, mwandishi wa Kifo Kisimani ana Askari watatu na makachero watatu. Kazi ya Mstahiki Meya mwandishi ana Madiwani watatu ambao ni Diwani wa Kwanza, Diwani wa Pili na Diwani wa Tatu.

Katika kifo Kisimani, Askari mmoja ambaye ni Askari wa kwanza ndiye ana msimamo tofauti na wengine kwa kuwa haungi mkono uongozi mbaya wa Mtemi. Katika Mstahiki Meya, Diwani wa Tatu Bwana Kheri ndiye vile vile ana msimamo tofauti na wenzake kwa kuwa haungi mkono uongozi mbaya wa Meya. Kwa kurejelea idadi, waandishi wote wawili wana ulinganisho kwa kuwa wanakuwa na wahusika wawili ambao wanaunga mkono na mmoja anayepinga. Hali hii ya mgao wa wahusika inaashiria mwingilianomatini katika kiwango cha uhusika. Aidha, hali hhii ya mgao wa wahusika haidhihiriki katika Utendi wa Fumo Liyono.

Wahusika hubeba maudhui ya mtunzi ambayo huendeleza dhamira ya mtunzi. Hivyo basi, wahusika husukuma ajenda kuu ya mtunzi katika kazi yake. Katika matini hizi tofauti, matini tofauti ambazo ni tatu zimetumia wahusika ambao wanadhihirisha ujalizano na uathiriano wa kazi tofauti. Kama vile imejitokeza wahusika tofauti katika matini zenye kipindi tofauti cha kihistoria huweza kuchukua nafasi sawa katika uwasilishaji wa maudhui katika matini.

### 4.3 Mwingiliano wa Kimaudhui

Katika sehemu hii mtafiti amehakiki maudhui kama kipengele cha kimwingilianomatini. Maudhui ni mawazo mbalimbali ambayo yanaibuka katika kazi ya fasihi na dhamira ni swala kuu linalojitokeza katika kazi ya fasihi kuanzia mwanzo hadi mwisho wa kazi hiyo. Hujengwa na kuathiri vipengele vingine vyote vya kazi husika maksudi ili kujenga dhamira. Kwa mujibu wa Wamitila (2003), Julia Kristeva anasisitiza

kuwa, hamna matini yoyote ya kifasihi ambayo inaweza kuangaliwa kivyake. Kazi za kifasihi huingiliana na kuchangizana katika kipengele kimoja au zaidi. Waandishi wa fasihi wanapoandika kazi zao, hawana budi kuwa na mshabaha katika maswala wanayozungumzia. Hii ni kwa sababu fasihi ni zao la jamii na wote huchota ni malighafi yao kutokana na jamii. Isitoshe, binadamu wote ulimwenguni hughasiwa na maswala yanayofanana. Kwa sababu hii, si ajabu kupata waandishi waliokua katika mazingira mbalimbali wakiandika mambo yayo hayo kwa njia zinazolandana.

Kwa mujibu wa Wamitla, Bakhtin (1990) anasema kuwa semi zote kimaumbile ni za kisemezano. Kwa mujibu wa maoni ya mwananadharia huyu, tumehakiki jinsi tamthilia hizi zinavyoingiliana kimaudhui. Waandishi Mberia na Arege wameangazia mambo mengi kama vile, ufisadi, uongozi mbaya, migogoro, ukatili na kadhalika.

Wamitila (2008) anaelezea kuwa maudhui katika kazi ya kifasihi hayawezi kumfikia msomaji bila ya kuwepo na nyenzo za kuyapitisha au kuyawasilisha. Uhusiano uliopo basi kati ya maudhui ni wa kutegemeana bila fani na maudhui hayapo; na maudhui nayo hayawezi kuwasilisha bila ya kuwepo kwa fani. Mawazo ya Wamitila ndiyo yalimpa mtafiti vigezo mwafaka vya kuhakiki kazi teule za kifasihi. Mtafiti alitumia vigezo vifuatavyo katika kuhakiki maudhui huku akiongozwa na mihimili ya uigaji na urudufiano:

a) Dhamira
b) Ujumbe
c) Mtazamo na msimamo

### 4.3.1 Mwingiliano wa Kimaudhui kwa kurejelea Dhamira

Kwa kurejelea dhamira, hali ya uathiriano na uigaji ulijitokeza baina ya kazi teule za kifasihi. Wamitila(2008) anaelezea kuwa, dhamira ni jumla ya mambo yanayojadiliwa katika kazi za fasihi. Anaendelea kuelezea dhamira za kazi za fasihi hujitokeza kulingana na matukio ya jamii. Kwa kuangazia utendi wa *Fumo Liyongo*, unadhamiria kukashifu uongozi mbaya na kukusudia kuijenga jamii mpya isiyo na matabaka. Haya yanafanikishwa kwa kuweka wazi hali ya mhusika Fumo ambaye alikuwa rasilmali kwa jamii yao lakini kwa sababu ya uongozi mbaya anpangiwa njama na kuuliwa. Katika jamii yao kuna matabaka ya watawala na watawaliwa ndio maana Mfalme Mringwari anapanga jinsi atakavyojidumisha mamlakani kwa kumwondoa Fumo ulimwenguni.

Mtunzi wa *Kifo Kisimani* anakuza dhamira iliyopo katika *Utendi wa Fumo Liyongo*. Hali hii inadhihirika kwa mshabaha uliopo katika matukio yanayowazunguka wahusika wa matini hizi. Mberia anaazimia kukashifu uongozi mbaya kupitia kwa mhusika Mtemi Bokono

anayeongoza Butangi kwa kidhalimu hali inavyojitokeza katika matini tangulizi. Aidha, analenga kujenga jamii mpya isiyo na matabaka. Anafanikisha lengo lake kupitia wahusika Askari I, Atega, Andua na Mwelusi ambao wako katika matabaka tofauti ya kielimu, kijinsia na kitaaluma ila wanaungana ili kupigania ukombozi katika Butangi. Wahusika hawa wanaamua kwenda kuteka maji katika kisima cha Mkomani ambacho kilikuwa kimetegewa Mtemi Bokono ili kupinga hali ya utabaka na kusawazisha wanajamii wote. Mberia vilevile anapinga hatua zaidi ya matini tangulizi kwa kuonyesha kuwa kuna mafanikio katika juhudi za kutafuta haki. Hali hii inawezekana wakati Bokono anaondolewa mamlakani kama Mtemi wa Butangi na kupelekwa gerezani. Aidha, kazi hii inadhamiria kustawisha demokrasia kwa kubeza ukoloni mamboleo unaoendelezwa na viongozi wa Kiafrika.

> **Atega**: Tumekuja kwa amani kukata kiu kwa kwa maji ya kisima cha Mkomani.
> **Zigu**: Mkitaka kukata kiu nendeni mbele. Nendeni hadi bwawa la Sulu.
> Uk. 93 *Kifo Kisimani*

Arege naye kwa kiwango fulani anachukua mkondo sawa wa dhamira kwa kuwa anasawiri namna uongozi mbaya unavyoendelzwa katika jamii kupitia mhusika Meya Sosi. Meya Sosi anaendeleza uongozi mbaya kama meya wa Cheneo. Jamii inakosa huduma za kimsingi kama vile matibabu na elimu bora ilhali yeye anazipata katika nchi za ng'ambo. Wanawe meya wanasomea ng'ambo na pia bibiye Meya anapojifungua anasafiri ng'ambo kwa kuwa huko ndiko kwenye huduma bora. Aidha, kama ilivyo katika matini tangulizi, tamthilia ya *Mstahiki Meya* inalenga kuonyesha namna jamii mpya isiyo na matabaka inavyoweza kujengwa kwa kuweka wazi athari za kimatabaka. Matini hii inatofautina kidhamira zaidi kwa kuweka wazi mchango wa dini katika ujenzi wa jamii mpya jambo ambalo halizamiwi kwa undani katika matini tangulizi. Anaafikia lengo ili kupitia kwa mhusika mhubiri anayekosa kumkosoa Meya ili aendelee kunufaika kwani anapewa sadaka nono anapokuja kuliombea baraza.

> **Bili**: (Kwa bashasha.) Maraile ya mwisho tulipokuwa pamoja alionekana amechoka sana!
> **Meya**: Ndiyo maana alisafiri ng' ambo. Madaktari wetu hawa wa kubabaisha tu. Kule ng' ambo ndipo walipo wakunga wenyewe. Sikutaka…
> Uk. 27 (*Mstahiki Meya*)
> **Meya**: Ninajua mpendwa akikuita unaitikia. Hii ndiyo kazi ya watumishi wote wa Mungu. Kutowatii ni kutomtii Mungu. Tulipoitwa kuhudumu

tuliitika na hakuna kurudi nyuma. Itakuwa makosa Mtumishi wa Bwana kuivuta nyuma kazi yake.

**Meya**: Kwa kweli Baraza la mji linashukuru kwa kulikumbuka daima katika maombi ya kulibariki. Baraza linaomba ufike kuliombea mara moja kwa juma. Litagharamia petrol ya kukuletea hapa na kukurudisha.

**Mhubiri**: Bwana asifiwe!

**Meya**: Pia Baraza litatoa sadaka ya shilingi laki moja kila mwezi. Watu wengi hawatambui mchango mkubwa wa wahubiri. Chini ya uongozi wangu Baraza hili litajitolea kutambua mchango wa wahubiri.

**Mhubiri**:Ameen!

**Meya**: Hilo ndilo nililokuitia mtumishi. Uk.41(*Mstahiki Meya*)

### 4.3.2 Mwingiliano wa Kimaudhui kwa kurejelea Ujumbe

Kwa kurejelea ujumbe, kazi tatu za kifasihi zilizoteuliwa ziliweza kutahminiwa. Mtafiti alitumia kigezo cha ujumbe kutathmini masuala muhimu ambayo yanafasiriwa katika matini zote tatu. Mtafiti aliongozwa na kigezo cha uathiriano na uigaji katika kuchambua masuala haya katika matini hizi. Masuala yafuatayo yalijitokeza kisambamba katika matini zote tatu kama ifuatavyo:

#### 4.3.2.1 Ufisadi

Ufisadi unadhihirika, wakati ambapo Mtemi Bokono anamtumia Gege ili kujinufaisha kwa kumuua kakake, Mwelusi. Aidha, ufisadi unadhihirika wakati Batu anatumia cheo chake kama mshauri mkuu wa Mtemi Bokono ili kumwua Mwelusi. Batu anawaita makachero na kuwapa mwongozo wa namna watakavyofaulu kumshawishi Gege. Makachero wanamuita Gege katika ukumbi wa utawala wa Butangi ili kumshawishi atekeleze mauaji ya Mwelusi. Ufisadi hapa unajitokeza kwa njia mbili; kwanza kuna matumizi mabaya ya mamlaka hasa kwa upande wa Bokono na Makachero. Aidha, kuna matumizi mabaya ya mali ya umma wakati Gege anapewa hongo kutokana na mali ya wizi ya umma. Jambo hili linaashiria ufisadi.

**Batu**: Ndiyo, Gege. Wewe ni 'mkuki wa Almasi'. Butangi nzima itafahamishwa Mtukufu Mtemi atakapokuwa na mkutano. Na si hivyo tu,Gege. Utapewa ardhi nzuri ili uitumie utakavyo.

**Gege**: (*Kwa furaha nyingi*) Asante sana. (*Akimwinamia Bokono*) Nashukuru sana,Baba wa Busara, Baba wa Wanabutangi wote.

Uk. 100(*Kifo Kisimani*)

Hali ya mwingilianomatini katika kiwango cha maudhui inadhihirika zaidi wakati mhubiri anamtembelea Mstahiki Meya. Uhusiano huu unajengwa na Bili ambaye anamjulisha Meya kuwa atamwambia mhubiri aje ili waweze kuzugumza na kuiombea Baraza pia. Aidha, anamhakikishia kuwa mhubiri pamoja na wenzake wote wako nyuma yake.

Mhubiri anaahidiwa sadaka ya hela nyingi kila mwezi na Mstahiki Meya. Hela hizi anapewa si mali ya Meya binafsi mbali ni mali ya umma. Mstahiki Meya anamahadi Mhubiri kuwa zaidi ya kupewa sadaka ya laki moja kila mwezi, atakuwa akigharamiwa mafuta kila mara anapokuja kuliombea baraza. Nia yake ni kujinufaisha kutokana na uongozi wa Mstahiki Meya kwani badala ya kuukashifu uovu unaoendelezwa na viongozi anamsifu ili kujipendekeza zaidi. Hali hii inaashiria urudufiano kwa kuwa anashabihiana na hali iliyopo kwa kazi tangulizi. Hali hii ya kujipendekeza kwa viongozi ili mtu anufaike inajitokeza kwa njia sawa katika kazi hizi.

> **Meya**: Kwa kweli Baraza la mji linashukuru kwa kulikumbuka daima katika maombi ya kulibariki. Baraza linaomba ufike kuliombea mara moja kwa juma. Litagharamia petroli ya kukuleta hapa na kukurudisha.
>
> **Mhubiri**: Bwana asifiwe!
>
> Uk.44(*Mstahiki Meya*)

Katika *Kifo Kisimani*, ufisadi unadhihirika zaidi wakati Bokono anawagawia watu ardhi ya umma kwa njia isiyo halali. Mtemi Bokono, anachukua ardhi iliyokuwa imetegewa kuchezea watoto na anapeana kwa Mkuu wa Askari.

Mkewe Nyalwe anapomuuliza anasalia kudai kuwa alipeana kwa kuzingatia kanuni ya ardhi. Aidha, baada ya kufuatiliwa kwa kina na Mama Agoro anakataa kutoa ufafanuzi mwafaka.

> **Nyalwe**: Ninayozungumzia ni muhumu. Usitie mzaha! Mama Agoro alikuja kulalamika.Anasema uwanja wa kuchezaea watoto wao umechukuliwa. Umepewa Askari Mkuu.
>
> **Bokono**: Aliyempa Askari mkuu ni nani?
>
> **Nyalwe**: Mgawa Ardhi.
>
> **Bokono**: Basi kwa nini alikuja hapa badala ya kwenda kwa mgawa ardhi?
>
> **Nyalwe**: Wafanyakazi wanaopuuza kanuni zinazoongoza mamlaka yao,sharti mkubwa wao akumbushwe kuzingatia kanuni hizo.
>
> **Bokono**: Mgawa ardhi amepuuza kanuni gani?
>
> **Nyalwe**: Ni ardhi ya matumizi ya umma kwa mujibu wa kanuni za ardhi.

Uk.18-19(Kifo Kisimani)

Ufisadi unajitokeza zaidi katika *Kifo Kisimani* ambapo Mtemi Bokono anawapa kazi wale wanaomfurahisha na kumsifu katika uongozi wake. Hali hii inajitokeza pale ambapo Kaloo ambaye ni kiongozi wa nyimbo za kumsifu Mtemi katika mikutano yake. Kutokana na hali hii, Mtemi Bokono anampa mwanawe kazi kama njia ya kumpongeza. Aidha, Kaloo anataka kwenda kwa Bokono akamshukuru kwa wema huo. Ni dhahiri kwamba, Mtemi Bokono anataka kushiriki na Kaloo katika Ngono pia.

**Kaloo**: Kwanza nataka kukushukuru.
**Zigu**: Shukrani ya nini?
**Kaloo** : Fadhila kubwa kwangu; kuzungumza na Mtemi juu ya haja yangu. Asante…
**Zigu**: Si neno Marafiki hawana budi kusaidiana kunapokuwa na haja. Pia mimi na washauri wengine wa Mtemi tunafurahi. Kwa hakika, hata Mtemi mwenyewe anafurahi.Kaloo, umeitendea Butangi mengi mema. Asante. Uk.88(*Kifo Kisimani*)

Katika Mstahiki Meya, hali kama hiyo inajitokeza wakati Msatahiki Meya anapeana kazi. Anampa kazi mhazili wake bila kuzingatia utaratibu unaofaa. Hali hii inaashiria ufisadi. Baadaye Mstahiki Meya anakiri kwamba alimpa kazi ambayo hakuwa anastahili baada ya kuungana na wengine katika mgomo.

**Meya**: (*Anajisemea*) Kagoma naye baada hisani ya kumpa ajira! Mtu ambaye hata hakustahili kupata kazi! *(Kwa uchungu.*) Nikampigania mimi na sasa anaungana na mahasidi kunitoa roho! Kumbe kufanya hisani ndiko kuharibu! Asante ya punda ni mateke. (*Akitazama Gedi*) Gedi!
**Meya**: Mpigie simu umwambie namtaka kazini mara moja.
**Gedi**: Nasikitika Mstahiki Meya, hawezi.
**Meya**: (*Kwa ukali*) Hawezi?

Uk.77(Mstahiki Meya)

Kuna ufisadi zaidi kuhusu matumizi ya mali ya umma. Mstahiki Meya anatumia mali ya umma kwa njia isiyo sahihi. Hali ya ubadhirifu inadhihirika wakati Mstahiki Meya anatumia mali ya umma kujinafasi akiwa na mwenzake Bili. Anampeleka Bili pamoja na familia yake katika hoteli inayoitwa Kajifahari. Wanakula vyakula vya bei ghali pamoja na watoto wao kupata nafasi ya kuogelea. Gharama hii inasimamiwa na *entertainment vote* ya

Meya ambayo ni kutoka kwa mali ya umma. Huu ni ufisadi kwa sababu Bili si kiongozi rasmi katika eneo la Cheneo bali ni rafiki tu. Anatumia mamlaka aliyo nayo kama njia ya kumfurahisha rafiki yake.

> **Bili**: (*Akiketi*). Ahsante. Nashukuru ndugu.
> **Meya**: Habari za siku nyingi?
> **Bili**:Nzuri ingawa si nyingi. Zimepita wiki mbili tu tangutuoane.Unakumbuka siku ile katika mkahawa wa kKajifahari?
> Uk.26(*Mstahiki Meya*)

Hali ya ufisadi inajitokeza zaidi katika tamthilia ya *Kifo Kisimani*. Gege anaahidiwa mali nyingi ambayo atapewa na utawala wa Mtemi Bokono. Makachero walipompeleka katika utawala wa Mtemi, wanamshawishi wamwue ndugu yake. Baada ya kutekeleza kitendo hicho, basi alimwahidi kuwa atapewa mali nyingi. Ukweli ni kwamba, mali anayopewa si ya mtu binafsi bali ni ya umma. Alifanikiwa kutekeleza haya kwa kuwa alikuwa na tamaa nyingi sana ya mali. Katika hali hii, Gege anashawishika na kukubali kumwua nduguye. Alipotekeleza unyama ule, Mtemi Bokono alisema apewe mali pamoja na jina la Mkuki wa Almasi. Aidha, alikataa wazo la kumpa bintiye Alida awe mkewe.

> **Gege**: (*Kwa furaha nyingi*) Asante sana. ( *Akimwambia Bokono*) Nashukuru sana, Baba wa Busara, Baba wa Wanabutangi wote. (*Bokono anatingisha kichwa polepole kama ishara ya kukubali shukrani za Gege).*
> **Batu**: Unaweza kuondoka. Keshokutwa utapelekwa kwa Mgawa Ardhi ili akuonyeshe mali yako. (*Mweke anaanza kuelekea kwenye mlango ili amfungulie Gege*). Uk.100(Kifo Kisimani)

Hali hizi zinadhihirisha hali ya uingiliano matini kwa kiwango maudhui kwani hali hizi zinashabihiana kwa njia ya kurudufiwa. Waandishi hawa wametoa hoja zao kwa njia inayoshabihiana. Ujumbe unaokusudiwa wa kuendeleza ufisadi kwa njia ya kuwapa maelezo mwafaka.

**4.3.2 .2 Unafiki**

Unafiki unajitokeza katika matini teule kwa njia ambayo inadhihirisha mwingilianomatini. Mwingilianomatini huu unajitokeza kwa hali ambayo inaegemea mihimili mbalimbali ya uingiliano matini. Uingiliano matini huu unajikita vilevile katika maudhui ila kwa kuhusiana karibu sana na uhusika. Unafiki ni hali ya mhusika kufanya jambo kinyume na jinsi anavyojaribu kusawiri. Kwa mujibu wa TUKI (1981), unafiki ni hali

ya kujifanya kuwa ni rafiki na hali ni adui; hali ya kutokuwa mkweli.Gege anadhihirisha unafiki katika uhusiano kati yake na Mwelusi. Gege anaunga mkono utawala wa Mtemi Bokono kinyume na kakake Mwelusi ambaye anapinga uongozi huo. Mwelusi anapinga uongozi wa Mtemi Bokono kutokana na hali mbaya ya uongozi ambayo inaendelezwa na Mtemi Bokono katika eneo la Butangi.

Gege anajali maslahi yake mwenyewe kwa hivyo hataki kuungana na wale wanaopinga utawala wa Mtemi Bokono. Badala yake, anajipendekeza kwa utawala wa Mtemi ili kujinufaisha. Ili afanikiwe katika mambo haya, Gege anakuwa mnafiki katika uhusiano huu ili asitambulike na mwenzake. Anajifanya kuwa rafikiye Mwelusi ili atambue siri zake. Baadaye anatumiwa na makachero wa Mtemi kutekeleza mauaji ya kakake.

> **Gege**: (*Kimya kifupi*) Unamaanisha nini unaposema kwamba labda niyaporomoshe mambomwenyewe.
>
> **Mweke**: Namaanisha ya kuwa ndoa baina yako na binti Mtemi haina vikwazo vyovyote. Labda uvijenge mwenyewe.
>
> **Gege**: Sidhani naelewa jambo unalolizungumzia.
>
> **Mweke**: Bahati nasibu inapomteremkia mtu, mara nyingine uhalisi huonekana kama ndoto. Mambo huwa hayaeleweki kwa urahisi. Kimya…
>
> **Gege**: Ushirikiano gani?
>
> **Mweke**: Ushirikiano kuhusiana na ndoa yako na pia kuhusiana na ujenzi wa Butangi. Unajua Bwana Gege, Butangi haiwezi kuendelea bila amani. Na haiwezi kuwa na amani watu wachache wasiotosheka wakiruhusiwa kuchafua vichwa vya Wanabutangi. Ili kuhakikisha kwamba Butangi inaendelea kuwa na amani, ni muhimukukomesha wachochezi.(*Kimya kifupi*) Unamfahamu vyema nduguyo Mwelusi. Uk.73 (*Kifo Kisimani*)

Hali hii inadhihirisha kuwa ni mwingilianomatini kwa kiwango cha maudhui kaitika Utendi wa Fumo Liyongo ambapo Mwanawe Fumo anadhihirisha aina hii ya njia ile ile. Hali hii ianegemea kwa mhimili wa urudufu kwani mwandishi anatumia njia hiyo hiyo kupitisha suala hili.

Katika Utendi wa *Fumo Liyongo,* mwanawe Fumo anadhihirisha unafiki kwa kujifanya kuwa ni rafiki wa karibu wa babake ili aweze kutambua siri ya nguvu zake. Aidha, babake hakutambua njama hiyo. Mfalme Mringwari anachukua nafasi ya kumshawishi mwanawe Fumo ili aweze kutekeleza mauaji ya babake.

Kwa kutojua unafiki wa mwanawe, Fumo anamjulisha mwanawe siri ya nguvu zake na jinsi angeweza kutolewa uhai. Anapomjulisha, mwanawe anatekeleza mauaji hayo na kusababisha taanzia katika jamii yao. Mwanawe Fumo hakutambua unafiki wa Mfalme Mringwari kuwa alikuwa anajifanya tu ilmradi Fumo Liyongo auliwe. Mfalme Mringwari anadhihirisha unafiki kwa kuwa, mwishowe hakuweza kumpa mwanawe Fumo zawadi aliyomhaidi.

144. Jamii silaha piya
Hazimwuwi swabiya
Ila nimezokwambiya
Ni ya kweli yote piya
145. Kijana akisikiya
Shughuli lalimngiya
Kataka kusikilya
Pate akanene haya.
150. Kenenda kwa Sulutwani
Akaitaka idhini
“akanena nitieni
Kwa upesi nawambiya.(*Utendi wa Fumo Liyongo*)

Mwingiliano wa maudhui haya katika tungo hizi mbili unadhihirisha mwingilianomatini katika kiwango cha maudhui. Unasawiri hali ya kurudufiwa kwa maudhui kwa njia ya uathiriano. Hali hii inaashiria mwingilianomatini katika uathiriano na uigaji.

Vilevile, katika Tamthilia ya *Mstahiki Meya*, unafiki unarudifiwa. Mstahiki ana urafiki wa karibu na mhusika Bili ambaye alikuwa ajihesabu kama mshauri wa baraza ilmradi afaidike tu. Aidha, Bili anadhihirisha unafiki kwa kujifanya kuwa pamoja na Meya ilmradi afaidike tu. Anampa Meya ushauri unaompotosha na mambo yanapoharibika hapatikani mahali popote.

Anafaidika na unafiki wake kwa kuwa alipata nafasi ya kujitajirisha. Kutokana na hali hii, Mstahiki Meya anampa Bili vipande vya ardhi. Aidha, kwa wakati mwingine anatumia mamlaka aliyo nayo kumpeleka Bili pamoja na familia zao kujivinjari. Pesa wanazotumia ni mali ya umma. Bili anazima simu mambo yanapomharibikia Meya badala ya kujitokeza kumsaidia. Hali hii inadhihirisha mwingiliano matini kwa njia ya kurudufiwa na pia uathiriano.

Bili: Nzuri ingawa si nyingi. Zimepita wiki mbili tu tangu tuonane. Unakumbuka sikuile katika mkahawa wa Kajifahari?

Meya: Wiki mbili chache?
Bili: Si chache vile. Nyingi kwa ndugu waliozoeana.
Uk.26 (*Mstahiki Meya*)

Mambo yamebadilika katika usemi wao baada ya hali ya Cheneo kuharibika kama inavyodhihirika.

Meya: (*Amechanganyikiwa.*) Bili yuko wapi?
Diwani I: Siku mbili sasa sijamsikia.
Meya: Kweli (*Anachukua simu na kupiga. Anasikiliza.*)
Mteja!
Diwani III: Mimi nimempigia tangu juzi naye hapatikani.
Uk.75 (Mstahiki Meya)

**4.3.2.3 Dini**

Kwa nujibu wa TUKI (2004), dini ni imani inayohusiana na maumbo ya kiroho kwamba kuna Muumba aliyeumba ulimwengu huu, na kwamba, ndiye mtawala wa kila kilochomo. TUKI wanaongeza kwa kusema kuwa, ni mfumo fulani wa imani na njia ya kuabudu, kusali na na kumtii huyo Muumba.

Katika utendi wa fumo Liyongo, wazo la dini linaangaziwa kupitia hali ya watesi wa Fumo Liyongo. Wakati Fumo Liyongo alikuwa gerezani na wakaamua kumwua, wanampa Fumo nafasi ya kujisalimisha kwa Mola kwa njia ya maombi. Wazo hili linazua dhana mwafaka kuwa jamii hii ina imani kwa Muumba. Wanadhihirisha kupitia wazo la kumpa Liyongo nafasi ya kujiunganisha na Muumba wake kabla hawamtoa uhai. Aidha, hawakufanikiwa kwa sababu Liyongo alitoa ombi kuwa apigiwe ngoma ya mwao na gungu na katika hali hiyo akazungumza na kijakazi Saada ili ampe mama ujumbe mwafaka.

Ujumbe wa Liyongo ni kuwa atengenezewe mkate wa wishwa halafu ndani yake tupa kutiwa ndani. Kijakazi Saada anapofiksha ujumbe kwa mama yake, mama nafanya hivyo na hivyo Liyongo kutumia tupa hiyo kujiopoa gerezani. Anatumia tupa hiyo kukereketa vyuma vilivyomfungia gerezani.

"Mekwambia Bwana wetu
Menituma mimi mtu
Muhula wa siku tatu
Fahamu utauwawa."

Akajibu "Usikhini
Kamwambie Sultwani

Mwao nimeutamani
Na gungu liwe pamoya."
(Ubeti 97-98) (*Utendi wa Fumo Liyongo)*

Maudhui ya dini yanajitokeza zaidi katika tamthila ya *Kifo Kisimani* kupitia. Hali hii inajitokeza kupitia kwa mhusika Azena. Ijapokuwa si wazi kabisa ila Askari wanadhihirisha kuelewa misingi ya dini hasa kuhusu usamehevu. Baada ya Mwelusi kutoroka gerezani, Askari II anaomba msamaha kwa Batu kama njia ya kupata afueni.

**Batu**: Mtasamehewa! Mtasemehewa baada ya kuomba msamaha-msamaha imara.
**Askari II**: (*Kwa unyenyekevu mwingi*) Tafadhali. Uk.63(*Kifo Kisimani*)

Arege anaweka wazi maudhui ya dini kupitia mhusika mhubiri. Mhubiri ni mhusika katika tamthilia ya Mstahiki Meya ambaye amepata mwaliko na Meya Sosi awe anaenda kuiombea Baraza. Hii ni baada ya Meya kushauriwa na Bili kuwa amtafute kwa kuwa atakuwa wa msaada kwa kumwezesha kupata wafuasi wengi.

Dini inachorwa kama njia ya kujipatia mali. Mhubiri anakosa kuwajibika katika wajibu wake kama mhubiri ambaye anapaswa kukosoa uongozi mbaya. Mhubiri anakubali kuumunga mkono Meya kwa kuwa anampa sadaka nono na zaidi anagharamia usafiri wake kila mara anpoenda kuiombea baraza.

**Meya**: Nashukuru mtumishi kwa kufika hapa.
**Mhubiri**: Karibu ndugu mstahiki.
**Meya**: Ninajua mpendwa akikuita unaitikia. Hii ndiyo kazi ya watumishi wote wa Mungu. Kutowatii ni kutomtii Mungu. Tulipoitwa kuhudumu tuliitika na hakuna kurudi nyuma. Itakuwa makosa Mtumishi wa Bwana kuivuta nyuma kazi yake.
Uk.41(*Mstahiki Meya*)
**Meya**: Kwa kweli Baraza la mji linashukuru kwa kulikumbuka daima katika maombi ya kulibariki. Baraza linaomba ufike kuliombea mara moja kwa juma. Litagharamia petrol ya kukuletea hapa na kukurudisha.
**Mhubiri**: Bwana asifiwe!
**Meya**: Pia Baraza litatoa sadaka ya shilingi laki moja kila mwezi. Watu wengi hawatambui mchango mkubwa wa wahubiri. Chini ya

uongozi wangu Baraza hili litajitolea kutambua mchango wa wahubiri.

**Mhubiri**: Ameen!

**Meya**: Hilo ndilo nililokuitia mtumishi.

**Mhubiri**: Hilo ndilo nililokuitia Mtumishi.

Uk. 44(*Mstahiki Meya*)

Dini inadhihirika kuegemea upande wa kisiasa kwani Meya anaelewa kuwa ili aweze kukubalika na watu wengi basi itabidi apate kuungwa mkono na mhubiri. Mhubiri anakubali kutumiwa na Meya kwani anajitolea kutekeleza yale ambayo mhubiri anataka kutoka kwake. Anachukua mkondo mpya wa kisiasa bila kujali hali ya wanacheneo wanaoteseka.

Dini inaendeleza ubinafsi. Mhubiri ana jukumu la kuhubiri amani na kuwatakia watu katika jamii maisha mema. Aidha, hali ni todfauti kwa kuwa mhubiri anajali maslahi yake binafsi kwa kuwa anakataa kumkosoa Meya kwa uovu anaoendeleza. Anamrejelea Meya kama mtumishi wa Bwana hali ambayo inaashiria kuwa anaunga mkono uongozi wake.

Tamaa ya mali inachipuka wazi kupitia kwa dini. Meya anelewa kuwa mhubiri ana tama ya mali. Kutokana na hali hii, anamtumana Mhubiri aje kwake ili atoe maombi kwa baraza. Meya naye kwa sababu ya tamaa anaingia katika mtego wa Mstahiki Meya Sosi. Anakubali kutumia cheo chake kama Mhubiri ili kujinufaisha. Kama vile imetajwa hapo juu, anakubali sadaka ya laki moja kila mwezi kutoka kwa baraza.

Dini inaendeleza ubadhirifu katika jamii. Pesa za kiwango laki moja kwa kila mwezi ni pesa nyingi kwa matumizi ya mtu mmoja ambaye hana kazi maalum katika baraza. Baraza linaeleza kuwa lina nakisi. Watu wanaotozwa kodi ili kufidia nakisi ya fedha iliyopo katika bajeti lakini bado kuna nakisi. Nakisi hii inachangiwa zaidi na dini kupitia kwa mhubiri ambaye anapokea kiasi kikubwa cha pesa kama vile imetajwa hapo juu.

Kwa kutamatisha, inadhihirika kuwa dini ina nafasi kubwa katika ukamilifu wa jamii yoyote ile. Kazi hizi ambazo zina mandhari tofauti lakini bado waandishi wanazua wazo la dini kwa kiwango tofauti kufafanua nafasi yake katika jamii. Aidha, hali mwingiliano wa kipekee unajitokeza kama vile inavyoakisiwa katika mjadala huwa maudhui ya dini. Ni wazi kuwa uathiriano huu katika kiwango cha maudhui unadhihirisha mwingilianomatini katika matini hizi tofauti.

#### 4.3.2.4 Ukosefu wa Uwajibikaji

Uwajibikaji ni hali mhusika kujua kazi yake katika jamii na kuitekeleza.Kwa mujibu wa Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2011) kuwajibika ni hali ya mtu kuwa na wajibu wa

kufanya. Katika matini hizi watu mbalimbali wana majukumu mbalimbali ya kutekeleza kutegemea vyeo wanavyo katika jamii. Katika hali hii, wengine wamekosa kuwajibikia nafasi zao katika jamii hali ambayo inadhihirisha ukosefu wa uwajibikaji.

Katika utendi wa Fumo Liyongo, uwajibikaji unajitokeza kupitia kwa mhusika Mfalme Daudi Mringwari. Kama mfalme, ana jukumu la kulinda uhai kwa kila mwanajamii. Kama mfalme, ana jukumu la kulinda kila mmoja aliye chini ya utawala wake. Aidha, anatumia nafasi yake kama kiongozi kumwangamiza Fumo Liyongo. Anapanga jinsi ya kumwua Fumo kwa kutumia mwanawe Liyongo.

83. Naye huyo Sultwani
Kuuwa hawezekani
Akinena ni yakini
Hutimiza mara moya (*Utendi wa Fumo Liyongo*)

Hali ya kutowajibika inadhihirika katika tamthilia ya Kifo kisimani kupitia kwa wahusika mbalimbali. Kwanza kabisa ni kupitia kwa mhusika Mtemi Bokono ambaye amepewa nafasi ya kuwa kiongozi katika utawala wa Butangi. Kama kiongozi katika utawala wa Butangi ana jukumu la kuhakikisha kuwa Wanabutangi wana maisha mazuri na kuwa matakwa yao yameshughulikiwa.

Ni wazi kuwa matakwa yao hayashughulikiwi kwa sababu wanakosa maji jambo ambalo ni la kimsingi. Wanakatazwa kuteka maji katika kisima cha Mkomani. Wanaambiwa kuwa hawana ruhusa ya kuteka maji katika kisima cha Mkomani.

Kuna unyakuzi wa ardhi ya umma kwa matumizi ya watu binafsi. Mama Agoro anaenda kwa Mtemi Bokono kulalamika kwa sababu uwanja wa kuchezea watoto wao umenyakuliwa na kupewa Mkuu wa Askari. Mkuu wa Akari amepewa uwanja ambao ni mali ya umma kwa kuelekezwa na Mtemi Bokono.

Askari wanakosa kuwajibika katika kuwalinda wafungwa gerezani. Wafungwa gerezani wanateseka kwa kukosa chakula kwa sababu chakula wanacholetewa kinaliwa na Askari. mamake Mwelusi anamtuma Andua kumpelekea chakula lakini badala ya kuwapa wanakila wenyewe.

Mtemi Bokono ana washauri ambao wanapawsa kumshauri jinsi ya kuiongoza Butangi lakini badala yake wanatumia nafasi zao kujinufaisha wenyewe na kumpotosha. Wanampotosha kwa kumuelekeza kuiongoza Butangi kwa njia ambayo inawanyanyasa Wanabutangi. Nyalwe ambaye ni mkewe mtemi anamwambia mumewe ajiepushe na ushauri

mbaya anaopata kutoka kwa hao washauri wake lakini anakosa kumsikiliza. Mwishowe alijitosa katika hatari anapong'atuliwa mamlakani na wakereketwa wa uongozi mbaya.

**Bokono**: Hilo si kweli.
**Nyalwe**: Hilo ni kweli. Ndiyo sababu unaona watu wakikuzika.
**Bokono**: Ilikuwa ndoto tu.
**Nyalwe**: Ndoto ni picha ya yaliyomo akilini.
**Bokono**: Najielewa vyema kuliko mke wangu anavyonielewa.
**Nyalwe**: Mbona usibadili mienendo yako?
**Bokono**: Mienendo gani?
**Nyalwe**: Uongozi mbaya! Acha kuteda mambo yanayowaumiza watu.
**Bokono**: (Kwa sauti dhabiti) Napendwa sana na watu. Uongozi wangu ungelikuwa mbaya, watu hawangelikuwa wakinipongeza katika kila pembe ya Butangi.)
**Nyalwe**: Unadanganywa. Unadanganywa na wanafiki unaowaita washauri waaminifu.
Uk.15-16(*Kifo Kisimani*)

Katika Tamthilia ya *Mstahiki Meya*, hali ya utowajibikaji bado inaendelezwa. Mtunzi anamtumia wahusika mbalimbali kuleta dhana ya watu kutowajibika katika matini yake. Kwanza kabisa anamchora mhusika Meya kama kiongozi asiyewajibika katika kazi yake. Kiongozi huyu hawajibiki kwani Wanacheneo wanateseka chini ya uongozi wake mbaya. Anakosa kuleta dawa hospitalini na watu waneaendelea kufa kwa kukosa dawa. Anadaganya kuwa dawa zimo njiani lakini ukweli ni kwamba hakuna dawa ambazo ameagiza kutoka ughaibuni.

**Waridi**:Baada ya siku tatu dawa zitakuwa tayari zimeisha kuwasili bandarini. Siku tatu hivi baada ya kuwasiliti tutakuwa tumezipokea hapa hospitalini.
**Siki**: (*Anamtazama kwa kudadisi*.) Una hakika?
Uk.2(*Mstahiki Meya*)

Kama kiongozi anapaswa kuwajibika kwa kuhakikisha kuwa watu wamepata elimu. Kinyume na hayo, anakosa kushughulikia elimu katika shule za cheneo. Yeye mwenyewe anakiri kuwa kiwango cha elimu Cheneo ni cha kiwango cha chini zaidi. Kwa sababu kiwango cha elimu katika Cheneo ni cha chini, anawepeleka wanawe Ng'ambo kwenda kusomea huko huku watoto wa maskini wakiendelea kupata elimu duni.

**Bili**: Nakumbuka uliisha kunitajia kuwa wangeenda kusomea ng'ambo. Mpango mzuri.

**Meya**: Ndiyo hivyo bwana. Elimu yetu hapa ni ya kawaida mno. Haina kubwa la kumfaa mtoto mwenye mzazi anayeona mbali.

Uk. 26(*Mstahiki Meya*)

Madiwani wamechaguliwa na watu ili kuhakikisha kuwa wamewashughulikia katika mahitaji yao. Wanakosa kufanya hivyo na badala yake wanajali maslahi yao wenyewe. Wanajali maslahi yao wenyewe kwani walipuuza matatizo ambayo wanacheneo wanayopitia na badala yake wanaendelea kujinufaisha. Wanajiongezea mishahara ilhali wengine wamekosa mishahara na wanapolipwa wanalipwa mshahara nusu. Zaidi ya kjiongezea mishahara wanajipa ovataimu na hawatozwi kodi. La kushangaza ni kuwa hawatozwi kodi ilhali mama muuza ndizi anatozwa kodi.

**Meya**: Wewe hukubaliani na chochote siku zote. Kauli yako ndiyo waiona kuwa yenye hoja inayostahili kufuatwa. Lakini usisahau kuwa sisi pia tulichaguliwa wewe. Wale watu wangekuwa na uzito wangekuwa hapa kuliongoza baraza.

**Diwani III**: Kumbuka wametutuma kuwawakilisha.

Uk.53(*Mstahiki Meya*)

Mhubiri ni mhusika mwingine asiyewajibika katika kazi yake. Anakosa kuwajibika kwa sababu badala ya kuwatetea wanyonge wanaokandamizwa na Meya anaendelea kuunga mkono uongozi mbaya wa Meya. Kama kiongozi wa dini anapaswa kuhakikisha kuwa anawakosoa wanaoendeleza uozo katika jamii. Kinyume na hayo, anaendelea kuwasifu na kuwaunga mkono ili ajinufaishe menyewe. Anamsifu Meya ambaye anaendeleza uongozi mbaya na kudanganya kuwa wafuasi wake wako nyuma ya Meya. Kwa kufanya hivi anakosa kuwajibika katika kazi yake kama kiongozi wa kidini anayepaswa kukashifu maovu katika jamii.

**Meya**: Ninajua una shughuli nyingi ulizoacha na kufuata wito wangu. Ni ukarimu mkubwa huu kutoka kwako.

**Mhubiri**: Ndugu mpedwa akikuita unaitika. Hii ndiyo kazi ya watumishi wote wa Mungu. Kutowatii ni kutomtii Mungu. Tulipoitwa kuhudumu tuliitika na hakuna kurudi nyuma. Itakuwa makosa Mtumishi wa Bwana kuivuta nyuma kazi yake.

Uk.41(*Mstahiki Meya*)

#### 4.3.2.5 Ubinafsi

Kwa mujibu wa TUKI (2013), ubinafsi ni hali ya mtu kujifikiria na kujipenda yeye mwenyewe. Kutokana na maelezo haya, hali ya ubinafsi inajitokeza wakati wahusika mbalimbali wanadhihirisha kujiwazia wao wenyewe ili kujifaidi bila kuwawazia wengine. Hali ya ubinafsi inajitokeza katika wahusika hawa kutenda maovu ambayo yanawaumiza wegine ili wajinufaishe.

Katika Utendi wa Fumo Liyongo, mhusika Mringwari anadhihirisha ubinafsi anapopanga njama ya kumwangamiza Fumo ili aendelee kutawala Pate. Ni dhahiri kuwa, Fumo hana nia ya kumtoa Mfalme Mringwari mamlakani lakini Mfalme ana hofu. Kwa sasababu ya hofu aliyo nayo, anajaribu njama mbalimbali za kumwondoa Fumo duniani. Kwanza anatumia Askari wake ambao walishindwa kumuua Liyongo. Hii ni kwa sababu Liyongo alipotambua nia ya Mringwari aliamua kwenda nchi za mbali akaishi huko.

Alipotoroka Pate Liyongo alielekea kwa Wasanye. Akiwa huko, Fumo aliendelea kutafutiwa mbinu ya kuuawa. Mringwari alitafuta mbinu ya kumwua akiwa huko. Alipanga njama na Wasanye wamwue. Kwa vile walikuwa wanachuma makoma jangwani, walimhadaa Fumo kuwa wangefanya hivyo kwa zamu. Walitaka zamu yake ikifika wamwue kwa kumfuma mishale hali ambayo inadhihirisha ubinafsi. Walijali maslahi yao wenyewe. Aidha, hawakufaulu kwa sababu Liyongo aliamua kuyatunda kwa kuyafuma kwa mishale.

57. Kikowa tule makoma
    Kukuta hatutokoma
    Kula tukiiterema
    Kula mtu siku moya
58. Shauri likisa lao
    Wakenenda kwa kikao
    Mkoma waupatao
    Hupanda mtu mmoya
66. Achangusha ngaa ndima
    Ni mangi mno makoma
    Kwa wut'e wakaatama
    Ajabu zikawangiya (*Utendi wa Fumo Liyongo*)

Ubinafsi zaidi unajitokeza katika mauaji ya Liyongo. Mwanawe Liyongo aliahidiwa mali iwapo angefaulu kutambua ni kitu gani ambacho kingeweza kumwua babake. Kwa kutojua, Liyongo anamfunulia siri mwanawe kuwa angefariki kwa kudungwa na sindano ya shaba kitovuni mwake. Mvulana huyo alipogundua siri ya kumwua babake, alifululiza mara

moja hadi kwa Mfalme Mringwari. Mfalme anakubali kumwua Liyongo kupitia kwa mwanawe. Alimpa mwanawe sindano ya shaba akatekeleze mauaji hayo. Hali hii inadhihirisha ubinafsi kwani mwanawe Liyongo alimwua ili aweze kujinufaisha kwa kupata mali kutoka kwa Mfalme.

Maudhui ya ubinafsi yanaendelezwa zaidi na Mberia katika kazi yake. Katika matini yake, mhusika mkuu ambaye ni Mtemi Bokono, anaangazia hali ya uingiliano matini kimaudhui kwa kuendeleza maudhui ya ubinafsi hasa kwa njia sambamba ambayo inaendelezwa na matini tangulizi. Kama ilivyo katika utendi ambapo mfalme anapanga njama ya kumwua Mwelusi, ndivyo ilivyo katika hali hii. Mwelusi ambaye ni mpinzani wa Mtemi Bokono kwa kuwa anawazindua wanabutangi dhidi ya uongozi wake mbaya, anapangiwa jinsi atauliwa na vikaragosi wa Mtemi Bokono.

Batu anakutana na washauri wenzake ili kutafuta suluhu kumshughulikia Mwelusi. Katika kikao hicho kilihusu washauri ambao ni Zigu na Kame pamoja naye. Wanatafuta mbinu mwafaka ya kumnyamazisha Mwelusi. Katika kikao chao, Kame ana maoni tofauti kwa kuwa anapinga wazo la kumwondoa mfungwa duniani kwa njia ya mauaji. Kwa kufanya hivi, wanadhihirisha ubinafsi wa hali ya juu kwani wanajali maslahi yao wenyewe na si maslahi ya Wanabutangi au Mwelusi.

**Kame**: Napinga pendekezo la kumtenganisha mfungwa na uhai wake. Kwanza, hatuna ushaidi kwamba Mwelusi amekuwa akichochea umma dhidi ya Mtemi Bokono. Huenda ikawa anasingiziwa tu. Pili, hata ikiwa ni kweli amekuwa akichochea umma, kifungo kinatosha kulipia kosa hilo. Ni kosa kubwa kumtenganisha mtu na uhai.

**Zigu**: Msikize mwoga huyu!

UK.61(*Kifo Kisimani*)

Gege ambaye ni nduguye Mwelusi anadhihirisha ubinafsi zaidi kama ilivyo katika Utendi wa *Fumo Liyongo* kupitia kwa mhusika mwanawe Liyongo. Gege anaulizwa na makachero akubali kumwua Mwelusi ili atuzwe mali na ndoa kati yake na Alida. Anajifikiria mwenyewe mbali hafikirii maisha ya nduguye.

Tanya ambaye ni mamake Gege na Mwelusi anamwuliza iwapo ataenda gerezani kumwangalia nduguye. Gege anakataa na kusema kuwa yeye yuko na shughuli muhimu zaidi. Shughuli anazozirejelea hapa ni kutengeneza ala ya muziki ili aweze kutumbuiza wasichana katika ukumbi wa michezo. Anamwambia mama yake kuwa ana shughuli muhimu za kutengeneza maisha yake.

**Tanya**: Natumai leo hutakuwa kama jana ulivyokuwa jana!
**Gege**: Nilikuwaje jana, Mama?
**Tanya**: Nilikwambia ukamtazame nduguyo, ukakataa.
Uk. 43(*Kifo Kisimani*)

Mwishowe, Gege anamfuata Mwelusi kisimani na kumdaganya kuwa ana ujumbe muhimu kutoka kwa marehemu babake na hivyo ni vyema waende chemba. Kwa kutojua, Mwelusi anakubali kwenda chemba naye. Walipoenda chemba, Gege anamdunga Mwelusi kisu tumboni na kusababisha kifo chake. Kilichomwongoza Gege ni ubinafsi aliokuwa nao. Alitaka kupata mali kutoka kwa Mtemi Bokono kama alivyokuwa ameahidiwa.

**Zigu**: Kumbe mna zaidi ya kuteka maji?
**Gege**: Inaonekana kuna kutoelewana hapa. (*Kwa Mwelusi*) Habari gani? (*Akimpa mkono*) Pongezi kwa kufaulu kutoroka gerezani. **Uk. 94 (*Kifo Kisimani*)**

Katika Tamthilia ya *Mstahiki Meya*, ubinafsi wa viongozi walio mamlakani unaendelezwa hali ambayo inadhihirisha mwingilianomatini kimaudhui. Mstahiki Meya anaendeleza ubinafsi kwa njia mbalimbali. Kwanza kabisa, anakosa kuleta dawa hospitalini wala kuboresha huduma za afya. Yeye na familia yake wanapata matibabu kutoka nchi za ng’ambo. Kwa mfano, anmpeleka mkewe ng’ambo akajifungulie huko hali ambayo inadhihirisha kuwa anajali maslahi yake binafsi.

**Bili**: (*Kwa bashasha*). Mara ile ya mwisho tulipokuwa pamoja alionekana amechoka sana!
**Meya**: Ndiyo maana alisafiri ng’ambo. Madaktari wetu hawa wa kubabaisha tu. Kule ng’ambo ndipo walipo wakunga wenyewe. Sikutaka kubahatisha. Halafu tena mototo akizaliwa huko anapata uraia wa huko huko. Uk.27 (*Mstahiki Meya*)

Vilevile, kiwango cha elimu kimedorora katika eneo la Cheneo. Meya anakosa kuboresha kiwango cha elimu kwa kuwa anajali maslahi yake mwenyewe wala si ya Wanacheneo. Anawapeleka wanawe ng’ambo wakasomee huko kwa kudai kuwa kiwango cha elimu cha Cheneo kiko chini sana kwa mtu anayeona mbali kama yeye.

Madiwani wa Meya wanaendeleza ubinafsi pia. Wanapokea mshahara wa kiwango cha juu ambao hautozwi kodi ilhali mama muuza ndizi anatozwa kodi. Vilevile, wafanyikazi hawalipwi hali ambayo inachangia pakubwa katika kuzua migomo. Wanaolipwa hawapewi

mishahara yao ikiwa kamili mbali wanalipwa nusu. Hali hii inadhihirisha ubinafsi kwani wanajali maslahi yao lakini si maslahi ya wale ambao wamewachagua.

> **Diwani III**: Ndugu Meya! Usisahau kuwa wale wafanyakazi wanaogoma ndio wa chomwao na jua kutuletea sisi tunaopokea kivulini.
> **Meya**: Sikiliza Kheri. Diwani ni Diwani. Huwezi kumlinganisha na yule mtu pale chini. Mji huu hauendi bila madiwani.
> Uk.53(*Mstahiki Meya*)

Mbinu ya tenga utawale inayotumiwa na Madiwani inadhihirisha ubinafsi. Ubinafsi huu unajitokeza kwa kuwa Diwani I na Diwani II wanamtenga kwa kutomhusisha katika baadhi ya vikao ambavyo wanataka kuendeleza mambo yanayomuumiza mwananchi. Hali hii inaashiria ubinafsi. Wanajali maslahi yao wenyewe lakini hawajali maslahi ya Wanacheneo ambao wamewachagua wawaongoze.

> **Siki**: Ajabu hiyo!
> **Diwani III**: Meya ana uwezo mkubwa. Kushindana naye ni kama kushindana na ndovu. Utapasuka. Uk. 48(*Mstahiki Meya*)

**4.3.3 Mwingiliano wa Kimaudhui kwa kurejelea Mtazamo na Msimamo**

Matini tatu za kifasihi zilitathmniwa kimaudhui kwa kigezo cha mtazamo na msimao huku mchakato huu ukiongozwa na mihimili ya uathiriano, uigaji na urudufiano. Kwa kuangalia mtazamo na msimamo, mtafiti alitumia mafunzo na dhamira ya tungo zenyewe kutambua msimamo na mtazamo wa tungo zenyewe. Aidha, mtazamo na msimamo unalenga mtunzi au jamii ambayo kazi hizi zinalenga. Katika *Utendi wa Fumo Liyongo*, ilibainika wazi kuwa kazi hii inalenga jamii ya kabla ya ukoloni ambayo iliendeleza uovu bila uoga kwa kuwa sheria haikutiliwa maanani. Aidha, hakuna katiba iliyomfunga kiongozi dhidi ya kutekeleza aliyokusudia kutenda. Hivyo basi, msimamo wa jamii wa kujilinda dhidi ya maovu unatokea wazi wakati mwanawe Fumo anakashifiwa na jamii kwa maovu aliyotenda ya kumwua babake. Kwa kuwa jamii lengwa haina sheria zinazoifunga, hakuna anayedhubutu kumwuliza Mfalme Daudi Mringwari kwa nini alimwua Fumo Liyongo.

219. Watu akitahayari
Kwa ile yake amri
Watu wakimtiriri
Mayuto yakamwigiya
220. Kaingiya mayutoni
Katindikia nyumbani

Hata wenzi hawaoni
Hamu imezomngiya (*Utendi wa Fumo Liyongo*)

Mberia anaanza na mtazamo sawa na ule wa matini tangulizi kwa kuwa anaanza kwa kuweka wazi hali ya viongozi kuvunja sheria bila kujali kwa kuwa wao ndio walio mamlakni. Baadaye anachukua mtazamo tofauti kwa kuleta mtazamo wa kuwepo na sheria zinazomfunga kila mwanajamii licha ya tabaka lake. Anamtumia mhusika Mtemi Bokono na mawakala wake wanaopuuza sheria lakini mwishowe jamii inachukua hatua kuwasitisha dhidi ya maovu wanayowatendea. Wananyakua ardhi ya umma bila kujali. Mwishowe hali inakuja kubadilika pale ambapo Wanabutangi wanawatia mbaroni Mtemi pamoja na mawakala wake na kufikisha kikomo udhalimu wao. Katika kiwango hiki, mtafiti aligundua kwamba, Mberia ana mtazamo sawa na ule wa tungo tangulizi lakini kwa sababu hadhira lengwa ni ya karne ya ishirini, anatoa kauli zaidi ya dhidi ya kukabiliana na uovu ili kupata uhuru katika jamii.

Nyalwe: Ninayozungumzia ni muhimu. Usitie mzaha! Mama Agoro alikuja kulalamika. Anasema uwanja wa kuchezea watoto wao umechukuliwa. Umepewa Askari Mkuu.
Bokono: Aliyempa Askari Mkuu ni nani?
Nyalwe: Mgawa Ardhi.
Bokono: Basi kwa nini alikuja hapa badala ya kwnda kwa Mgawa Ardhi?
Nyalwe: Wafanyakazi wanapopuuza kanuni zinazoongoza mamlaka yao, sharti mkubwa wao akumbushwe kuzingatia kanuni hizo.
Bokono: Mgawa Ardhi amepuuza kanuni gani?
Nyalwe: Kanuni zinazolinda ardhi ya umma. Uk.19( *Kifo Kisimani*)

Uathiriano na uigaji katika kiwango cha maudhui kwa kurejelea maudhui unadhihirika zaidi katika kazi ya Arege. Matini ya *Mstahiki Meya* inaunga mtazamo na msimamo wa matini tangulizi kuwa uongozi ndio chanzo cha matatizo katika jamii. Haya ni kupitia mhusika Meya Sosi ambaye anaendeleza uongozi mbaya unaowaumiza Wanacheneo. Aidha, anapinga hatua zaidi ili kuafikia hadhira lengwa ambayo ni jamii ya sasa ya karne ya ishirini na moja. Anapinga hatua hii kwa kuonyesha vile tabaka la utawala linatumia sheria kujikinga wanapoendeleza maovu yao katika jamii. Meya ana *entertainment vote* inayomwezesha kutumia mali ya umma pasipo kulaumiwa. Meya na madiwani pia wanatumia *Mayor's act* ili kujilinda wanapotekeleza ufisadi na pia kujidumisha mamlakani. Ni dhahiri kuwa, mtazamo wa Arege unakubaliana na ule wa Mberia ila anapinga hatua zaidi kuakisi hali ilivyo katika jamii ya kisasa.

**Bili**: Wazima.Hawaishi kuizungumzia siku ile huko Kajifahari. Bado najiandaa halafu nitakuomba uje na Memsahib na watoto ili tukajinafasi.

**Meya**: Kama wanataka wewe walete tu. Kila kitu juu yangu. Nina entertainment vote ya Meyayangoja ualishi tu. Uk.26(*Mstahiki Meya*)

**Diwani III**: (*Polepole*) Anao tena sana. Kuna *Mayor's act* inayompa mamlaka kumchukulia mtu hatua kali. Kuna sheria nyingine iitwayo Riot *Act*. Hata akaitumia hii tu inatosha kumkunja kila aliye chini yake kama ua wakati wa alasiri.

**Siki**: (*Anamaka*.) Kumbe! Uk.48(*Mstahiki Meya*)

### 4.4. Namna Uathiriano, Uigaji na Urudufiano Unavyoelekeza Ufasiri wa Kazi za Fasihi

Kazi za fasihi huwa na maana mbalimbali kwa kutegemea namna zinavyohakikiwa. Misingi inayotumiwa kuhakikiwa ndiyo huelekeza namna kazi hizo zinavyofasiriwa. Maana mahususi huibuka huku lengo la mwandishi likiwekwa bayana. Hali hii imeidhihirika baada ya kuhakiki kazi teule za fasihi kwa misingi ya nadharia ya mwingiliano matini.

#### 4.4.2.1 Ujinasibishaji wa Masuala Ibuka

Hali ya ujinasibishaji wa kazi hizi unaleta masuala ibuka wazi katika ulingo wa fasihi. Ukatili wa viongozi ni jambo ambalo limekuwepo tangu jadi. Waandishi wa fasihi wamekuwa wakilishabikia jambo hili katika kazi zao. Jambo hili linaonekana kuwa tatizo katika historia ya Waswahili kama vile inavyodokezwa katika utendi wa *Fumo Liyongo*. Katika utendi huu, Fumo anaonekana kuwa tisho kwa Mfalme Mringwari jambo ambalo linamfanya Mfalme kupanga njama ya jinsi atakavyomwondoa katika ulimwengu. Baadaye, anamtumia mwanawe Fumo ambaye anamwuliza siri ya nguvu zake. Ukweli unaibuka baada ya Fumo kumwambia kuwa anaweza kufa iwapo atadungwa na sindano ya shaba katika kitovu chake. Baada ya hayo, mwanawe anamwua kwa kumdunga katika kitovu chake.

Jambo hili pia linaletwa wazi katika nyakati za baadaye kupitia uandishi wa Kithaka wa Mberia ambaye analijadili kupitia mauaji ya mhusika Mwelusi. Kwa vile suala hili linaendelea kuwepo katika jamii, mwandishi anachukua nafasi hii kulileta upya kupitia uandishi wa Kifo Kisimani. Mwandishi Kithaka wa Mberia anazua mtazamo mpya wa mauaji ya kijamii ambayo yanadokezwa wazi na kwa njia ya nyakati za kisasa. Mwandishi ametumia uathiriano kuleta dhana hili la ukatili na kwa njia inayooana na jamii ya sasa.

Usaliti uaendelea kutuma viongozi kama njia ya kujidumisha mamlakani. Wazo hili laibuka kwa uwazi kupitia urudufiano unaojitokeza katika tungo hizi. Mwandishi wa Kifo Kisimani anaweka kazi yake katika misingi maalum ya mwandishi wa awali wa utungo wa

Fumo Liyongo. Mwelusi anasalitiwa na nduguye Gege ambaye alikuwa ameahidiwa na kumwowa bintiye Bokono. Hali hii imerudufiwa kutoka kwa utungo wa awali wa Fumo Liyongo jambo ambalo linampa msomaji uwazi katika ufasiri wa utungo huo.

Mwandishi wa baadaye Arege katika uandishi wa *Mstahiki Meya* analeta ujumbe wake kwa njia ya uwazi zaidi katika uandishi wake. Kazi ya Arege inakuwa wazi zaidi inapotazamwa kwa misingi ya mwingilianomatini tukiegemea urudufiano. Suala la usaliti linakuwa wazi zaidi kwa kujaliza matukio ya tungo zote tatu.

Utendi wa Fumo Liyongo umetoa msingi imara wa kimaarifa wa kazi hizi zingine, yaani Tamthilia ya *Kifo Kisimani* na Tamthilia ya *Mstahiki Meya* mtawalia. Utendi wa Fumo Liyongo unazua dhana ya viongozi kutumia mbinu hasi kujidumisha mamlakani. Mfalme Mringwari anatoa wazo hili kwa kupanga njama Fumo Liyongo auliwe ili aendelee kudumu mamlakani. Hii ni kwa sababu Fumo Liyongo anaonekana kuwa tisho kwa mfalme Mringwari kwa sababu ya ushujaa wake. Njama inapangwa na mwishowe Fumo Liyongo anauliwa na mwanawe aliyekuwa ameahidiwa tuzo na mfalme Mringwari.

Hali hii ya uuaji wa viongozi wanaofikiriwa kuwa tisho kwa viongozi walio mamlakani linaendelezwa na Mberia ambaye ana mhusika anayeitwa Mwelusi. Mwandishi huyu anamjenga mhusika Mwelusi kama kiongozi ambaye amepata umaarufu zaidi kama mpiganiaji wa haki za kibinadamu. Suala hili linakuwa wazi zaidi likifumanishwa na maarifa ya nafasi ya mhusika Fumo katika Utendi wa Fumo Liyongo. Fumo Liyongo anazua wazo la ushujaa ambalo linampa mhusika msomaji nafasi ya kumwelewa Mwelusi. Mwelusi anapangiwa njama na viongozi Kame na Bokono ili kuondolewa katika jamii. Mwishowe njama yao inafaulu pale ambapo alikuwaameenda kisimani na nduguye Gege akamchoma kisu.

Ijapokuwa hali hii haijaendelezwa moja kwa moja na mwandishi wa Tamthilia ya Mstahiki Meya, mwandishi anaendeleza wazo hili kwa kumtumia mhusika Siki ambaye ni Daktari katika zahanati ya Cheneo. Mhusika huyu ambaye ana mawazo tofauti na viongozi walio mamlakani licha ya kuwa ni jamaa zake. Mwishowe, mhusika huyu anatemwa katika mipango na mikakati ya kuendeleza jamii. Aidha, katika baraza ambalo limeundwa na madiwani linakosa kuwa na uelewano. Mwandishi anamchora Diwani III kama kiongozi anayepinga uongozi mbaya. Hali hii inampa Diwani wa Tatu nafasi duni katika masuala ya kuiendeleza baraza. Mstahiki Meya anatumia mbinu ya tenga Utawala kumwondoa Diwani III katika kamati ya baraza. Hali hii ianadhihirisha kuwa Diwani III ameuliwa kitaaluma na Mstahiki Meya anayemwona kama tisho. Suala hili la kuuliwa kitaaluma linaeleweka wazi kwa kutazama utungo huu kwa misingi ya mwingiliano matini.

Suala la matumizi mabaya ya nafasi za uongozi mbaya linakuzwa zaidi na kazi hizi kwa njia inayoleta mfumo wa mtiririko wa vitushi. Kwa mujibu wa tungo hizi, suala la uongozi mbaya ni jambo ambalo limekuwa tatizo sugu katika jamii. Suala hili kwa vile limekua tatizo sugu linalozua mchango wa waandishi kwa karibu kila karne, mwandishi amelijadili kwa umakini huku akiliegemeza kwa misingi ya kazi tawalia.

Kwanza kabisa ni katika utungo wa Fumo Liyongo ambao unaibua suala hili kupitia kwa Mfalme Mringwari ambaye anataka kujilazimisha kwa watu kwa njia isiyofaa. Anaonekana kutishwa na mchango wa Fumo Liyongo ambaye amejizolea umaarufu zaidi kwa wanajamii kupitia matendo yake ya kishujaa. Mringwari anadhihirisha uongozi mbaya kwa kuhusika katika kupanga njama ya kumwua liyongo ambaye hakuwa na hatia.

**4.4.3 Usisitizo**

Katika jamii, kuna mambo mengi ambayo huwa yamechukua muda na kuendelezwa katika jamii. Kwa kutumia dhana ya uigaji, watunzi wamepata nafasi murua ya kuendeleza masuala haya. Masuala haya yameweza kuletwa upya kwa jamii na kwa njia inayosisimua kupitia kazi za kifasihi.

Katika utendi, dhana ya kuhujumu watu katika jamii kwa misingi ya kisiasa inaendelezwa na mhusika Mfalme Mringwari ambaye anamshambulia Fumo Liyongo kwa kuwa ana umaarufu mwingi. Aidha, Fumo Liyongo anaepuka mara kwa mara mitego aliyokuwa amewekewa na mfalme Mringwari.

Baadaye Mfalme Mringwari anamtumia mwanawe Fumo Liyongo ambaye anahakikisha kuwa amepata siri ya nguvu za babake. Fumo Liyongo kwa kutojua anampasha ukweli kuhusu siri za nguvu zake. Baadaye, Fumo Liyongo anauliwa na mwanawe kwa kudugwa sindano ya shaba katika kitovu chake. Mfalme Daudi Mringwari anafaulu katika mpango wake wa kummaliza aliyemwona kama tisho la kisiasa kupitia kwa mauaji hayo.

Hali ya kuhujumu viongozi inaendelezwa katika Tamthilia ya *Kifo Kisimani* na mwandishi Kithaka wa Mberia. Hali hii inaashiria kuwa uovu huu unaendelea kukithiri kupitia viongozi wa baadaye. Mtemi Bokono ndiye anachukua nafasi ya Mfalme Mringwari katika kazi hii. Mtemi Bokono anmwona Mwelusi kuwa tisho kwa uongozi wake ambao hauwarithishi watu wa Butangi. Anajaribu awezalo kupitia kwa washauri wake (Batu, Zigu na Kame) kumnasa Mwelusi. Washauri hawa wanafanikiwa kupitia nduguye Mwelusi anayeitwa Gege. Batu anamshauri Gege kumwua nduguye kwa ahadi za kupata mali na kumwoa bintiye Bokono aliyeitwa Alida.

Gege anamwuliza mama aliko Mwelusi na kwa kutojua, Tanya (mamake Mwelusi) anamwambia kuwa Mwelusi ameenda kisimani. Gege anafululiza hadi kisimani alipomkuta Mwelusi. Baada ya kumpata Mwelusi, anamdaganya kuwa ana ujumbe muhuimu na ni vyema waende chemba. Walipoenda chemba Gege anamdunga Mwelusi kisu tumboni na kusababisha mauaji yake. Hali hii ya kuhujumu wapinzani wa kisiasa inaendelezwa katika jamii ya kisasa kwani mwandishi wa *Mstahiki Meya* anadhihirisha hili. Katika tamthilia hii, kiongozi wa jimbo linaloitwa Cheneo anaonekana kugadhabishwa na binamuye anayeitwa Siki. Siki ni daktari katika zahanati iliyopo Cheneo.

Mhusika huyu na maoni tofauti na Meya Sosi kwani Meya Sosi anaongoza Cheneo vibaya kwa kuwanyanyasa Wanacheneo. Katika Hospitali hakuna dawa na watu wengi wamekufa kwa kukosa matibabu. Siki anajitolea kwenda kwa Meya kumwelezea hali ilivyo Cheneo. Meya anakirihishwa na maelezo ya Siki na kumfukuza huku akimwonya asije akarudi tena. Anamwamrisha aione nyumba yake paa maneno ambayo yametumiwa na Mhusika Maksudi katika Riwaya ya S.A. Mohammed ya *Utengano*.

**Meya**: (*Kwa dharau*) Hivyo unaona kuwa uongozi wangu hutaenda mbali?

**Siki**: Sivyo nisemavyo. Ninalosema ni kuwa watu wengi hawajaridhishwa kwa namna mambo yanavyokwenda.

Uk. 12

**Meya**: Hakikisha mtu huyo halikaribii lango kuu kuanzia sasa. Jengo langu alione paa.*Alright*?

**Gedi**: *Yes sir*.

Uk.15 (Mstahiki Meya)

Kama inavyojitokeza katika mazungumzo yao, Daktari Siki anahujumiwa kwa kupinga uovu unaoendelezwa Mstahiki Meya. Meya hajafurahishwa na msimamo wake jambo ambalo linakuza utengano kati yao licha ya kuwa ni njama. Kwa kuweka kazi hizi kwa mizani ya mwingilianomatini, ni dhahiri kwamba hali ya kuhujumu wapinzani wa kisiasa limekuwa donda sugu katika bara la Afrika jambo ambalo linatiliwa mkazo na fasihi katika jamii. Hali hii imejitokeza kwa njia wazi kuwa hili ni tatizo sugu ambalo limekita mizizi katika Afrika Mashariki kama inavyodhihirika katika mawazo ya waandishi hawa. Mbinu ya uigaji imetumiwa kufanikisha wazo hili.

Vilevile, hali hii ya usisitizo inawapa wanajamii mwanga kuwa kuna haja ya kupambana na ukatili unaoendelezwa na viongozi wa kisiasa wanaokiuka maadili ili

kujinufaisha. Aidha, inawaelekeza wanajamii kuwa na msimamo dhabiti wanapotetea haki zao kwani kuhujumiwa kumekuwepo tangu enzi zile na hakuna wakati uovu umewahi kushinda wema kama inavyodhihirika katika kazi zote tatu.

Waswahili husema kuwa, damu ni nzito kulio maji. Aidha, jambo hili limekuwa kinyume katika kazi zote tatu. Katika kazi ya kwanza, Mfalme Mringwari anachukizwa na ndugu yake ambaye ni Fumo Liyongo. Anahofia kuwa huenda ndugu yake akamnyan'ganya ufalme.

Uhasama huu wa kifamilia unaochangiwa na masuala ya kisiasa unadhihirika zaidi katika utendi huo kwani mwanawe Fumo ndiye anayetumiwa kumwua Fumo Liyongo. Mfalme anahakikishia mwanawe Fumo Liyongo kuwa, iwapo angefaulu katika mauaji ya babake basi angemtunuku. Ahadi aliyopewa mwanawe Fumo Liyongo inampandisha mzuka mvulana huyo na kutekeleza mauaji ya babake.

Katika Kifo Kisimani, mhusika Mwelusi anauliwa na mhusika Gege ambaye ni ndugu yake. Gege anamuua nduguye kwa kumchoma kisu tumboni jambo ambalo linawaudhi watu wa Butangi. Mamake Mwelusi alikuwa miongoni mwa waathiriwa kwani hakuamini uhasama uliojitokeza baina ya wanawe.

Hali hizi mbili zinazidi kuibua hisia kali hasa suala la uhusiono uliopo baina ya wanajamii. Ni dhahiri kuwa, kutokana na kazi hizi mbili, fasihi Afrika Mashariki inaweka wazi tamaa kama chanzo cha uhasama miongoni mwa wanajamii. Ufasili huu unatokana na hali za kazi mbili ambapo hali sawa inashuhudiwa.

Mwandishi alitaka kuweka wazi nafasi ya tamaa ya mali miongoni mwa watu katika jamii ya Afrika Mashariki. Mwandishi anaonyesha kuwa, watu katika jamii wanapaswa kuzingatia wazo la kuwa damu ni nzito kuliko maji. Linaonekana kuwa suala ambalo limepuuzwa sana katika jamii na kuwa kuna haja ya kuwa na hisia za kiutu hasa wakati ambapo tunapaswa kufanya uamuzi unaoathiri maisha ya wengine.

Ni hali hii ya tamaa ya mali na umaarufu inadhihirishwa na mhusika Mstahiki Meya katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*. Mwandishi Arege anaibua suala la kuwa viongozi katika Afrika Mashariki wanatawaliwa na tamaa ya umaarufu na mali kuliko kuwa na utu. Hali hii indhihirika wakati Meya Sosi anakanusha madai ya binamuye Siki na kudai kwamba Cheneo itaendelea kumchagua kama kiongozi. Anapuuza wazo la Siki na kuamuru Siki amwondokee kwa kuwa aliwasilisha matatizo ya Wanacheneo kwa Meya. Kazi hii ya Arege inaendelea kusisitiza vile viongozi wanaendelea kuthamini mali na umaarufu kuliko utu, suala ambalo limetiliwa mkazo katika kazi ya awali ya Utendi.

### 4.5 Hitimisho

Sehemu hii imetalii hali ya mwingilianomatini kwa njia ya uathiriano, urudufiano na uigaji katika kazi za fasihi zilizoteuliwa. Imejadili na kutathmini kwa kina hali ya mwingiliano katika kiwango cha msuko, uhusika na wahusika na maudhui. Mifano mahususi imetolewa kuambatana na kauli zilizojadiliwa. Imebainika wazi kuwa kazi ya *Utendi wa Fumo Liyongo*, *Kifo Kisimani* na *Mstahiki Meya* zinaingiliana kwa kuathiriana kwa kiwango cha msuko, uhusika na maudhui.

# SURA YA TANO
# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Katika sura hii mtafiti alishughulika muhtasari wa utafiti huu kwa kuelezea suala la utafiti, malengo ya utafiti, nadharia mwafaka iliyoongoza mtafiti katika utafiti huu, deta iliyofasiriwa na matokeo yaliyopatikana. Matatizo yaliyotokea katika utafiti yameonyeshwa na mapendekezo ya utafiti wa usoni kutolewa.

## 5.2 Muhtasari

Tasnifu hii ina sura tano ambazo zimeelezea utafiti huu katika viwango mbalimbali. Katika utafiti huu, mtafiti amehakiki na kutathmini swala la mwingiliano matini katika tamthilia za *Kifo Kisimani*, *Mstahiki Meya* na Utendi wa *Fumo Liyongo*. Kwa mujibu wa utafiti huu, tumegundua kwamba fasihi huingiliana, kuathiriana na kujalizana katika viwango mbalimbali. Hii ni kauli inayodhihirika kuwa fasihi ni kioo cha jamii na na wasanii huchota malighafi kutoka kwa jamii. Hali hii inasababisha waaandishi tofauti kuwa na kazi zinazolingana na kuathiriana. Vilevile, binadamu ulimwenguni hughasiwa na mambo yanayofanana hali ambayo huchangia katika uathiriano wa matini mbalimbali. Aidha, tumeona kuwa matini hizi tatu zimeandikwa katika vipindi tofauti vya kihistoria hali ambayo inaashiria kuwa maswali mbalimbali ya kijamii yanaendelea kusisitizwa. Uathiriano huu umedhihirika katika kiwango cha msuko, uhusika na maudhui. Uathiriano huu umechangia pakubwa katika ujalizano na uingiliano wa matini hizi tofauti.

Katika sura ya kwanza, mtafiti ameelezea suala la utafiti ambalo ni uchanganuzi ili kudhihirisha ujalizano na mwingiliano katika kazi za fasihi zilizoteuliwa. Katika sura hii, mtafiti ameweza kuonyesha jinsi alipofikia suala hili katika usuli wa mada. Aidha, kwa kuzingatia nadharia ya mwingilianomatini, mtafiti aliweza kupata maswali ya utafiti ambayo yameongoza na dhahiri kwamba maswali haya yote yamejibiwa.

Sura ya pili imezingatia maandishi ya wataalamu mbalimbali ambao wamezungumzia masuala mbalimbali na hasa kuhusu suala la mwingilianomatini. Mtafiti ametalii tasnifu mbalimbali zinazohusiana na kazi yake ili kupata msingi imara wa kuyaweka mawazo yake. Aidha, ameonyesha jinsi tafiti hizo zilivyosaidia katika utafiti huu na kuonyesha pengo la kiusomi ambalo aliazimia kulijaza. Katika sura hii pia suala la nadharia limeshughulikiwa vilivyo na mihimili itakayotumika kuorodheshwa. Kwa kuwa suala la mwingiliano matini ni pana, mtafiti alijikita katika vipengee vitatu vya mwingiliano matini ambavyo ni uigaji, urudufiano na uathiriano.

Mtafiti alitoa dira ya utafiti huu katika sura ya tatu. Katika sehemu hii, mtafiti ametoa muundo wa utafiti ambao ni uchanganuzi wa yaliyomo. Mtafiti aliafikia deta yake kwa kusoma kazi teule za kifasihi huku akiongozwa na vipengee vitatu vya mwingiliano matini ambavyo ni uigaji, urudufiano na uathiriano. Katika utafiti huu, mtafiti alitoa dira ya uchanganuzi na ufasiri wa deta iliyopatikana. Mbinu ya kimaelezo ndiyo iliyoafikiwa kutoa maelezo kuhusu suala la utafiti yatakayojibu maswali ya utafiti.

Uchanganuzi na ufasiri wa deta ndio unaochukua sura ya nne. Sura hii ina sehemu tatu ambazo zinajibu maswali ya utafiti. Sehemu ya kwanza inahusu uathiriano katika kiwango cha msuko urudufiano katika wahusika na uhusika. Katika msuko, mfumo wa kazi za fasihi teule umeangaziwa. Aidha, uathiriano katika kiwango cha msuko umehakikiwa kwa msingi wa vitushi na umantiki. Mtafiti aliwachunguza wahusika hao kwa mujibu wa vipengee vya tabia, wasifu na usawiri wa majina akiongozwa na mhimili wa urudufiano katika mwingilianomatini na kudhihirisha uathiriano na urudufiano uliopo katika kiwango cha wahusika na uhusika katika kazi tatu za kifasihi zilizoteuliwa.

Sehemu ya mwisho katika sura ya nne imeangazia uigaji katika maudhui ya kazi hizo tatu. Imedhihirika wazi kuwa maudhui mahususi yalihitajika kuendelezwa katika sehemu mbalimbali za kihistoria. Maudhui haya yamejadiliwa kama vile mwandishi ameonyesha katika kila kazi mahususi.

Wahusika na uhusika wao uliangaziwa kwani mwandishi hutumia wahusika kufanikisha kazi za fasihi. Wahusika wamengaziwa kwa kuangazia sifa za ndani na sifa zao za nje. Tabia na usawiri wa majina uliangaziwa. Wasifu wa wahusika mbalimbali uliangaziwa na nafasi zao kuonyeshwa.

## 5.3 Hitimisho

Mtafiti aliafiki malengo ya utafiti huu kama yalivyotarajiwa katika sura ya kwanza. Uathiriano umebainika wazi katika msuko na uhusika kati ya kazi ya Utendi wa *Fumo Liyongo*, *Kifo Kisimani* na *Mstahiki Meya*. Urudufiano na uigaji katika maudhui umebainisha kuwa, iwapo kazi hizi ni tofauti, malengo, dhamira, na mafunzo yanayolenga jamii ni yale yale hali ambayo inadhibitisha kuwa kazi teule za kifasihi zinaingiliana. Mtafiti amefanikiwa kutathmni namna uigaji, urudufiano na uathiriano unavyoelekeza kazi ufasiri na utunzi wa kazi za fasihi kama inavyodhihirishwa kwenye sehemu ifuatayo:

### 5.3.1 Mafaniko ya Utafiti

Utafiti huu ulifanikiwa katika kubainisha hali ya ujalizano na mwingiliano uliopo katikakazi teule za kifasihi ambazo ni Utendi wa Fumo Liyongo, *Kifo Kisimani* na *Mstahiki Meya*. Utafiti huu umefanikiwa kuonyesha kuwa ijapokuwa kazi hizi zilizoteuliwa ni tofauti zina malengo sawa na muundo wake ni sawa kama vile imedhihirika katika msuko, uhusika, wahusika na maudhui. Ni bayana kuwa utafiti huu umefanikisha kuelewa kazi za baadaye kwa uwazi zaidi ambazo ni Kifo Kisimani na Mstahiki Meya kwa kutathminiwa kwa misingi ya mwingiliano matini. Mafunzo zaidi yamechipuka zaidi kuhusu maendeleo ya demokrasia barani Afrika kwa mujibu wa Utendi wa Fumo Liyongo, *Kifo Kisimani* na *Mstahiki Meya*. Mathalani, utafiti huu umewapa watunzi wa fasihi dira ya kuendeleza masuala mbalimbali yanayojirudia katika vipindi mbali mbali vya kihistoria bila kuwa na ukinaifu au wizi wa kitaaluma. Mafanikio ya utafiti huu yamezua dhana zilizojadiliwa hapa chini ambazo ziliweza kujengwa.

### 5.3.2 Utathmini wa Utendakazi wa Fasihi

Kazi za fasihi hulenga jamii husika kwa kuangazia masuala ambayo yanapaswa kutiliwa mkazo katika jamii. Hali hii huongozwa na dhamira ambayo mwandishi. Dhamira hiyo huwa ndiyo dira ya kumwongoza mtunzi katika uteuzi wa wahusika, maudhui na mtindo maalum katika kuwasilisha mawazo yake. Dhamira ya mwandishi huelekezwa na masuala nyeti yanayostahili kulengwa katika jamii husika.

Kwa kuegemea kazi nyingine, kazi za fasihi huweza kutathmiana. Kazi za awali hutathminiwa kwa kazi za baadaye ili kujua kwamba malengo ya kazi za awali yameafikiwa. Kwa kutumia kazi ya Mberia, ni dhahiri kuwa kuna musuala ambayo yamedokezwa naye kama njia ya kudhihirisha kuwa malengo fulani yaliyotolewa na utendi wa Fumo Liyongo bada hayajaafikiwa.

### 5.3.3 Jinsi Utendi wa Fumo Liyongo unavyotathminiwa na Tamthilia ya Kifo Kisimani.

Mauaji ya kiholela ni suala ambalo limekithiri katika jamii hasa katika tabaka la kisiasa. Hali hii ni mojawapo ya masuala yanayokashfiwa katika utendi wa Fumo Liyongo. Hali hii ya mauaji ya kiholela yanajitokeza wakati mwanawe Fumo Liyongo anasababisha kifo cha babake bila sababu maalum.

Ijapokuwa katika kazi hii ambayo inaaminika kuwa ni ya karne ya kumi na nane na suala hili limekashfiwa, bado linazidi kuendelea jambo ambalo linampa msukumo mwandishi wa awali kulikashifu. Mberia katika *Kifo Kisimani*, anadhihirisha kuwa bado uozo huu unaendelezwa katika jamii jambo ambalo linampa msukumo wa kulizua upya katika kazi

yake. Katika tamthilia yake, Mberia anamtumia mhusika Mwelusi ambaye ni mpinzani wa Mhusika Bokono aliye kiongozi wa Butangi. Bokono kupitia kwa vikaragosi wake anamwua Mwelusi ambaye anauliwa kisimani na nduguye Gege.

Kazi ya baadaye ya *Mstahiki Meya* inadhihirisha kuwa kuna kupiga hatua katika suala hili kwani ijapokuwa inaathiriwa na kazi tangulizi, mauaji ya kiholela haya ya wapinzani wa kisiasa hayatokei. Hali hii inadhihirisha kukua kwa demokrasia katika Afrika Mashariki ambapo ndio mandhari ya kazi hizi.

### 5.3.4 Kuelekea Ustawi wa Kidemokrasia Katika Jamii ya Kiafrika; Mafunzo kutoka Utendi wa Fumo Liyongo, Kifo Kisimani(2001)na Mstahiki Meya (2009)

Matini hizi tatu zinatupa mwanga wa jinsi jamii ya Kiafrika inavyoendelea kidemokrasia. Cheeseman (2015) anaelezea kuwa, demokrasia katika bara la Afrika ni mojawapo ya masuala changamano. Anaelezea kuwa demokrasia ya bara la Afrika inachukua mtindo wa kihistoria jambo ambalo linawekwa wazi na matini hizi zinapotazamwa kwa mtindo wa kihistoria. Anaendelea kukiri kuwa demokrasia imekuzawa kutoka kiwango kimoja hadi kingine. Mawazo ya Cheeseman yanawekwa bayana na matini hizi.

Kazi hizi zimechapishwa katika vipindi mbalimbali vya kihistoria. Aidha, vimeangazia nyakati tofauti za kihistoria jambo ambalo linatupa mwanga dhidi ya kutathmini ni hatua zipi za kidemokrasia ambazo tumepiga kama jamii. Matini ya kwanza ambayo ni *Utendi wa Fumo Liyongo* inaangazia kipindi cha kabla ya maajilio ya Wakoloni. Wakati huu, kiongozi alikuwa ni Sultan jina ambalo watu wa Mwambao wa Pwani waliwapa viongozi wao.

Sultan ambaye alikuwa ni Mfalme Mringwari anatekeleza unyama dhidi ya ndugu yake Fumo Liyongo kwa kuwa alimwona kama tisho katika uongozi wake. Hali hii inaelezea dhidi viongozi wa zama hizo walinyanyasa wengine ili waendelee kudumu mamlakani. Katika enzi hizi, kiongozi alionekana kama mungu mdogo na hivyo hakuulizwa lolote hata alipowanyanyasa watu.

Hali hii inadhihirika kwani Sultan hata baada ya kumwua ndugu yake hakuna hata aliyemwuliza kuhusu yaliyotendeka. Badala yake, watu walighafilika kuhusu kilichotendeka na badala ya kumuuliza wakamchukia mwanawe Fumo ambaye alihusika kutekeleza mauaji hayo. Hii ni picha mwafaka ya jinsi demokrasia iliweza kunyamazishwa pasipo yeyote kuuliza.

Mambo yanaashiria kubadilika jambo ambalo linadhihirisha ustawi wa kidemokrasia. Katika matini ya pili, demokrasia inachukua mkondo mpya. Hali hii inadhihirika kupitia

uhusiano uliopo kati ya Mzinduzi Mwelusi na mhusika Mtemi Bokono ambaye ni kiongozi wa Butangi. Katika Butangi, Bokono anaendeleza uongozi wa kidhalimu kama vile imejadiliwa katika maudhui. Anatumia nguvu kukabiliana na Mwelusi ambaye anazindua watu dhidi ya kunyanyaswa na Mtemi Bokono.

Ni haki ya kidemokrasia kwa kila Mwanabutangi kupigania haki zake na haki za wenzao kama anavyofanya Mwelusi. Bokono na washauri wake wakuu ambao ni Batu na Zigu, wanapanga njama ya kumkamata Mwelusi. Baadaye wanajiunga pamoja ili kutafuta suluhu la kudumu. Wanafunga Mwelusi gerezani lakini baadaye anatoroka. Baadaye, wanaamua kumnyamazisha Mwelusi kabisa. Katika harakati hizo, wanawatumia makachero ambao wanamshawishi Gege ambaye ni nduguye Mwelusi kutekeleza mauaji hayo. Gege anashawishika na bila shaka kumwua nduguye kwa kumchoma kisu tumboni.

Kwa kutekeleza mauaji ya Mwelusi ambaye ndiye aliyeongoza kikosi cha kuleta mabadiliko Butangi, washauri wa Mtemi pamoja na Mtemi Bokono, walifikiri walikuwa wamekomesha demokrasia kama ilivyo katika matini iliyotangulia. Hali inakuwa kinyume kwani ndio mwanzo wa mwamko mpya na mwisho wa Udikteta. Hii ni kwa sababu, watu wa Butangi waliungana pamoja na kuandamana hadi ikulu. Walipofika ikulu, walimtia mbaroni Mtemi Bokono pamoja na vibarakala wake hali ambayo inaashiria mwisho wa utawala mbaya. Watu wa Butangi wanapata ukombozi kutoka kwa uongozi mbaya, licha ya kumpoteza mwanademokrasia mkuu kinyume na hali ya awali.

Hali hii inaashiria kuwa tumepiga hatua kidemokrasia licha ya kuwa mauaji yaliendelezwa lakini bado ukombozi unapatikana katika awamu za hapo awali. Awamu ya pili ambayoinaashiria kipindi cha muda mfupi tu baada ya uhuru ni ishara tosha kuwa jamii ya Kiafrika inayolengwa na kazi hizi inaendelea kupiga hatua kidemokrasia.

Tamthilia ya Mstahiki Meya inawakilisha kipindi cha kihistoria cha sasa. Katika kipindi hiki, watu wanaelewa sheria kama ilivyo katika katiba. Mbinu wanazokabiliana nazo ni tofauti na mbinu za kijadi. Wanaompiga Mstahiki Meya kwa sababu ya uongozi wake wa kidhalimu ni Diwani III na binamuye Meya anayeitwa Siki. Siki anafanya kazi ya udaktari katika zahanati ya Cheneo. Kwa sababu ya uongozi mbaya, zahanatini hakuna dawa na vifaa muhimu vya kutekeleza matibabu. Jambo hili linamsukuma Daktari siki kuwa na mazungumzo (*dialogue*) na kiongozi wa Cheneo. La kushangaza ni kuwa, Meya anampuuza na kusema kuwa asiwahi rudi nyumbani kwake kwa kumwambia aione nyuma yake paa.

**Meya**: Mwondoe huyu mara moja!

**Siki**: Haina haja kuniondoa. (*Kwa Meya*) Ungeniambia kuondoka ningeondoka tu. (*Anainuka na kuelekea mlangoni. Anaongozana na Gedi. Gedi anapoelekea kuufunga mlango Meya anamwita.*)

**Meya**: Hakikisha mtu huyo halikaribii lango kuu kuanzia sasa. Jengo langu alione paa. *Alright*?

Uk.15 (***Mstahiki Meya***)

Baadaye, mazungumzo zaidi yanaendelezwa na Diwani III ambaye haridhishwi na uongozi mbaya wa Mstahiki Meya. Mara nyingi katika mazungumzo baina ya madiwani na Meya anatumia nafasi hiyo kukabiliana na uovu wa Meya. La kushangaza ni kuwa, Meya anaendelea kuongoza vibaya na kupuuza ushauri wa Diwani III. Badala yake, anawasikiliza wanaomshauri vibaya kama vile Bili na na Diwani I na Diwani II. Mwishowe anajuta mambo yanapoharibika kwa kutomsikiliza Diwani III ambaye pia ndiye bwana Uchumi na Kazi.

**Meya**: Heri ningemsikiliza Bwana Uchumi na Kazi. Manen yake sikuyapenda lakini naona yalikuwa na ukweli fulani.

**Diwani I**: Yaliyopita yamepita. Tugange yajayo.

Uk. 75(*Mstahiki Meya*)

Baada ya mazungumzo kutofua dafu, hali ya kidhalimu inakomeshwa kwa njia ya kidiplomasia. Mstahiki Meya anakosa kuwajibika na hivyo mambo yanaendelea kuharibika vibaya zaidi. Hali hii inazua mtafaruku katika jamii. Mtafaruku huu unaibua hisia za wakuu wa utawala kutaka kujua hasa ni nini kinachoweza kufanywa hili hili kuleta suluhu. Ni katika hali hii ambapo uongozi wa Mstahiki Meya unapofikia kikomoni kwa kuitwa mbele ya makao makuu ambapo inaashiria kuwa hangeweza kuendelea tena kama kiongozi wa Cheneo. Uongozi wa kidhalimu unakomesha kwa njia ya kidiplomasia jambo ambalo linaashiria kuwa tunaendelea kukua kidemokrasia.

**Askari II**: Kweli mambo hujipanga.

**Askari II**: ( Kwa udhabiti). Ndugu Meya, tumetumwa na makao makuu kuwachukua mwende kuelezea mbele hali hii ya mambo.

Uk.79(*Kifo Kisimani*)

### 5.3.6 Mapendekezo

Utafiti huu umejikita katika vipengele viitatu ambavyo ni uathiriano, ujalizano na urudufiano katika mwanda wa mwingilianomatini. Aidha, umeangazia matini za tamthilia za *Kifo Kisimani*, *Mstahiki Meya* na Utendi wa *Fumo Liyongo*. Hivyo basi mtafiti anapendekeza yafuatayo:

- Kazi ya *Kifo Kisimani* na *Mstahiki Meya* zitazamwe kwa msingi wa mwingilianomatini katika viwango vya uhusika, maudhui na msuko.
- Waandishi waangazie upya masuala yanayoendelezwa katika jamii kwa kuzingatia misingi ya kazi za awali ili kuleta upya kwa kazi zao.
- Jamii ya Afika inajukumu la kuikomboa jamii yao kwa kuwa kila hatua inayopigwa inazua mwamko upya katika jamii. Kuna uwezekano wa kuafikia demokrasia Barani Afrika iwapo juhudi za wanajamii hazitasitishwa.
- Kuna haja ya kutathmini nafasi ya mwingilianomatini katika fasihi simulizi katika tanzu mbalimbali za fasihi simulizi.

## MAREJELEO


Abdulaziz M. (1979) *Muyaka 19th Century Swahili Popular Poetry*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Abushiri J. (1985) *Utenzi wa Kumpokea Gavana.* Morogoro. ECOL Publicitions.

Arege T. (2009) *Mstahiki Meya.*Nairobi: Vide-Muwa Publishers.

Ayodi N. (2011) *Tashtiti katika Tamthilia Teule za Kiswahili*; Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Egerton.

Bakari M. (2011) *Usemezano kama Mkakati wa Kufahamu riwaya za Babu Alipofufuka Bin-Adamu* na *Mkusanyiko wa hadithi fupi Sadiki Ukipenda.* Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu Cha Kenyatta.

Bakhtin M. (1990) *The Dialogic imaginations*. University press of manitoba

Bosire T. (2016) *Mwingilianomatini kati ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali na Mstahiki Meya*. Tasnifu ya Uzamili.Chuo Kikuu cha Nairobi.

Bowen. K. (2006) *Uhakiki wa Wahusika Watoto Katika Tamthilia Zilizopendekezwa katika Shule ya Upili*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Egerton.

Buliba A, Gwachi M, na Matinde R. (2014) *Misingi ya Nadharia na Mbinu za Utafiti*. Mwanza: Serengeti Educational Publishers.

Chiraghdin S. (1987) *Malenga wa Karne Moja*. Nairobi: Longman.

Daecon D, Pickering M, Goldging P,na Murdock, G. (1999). *Researching Communications*.Great Britain; Hodder Arnold Headline Group.

Deigner L. (2005) *Intertextuality in the Contemborary Swahili Novel*: Euphrase Kezilahabi’s *Nagona* and William E. Mkufya’s *Ziraili na Zirani*. *Swahili Forum*

Endovu B. (2017*) Mikakati ya upole katika Mstahiki Meya*. Tasnifu ya uzamili, Chuo kikuu cha Nairobi.

Faki M. (2015) *Kuchunguza Sifa za Fani za Utendi wa Kiswahili*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: Dar es Salaam.

Gadavanij S. (2002). *Intertextuality as Discourse Strategy*.School of Languge and Communication.

Ivanic, R. (1998) *Writing and Identity: The Discoursal construction of identity in acadmic*. Amsterdam: John Benjamins publishing Co.

Habel A. (1989). *Intertextuality, Allusion and quotation: An international bibliography of critical studies*. Greenwood Press.

Kamau W. (2015) *Mgawanyo wa Wahusika katika Mstahiki Meya*- Swahili Hub

Kang'e J. (2011) *Mwingilianomatini katika Tamthilia ya Kiswahili*; Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyata.

Kavoi M. (1996) *Uhakiki wa Tamthilia kwa Kuzingatia Ploti, Maudhui, Wahusika na Fani*; Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Egerton.

Kibaara S. (2012). *Matumizi ya Lugha katika Kusawiri Umenke katika Matini ya Utengan*o; Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Egerton.

Kijumwa M. (1913) *Utenzi wa Fumo Liyongo*. IKR: Dar es Salaam.

Kipyegon (2013) *Nafasi dhalishi na dunishi katika Kifo Kisimani na Natala*. Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Kristeva J. (1986) *Intetextuality and reimaging*. Rock wood Press

Kazungu P. (1982). *Ukiushi na Uchimuzi katika Tamthilia Teule.* Tasnifu ya Uzamili.Chuo Kikuu cha Egerton.

Levinson D. (1987) *Theories of Adult Development*. Mc Hill Press

Mansure L. (1982). *Makers of African History*. Essex: Longman.

Massoud S. (2013) *Maudhui ya Fani katika Tamthilia za Kiswahili Mashetani na Kivuli Kianishi*. Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mazrui A. na Syambo, B. (1992). *Uchambuzi wa Fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Mberia K. (2001). *Kifo Kisimani*. Nairobi: Marimba Publishers.

Mecha E. (2013) *Uhalisiajbu Unavyojitokeza katika Ukawafi wa Miraji na Utenzi wa Fumo Liyongo.* Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Merimba (2015*). Uingiliano Matini Katika Filamu za Drama Teule Nchini Kenya*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Meyer J. H. (1998). *Ever After: A study in intertextuality*. Carl Hanser Verlay

Mirikau A. (2010). *Kiswahili kwa Vyuo vya Ualimu*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Mlama P. (1993) Fasihi, *Uandishi na Uchapishaji*. Dar es Salaam: University Press

Mugambi J. M. (1982). *Uhakiki wa maudhui katika Tamthilia za Kiswahili za Kikenya* zilizochapishwa. Tasnifu ya Uzamuli.Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mulokozi M. (1999). *Tenzi Tatu za Kale*.Dar es salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Mulokozi M. (1996) *Utangulizi wa Fasihi*. Tuki Dar es Salaam

Mulokozi M. (1997). *Utenzi wa Nyakiiru Kibi.* Morogoro. ECOL Publicitions:

Mumia J. (2000). *Matumizi ya Mtindo Kuimarisha Muamana.* Tasnifu ya Uzamili., Chuo Kikuu cha Egerton.

Mutua J. (2015) *Fani za Fasihi Zinazoibua Fantasia katika Hadithi za Watoto za Nyambura Mpesha*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Egerton.

Mushengyezi A. (2003). *Twentieth Century Literary Theory.* Kampala: Makerere University.

Musyoka J. (1999). *Uasi katika Tamthilia Teule za Kiswahili*: Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Egerton.

Mwanzi H. (1995). *Matumizi ya Maneno ya Kipekee Kupitisha Mawazo*.Tasnifu ya Uzamili.Chuo Kikuu cha Egerton.

Nduti S. (2000) *Uingilianomatini Katika Filamu za Drama Nchini*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi

Njogu K. na Wafula R. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi.*Nairobi*:* Jomo Kenyatta Foundation.

Njogu K. na Chimerah R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Njoroge H. (2007). *Mwingilianomatini katika riwaya za Tata za Asumini na Rosa Mistika.* Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Ngugi wa Thiong'o na Mugo, M. (1978). Mzalendo Kimathi (Tafsiri). Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Nzuki P. (2003). *Mwingiliano wa Fani na Maudhui katika Ushairi wa Kithaka wa Mberia*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Ochoki J. (2005). *Sitiari, Jazanda na Mwingilianomatini katika Nagona na Mzingile*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Peter A. (2015). *Intertextuality Essay writing by Students in High Schools in Tharaka Nithi* County Kenya. Chuka University. Unpublished thesis.

Senkoro. (2011) *Lugha na Fasihi ya Kiswahili Afrika Mashariki*. TUKI Dar es Salaam . Tanzania

TUKI. (1981). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu:*Dar es Salaam.

Wamitila K.W. (2003) *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi*. Nairobi: Focus Publishers.

Porter J.E (1986). *Intertextuality and the Discourse Community*. Rhetoric review,Fall.

Wamitila K.W. (2006). *Uhakiki waFasihi*: *Misingi na vipengele vyake.* Phoenix Publishers Ltd: Nairobi.

Wamitila K.W. (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingiya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi. Vide-Muwa Publishers Ltd.

Wafula R.M. (1999). *Uhakiki waTamthilia: Historia na Maendeleo yake*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi na Istilahi za Nadharia*. Nairobi: Focus publications Ltd.

Wamitila K.W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi Simulizina Andishi*. Nairobi: Focus publications Ltd.

Wanyama N. (2013). *Matumizi ya Mtindo katika Riwaya za Habwe*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Egerton.

**KIAMBATISHO: YALIYO CHAPISHWA**

1

ARJESS Journal African Research Journal of Education and Social Sciences, 5(2), 2018
ISSN (online): 2312-0134 | Website: www.arjess.org

# Inter-textual Relation between the Epic of Fumo Liyongo, Kifo Kisimani and Mstahiki Meya

Authors: Daniel Kioko Ngunzi[1], AbdulRahim Hussein Taib Ali[2] and Mayaka Gwachi[3]

[1]Egerton University, P.O Box 536, Njoro - Kenya
Department of Literature, Languages and Linguistics
E-mail of the corresponding Author: ngunzidaniel@yahoo.com

[2]Lecturer, Department of Literature, Languages and Linguistics
Egerton University, P.O Box 536, Njoro – Kenya
E-mail Address: husseintaibali@gmail.com

[3]Lecturer, Department of Literature, Languages and Linguistics
Egerton University, P.O Box 536, Njoro – Kenya
E-mail Address: mayakagwachi@gmail.com

**Abstract:** *This paper intended to illustrate pastiche, parody and allusion in the selected texts as well as exposing new information which can only be understood when these texts are interpreted according to the selected theory. The paper focuses on interrelationship of texts in Kiswahili literature in East Africa which touches on allusion, pastiche and parody in interpretation of Kiswahili literature in East Africa. The selected texts that informed this paper included Fumo Liyongo (1950), Kifo Kisimani (2001) and Mstahiki Meya (2009). The epic of Fumo Liyongo is compiled by Mulokozi (1999) in his collection of three epics in the history of the Swahili community. In this paper, the researcher has been able to analyze inter-textual relation at the level of characterization. The paper successfully illustrates how allusion in the selected texts is portrayed and how pastiche and parody is illustrated at the level of characterization of the selected texts. The paper provides a basis on the use of the selected theory to guide interpretation and creation of Kiswahili literature works. The selected theory has guided the study to achieve the set objectives.*

**Keywords:** *Fumo Liyongo Epic, Kifo Kisimani Epic, Mstahiki Meya Epic, interrelationship of texts, Inter-textual Relation*